Nipashe

Jumatano Desemba 4, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580092

www.ippmedia.com

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710



## Auawa kwa kukatwa na jembe shingoni kisa ugomvi 20,000/-

UKURASA 3


siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ninavyoikumbuka siku ya uhuru kijijini kwetu

Ulivyokamilishwa uchaguzi kanda: Chadema ya 'milima na mabonde'

• Ni miezi 11 kuelekea uchaguzi 'baba lao'

Bashir aongezewa vikombe zaidi vya mateso

Miaka 24 ya Moi alivyoitumia 'kuwashughulikia' wasaidizi

UKURASA 13

# Jela miezi 24 kutishia kumuua Rais Magufuli

UKURASA 2



Mtuhumiwa Joseph Lucas (kushoto) ambaye anatuhumiwa kufanya mauaji ya Fadhili Rashidi mkazi wa Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga akiwa chini ya ulinzi wa Polisi. PICHA NDOGO: Mtuhimiwa akiwa na mwenzake mwenye fulana ya njano, Abdallah Shabani ndani ya gari la Polisi. **PICHA: WILLIAM STEPHEN**

## UCHAGUZI NAFASI YA SUMAYE KURUDIWA

UKURASA 3






# Ulawiti, ubakaji vyashika kasi jijini Dar es Salaam

**KILA** siku watu wawili wanabakwa, wanaume wanaopigwa na wake zao wapewa neno...*Endelea ukurasa wa 2*

MICHEZO SAMATTA NJIA NYEUPE EPL UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Afungwa kwa kutishia kumuua Rais Magufuli

**Na Elisante John, SINGIDA**

MAHAKAMA ya Mwanzo ya Ipembe mjini hapa, imemhukumu mkazi wa mtaa wa Minga, Bahati Martin (39), kifungo cha miaka miwili jela baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kutamka maneno ya kwamba atamuua Rais John Magufuli.

Mshtakiwa anadaiwa kuropoka maneno hayo Novemba 26, mwaka huu, huku siku ya pili yake (Novemba 27) Rais Magufuli na msafara wake ukipita mkoani Singida kwa njia ya barabara kwenda Chato.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Yohana Zakaria, alitoa adhabu hiyo juzi baada ya kusema mahakama imetibitisha pasi na chembe ya shaka kwamba mtuhumiwa alitishia kwa maneno hayo, kosa ambalo ni kinyume cha kifungu cha 89 (2) (9) sura ya 16 ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu.

Zakaria alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo katika eneo la kituo kikuu cha mabasi cha zamani mjini Singida, kwenye meza maarufu ya kuuzia magazeti, inayosimamiwa na kijana aliyetajwa kwa jina la John.

Alisema baada ya mshtakiwa kuropoka maneno hayo, mara moja raia wema waliripoti katika kituo kikuu cha polisi askari wa jeshi hilo walifika na kumtia mbaroni.

Kijana huyo aliyefungwa awali alikuwa akijihushisha na kazi ya kuonesha picha, hususani mipira kupitia kibanda stendi hapo.

Hakimu Zakaria alisema baada ya kukamatwa na polisi, alikiri kutamka maneno hayo na hata alipopandishwa kizibani pia alikiri kosa lake.

Pamoja na kukiri huko, lakini alijitetea kwamba alifanya hivyo akiwa na lengo la kutania tu wala hakuwa na lengo la kuua.

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo, Hakimu Zakaria alisema Rais wa nchi ni nembo ya taifa, hivyo mtu anapotishia uhai wake ni sawa na kutishia amani na usalama wa nchi kwa ujumla, hivyo mahakama inamtia hatiani kwa kosa alilofanya.

"Mshtakiwa pamoja na kuwa hujaisumbua mahakama hii inakupa adhabu ya kutumikia jela miezi 24 ili iwe fundisho kwako na wengine wanaokusudia kufanya kosa kama hili. Adhabu hii iwaogopeshe wengine wanaotarajia kufanya makosa ya aina hii," alisema hakimu.

Baada ya hukumu hiyo, mshtakiwa alipelekwa jela tayari kuanza maisha mapya ya kutumikia kifungo chake cha miaka miwili.



Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa David Msuya (kushoto), ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Jukwaa la Maendeleo Kilimanjaro (KDF), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano mkuu wa mwaka wa jukwaa hilo, utakaofanyika mwezi huu. Katikati ni Ofisa Mtendaji mstaafu KDF, Balozi Fadhil Mbaga na Mweka Hazina, Leonard Kisarika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ubakaji, ulawiti vyashika kasi Dar

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema matukio ya ubakaji yameongeza kutoka 608 katika kipindi cha miezi 10 ya mwanzo ya mwaka jana hadi kufikia 719 katika kipindi kama hicho mwaka huu.

Takwimu hizo zinatoa tafsiri kwamba, kwa wastani kila siku, watu wawili wanabakwa katika jiji hilo la kibiashara.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Kamanda Mambosasa alibainisha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Oktoba mwaka jana, matukio ya ubakaji yalikuwa 608 mwaka jana na katika kipindi kama hicho mwaka huu, yalikuwa 719.

"Ulawiti nao umeongezeka kutoka 259 mwaka jana na kufikia 319 mwaka huu, matukio ya wizi wa watoto yamepungua kutoka 12 hadi matukio saba," alisema.

Takwimu hizo za Jeshi la Polisi zinatoa tafsiri kwamba, kila siku kuna tukio moja la ulawiti jijini.

Kamanda Mambosasa alisema matukio ya utupaji wa watoto yamepungua kutoka 17 mwaka jana hadi kufikia 15 mwaka huu.

Alisema kesi za matukio hayo zimeongezeka, akieleza kuwa imetokana na elimu inayotolewa na madawati ya jinsia 25 yaliyoko jijini.

"Kesi 218 zimepelekwa mahakamani. Kati yake, za kubaka zilishinda 27, kulawiti zilishinda 99, kutupa watoto kesi zilizoshinda ni mbili," alisema.

Alisema kesi za ubakaji 19 zilishindwa kutokana na ushahidi hafifu, kesi 12 za ulawiti na mbili za utupaji watoto, pia zilishindwa kutokana na sababu hiyo.

Kamanda Mambosasa alisema kwa mwaka huu, watuhumiwa 298 walikamatwa kwa makosa ya kubaka, 133 kwa kulawiti, wanne kwa kutupa watoto na mmoja kwa wizi wa watoto. Alisema kati ya watuhumiwa waliokamatwa, wanawake ni wanne.

Kamanda Mambosasa aliwataka wananchi katika kipindi cha Siku 16 za Kupinga Ukatili, wafike vituo vya polisi ili kuhudumiwa na kuleta mabadiliko ndani ya jamii.

**WANAUME WANAOPIGWA**

Alisema wanawake na wanaume walioko katika uhusiano, kila mmoja ana wajibu wa kumheshimu mwenza wake ili kuzuia matukio ya ukatili wa kijinsia.

"Na ninyi wanaume, ikitokea umefanyiwa kitendo cha ukatili na mwenza wako, usisite kutoa taarifa," alishauri.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika

INAENDELEA UK 8

## Mnyika adai kumlalamikia Mkurugenzi NEC

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa nne katika kesi ya uchochezi inayowakabili viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), John Mnyika amedai mahakamani kwamba Februari 16, 2018 aliwasiliana na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Ramadhani Kailima, kumlalamikia kuhusu mawakala wa chama chake kunyimwa nakala za barua za usimamizi wa uchaguzi mdogo wa ubunge wa Jimbo la Kinondoni.

Mnyika ambaye ni Mbunge wa Kibamba, alitoa madai hayo wakati akijitetea dhidi ya kesi inayowakabili.

Ushahidi huo umesikilizwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakurugenzi wa Mashtaka Wasaidizi, Faraja Nchimbi, Joseph Pande, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Jaqline Nyantori.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, mshtakiwa huyo wa nne katika kesi hiyo, alidai kuwa Februari 16, 2018 saa tisa alasiri alikwenda viwanja vya Buibui kuangalia maandalizi ya mkutano wa kufunga kampeni kama yalikuwa yamekamilika kwa sababu viongozi wa kitaifa walikuwa wageni katika mkutano huo.

Alidai kuwa, alikuta maandalizi yote yapo sawa kasoro ilikuwa mawakala wao walikuwa hawajapata nakala za barua za usimamizi kutoka kwa msimamizi wa uchaguzi Kinondoni.

"Wabunge wawili wa Chadema, Esther Matiko na Susan Lyimo, walikuwa ofisi za msimamizi Kinondoni tangu asubuhi, nilimpigia Susan alinieleza walifika katika ofisi hizo asubuhi hi kwamba mpaka muda huo wa alasiri walikuwa hawajafanikiwa alinitaka nimpigie Mkurugenzi wa Uchaguzi," alidai na kuongeza.

"Ilipofika saa tisa na dakika zake nilirudi makao makuu nilichukua jukumu la kumpigia mkurugenzi

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Hatima CD ya Zitto kuhusu uchochezi leo

**NaMwandishi Wetu**

HATIMA ya kupokelewa mkanda (CD) wenye picha za video za mkutano kati ya Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo) na waandishi wa habari itajulikana leo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Jana, kesi hiyo ilisikiliza ushahidi wa Jamhuri kutoka kwa Sajenti James, ambaye aliomba kutoa CD hiyo kama kielelezo dhidi ya tuhuza za uchochezi zinazomkabili mbunge huyo. Kesi hiyo inaendelea kusikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi.

Awali, Wakili wa Utetezi, Jebra Kambole, alipinga CD hiyo kwa kuwa shahidi anayetaka kutoa kielelezo hicho hajaeleza ni namna gani video hiyo ilirekodiwa.

Utetezi ulidai kuwa CD hiyo ni ya kielektroniki, hivyo inatakiwa kufuata maelekezo ya sheria inayohusu utoaji wa kielelezo cha kielektroniki inavyotaka.

Alidai CD ambayo inatakiwa kupokewa mahakamani haijarekodiwa na shahidi huyo, hivyo ameshindwa kukidhi matakwa ya kifungu cha 18 (2) (a) cha sheria hiyo ya kielektroniki.

INAENDELEA UK 8



Rundo la takataka likiwa limeterekezwa bila ya kuzolewa kwa muda mrefu kando ya barabara, eneo la Kawe jirani na stendi ya daladala, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha harufu mbaya kwa wakazi wa jirani, pia kuleta magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu. PICHA: MIRAJI MSALA

# Chadema yatangaza kurudia uchaguzi kanda ya Sumaye

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimetangaza kurudia uchaguzi wa kiongozi wa Kanda ya Pwani baada ya aliyekuwa Mwenyekiti wa kanda hiyo, Frederick Sumaye, kupigiwa kura nyingi za hapana.

Alhamisi ya wiki iliyopita, kanda hiyo ilifanya uchaguzi huo, Sumaye akiwa mgombea pekee wa nafasi ya mwenyekiti, akapata kura 28 za ndiyo, 48 za hapana na moja iliharibika. Sumaye, waziri mkuu mstaafu pamoja na Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe, wamechukua fomu za kuwania uenyekiti wa Chadema kuchuana na mwenyekiti wa muda mrefu, Freeman Mbowe.

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene, ilieleza kuwa uchaguzi utarudiwa katika nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani baada ya kanda zote 10 kukamilisha uchaguzi.

"Uchaguzi wa kuwapata viongozi wa ngazi za kanda 10 za chama, uliokuwa ufanyike kuanzia Novemba 28 hadi Desemba Mosi, mwaka huu, ulikamilika rasmi jana (juzi) kwa mujibu wa ratiba, walipatikana viongozi 29," ilielezwa katika taarifa hiyo.

Makene alisema uchaguzi huo ulihusisha nafasi ya uenyekiti wa kanda, makamu mwenyekiti wa kanda na mweka hazina wa kanda.

Nipashe lilimtafuta Sumaye kwa simu kufahamu kama yuko tayari kushiriki tena katika uchaguzi huo ambao hata hivyo, tarehe ya kurudiwa haijawekwa wazi na chama hicho, akasema hana taarifa.

"Sina taarifa hizo za kurudiwa kwa uchaguzi wa kanda, wamesema utarudiwa lini?" alihoji. Hata hivyo, Sumaye hakuendelea na mazungumzo na mwandishi kutokana na kutingwa na majukumu.

Chama hicho pia kimetangaza tarehe ya mchujo wa majina ya wagombea wa nafasi za juu za uongozi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Makene, mkutano wa kuchuja wagombea hao utafanyika Desemba 16, mwaka huu, ukihusisha wagombea wa nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Makene alisema kabla ya kuteua wagombea wa nafasi hizo za juu za uongozi, Desemba 7, mwaka huu, kamati kuu itakutana kufanya uteuzi wa wagombea wa mabaraza ya chama. Alibainisha kuwa wanachama 171 walichukua, kujaza na kurejesha fomu za kuwania uteuzi wa wagombea wa nafasi 109 za uongozi ngazi ya taifa.

"Baada ya shughuli za uchukuaji, ujazaji na urejeshaji wa fomu kukamilika na kuwasilishwa makao makuu ya chama, kazi ya kuzichambua fomu tayari imeanza kuelekea vikao vya chama vitakavyoketi kwa mujibu wa taratibu za uchaguzi za uchaguzi mkuu wa ndani ya chama," alisema.

Taarifa hiyo ya Makene ilikuwa na majina ya waliotia nia kugombea nafasi zote za uongozi ndani ya chama, isipokuwa majina ya wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Chadema taifa.

Chama hicho kilichoanzishwa rasmi Mei 28, 1992, kinatarajiwa kufanya uchaguzi wa viongozi wa ngazi za juu Desemba 18, mwaka huu.

# Auawa kwa kukatwa na jembe shingoni

**Na Steven William, MUHEZA**

MTU mmoja aliyekuwa akifanya kibarua cha kulima Fadhili Rashidi (35), ameuawa kinyama kwa kukatwa na jembe shingoni.

Tukio hilo limetokea usiku wa kuamkia jana katika kitongoji cha Mgombezi, kijiji cha Mafere, kata ya Mkuzi wilayani Muheza ambako alikuwa anaishi.

Ofisa mtendaji wa kata ya Mkuzi, wilayani Muheza, Japhet Hayule, alisema mtuhumiwa wa mauaji hayo ni Joseph Lukas, ambaye alikuwa akiishi nyumba moja na marehemu, wote wakiwa wanafanya vibarua vya kulima.

Akizungungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa kitongoji cha Mgombezi, Athumani Hamisi, alisema vibarua hao mtuhumiwa na (marehemu) walipita nyumbani kwake saa saba usiku wakiwa wameongozana wakienda wanakoishi huku wakiwa wamelewa, lakini walikuwa wakigombana kwa kudaiana Sh. 20,000.

Alisema kuwa asubuhi walipata taarifa juu ya tukio hilo na yeye alitoa taarifa kwa mtendaji wa kijiji, Victoria Masanja, ambaye naye alitoa taarifa kwa mtendaji wa kata ya Mkuzi, Japhet Hayule.

Kufuatia tukio hilo Jeshi la Polisi wilayani Muheza linawashikilia watu watatu kutoka eneo hilo kwa uchunguzi zaidi ambao ni Lukas, Abdallah Shabani na Shabani Athumani.

Kaimu mkuu wa upelelezi wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Muheza, aliyeomba jina lake lisitajwe gazetini aliwataka wananchi kutofumbia macho matukio kama hayo na kwamba wakiwaona watu hawaeleweki wanajihusisha katika matumizi ya dawa ya kulevya ikiwamo mirungi, bangi, madawa ya kulevya na pombe haramu ya gongo watoe taarifa kwa viongozi wao kwa kuwa hiyo ndio inaleta watu kufanya mauaji.

Alisema kuwa Jeshi la Polisi wilayani Muheza litaanza msako katika vijiji vyote wilayani humo kwa ajili kukamata madawa ya kulevya ikiwamo bangi, mirungi, pombe ya gongo huku akiwataka maofisa watendaji kuwafichua vijana wanajihusisha na vitendo hivyo wakamatwe. Mwenyekiti wa kijiji cha Mafere, kata ya Mkuzi wilayani Muheza Haji Athumani, alisema vijana ndiyo wako mstari wa mbele kwa kutumia madawa ya kulevya.


## KUMBUKUMBU



***THOMAS MGANTE ALI TUKAI***

Ni mwaka moja leo tangu ulipoitwa mbinguni kwa Bwana. Tunaamini hujatuacha. Kiroho uko nasi kila wakati na kila mahali. Tunakupenda sana!

Unakumbukwa sana na Mama mpenzi Illuminata, kaka Mavere, dada Rehema, dada Faraja pamoja na ndugu jamaa na marafiki wote.

**Kutakuwa na Misa ya kusherehekea zawadi ya uhai wako nyumbani kwa familia ya Tukai Kibamba tarehe 14/12/2019 kuanzia saa kumi jioni.**

**Wote mnakaribishwa.**

# Jafo awapa majukumu viongozi Chamwino

**"Mkuu wa wilaya pamoja na timu yako ya ofisi ya mkurugenzi hakikisheni kuwa vifaa vyote vinapatikana mkandarasi asipate shida ili kukamilisha ujenzi huu katika kipindi kilichopangwa na mimi nitakuwa napita muda wote kukagua," alisema.**

**Na Paul Mabeja, CHAMWINO**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameutaka uongozi wa Halmashauri ya Chamwino mkoani Dodoma kusimamia upatikanaji wa vifaa vya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru kila hatua ili ikamilike kwa wakati uliopangwa.

Jafo alitoa maagizo hayo jana alipotembelea kukagua eneo jipya ambalo litajengwa hospitali hiyo kwa kutumia fedha zilizotolewa na Rais John Magufuli ambazo zingetumika katika sherehe za maadhimisho ya Siku Uhuru wa Tanganyika Desemba 9, mwaka jana.

Aidha, alisema serikali imeamua kuhamisha ujenzi wa hospitali hiyo kutoka enao ambalo Rais aliweka jiwe la msingi, kutokana na umbali uliokuwapo mpaka eneo la barabara kuu ya Dodoma-Morogoro.

Jafo alisema lengo la hospitali hiyo ni kusaidia watu ambao watapata ajali katika barabara hiyo, hivyo kuijenga umbali ambao ilikuwapo awali hakuta kuwa na tija.

"Lengo la hospitali hii kujengwa ni kwa ajili ya kusaidia wale wanaopata ajali, wanaopata dharura za kuzidiwa wakiwa barabarani wapate huduma katika maeneo ya jirani, hivyo kule ambako tuliweka awali ni zaidi kilomita tatu kutoka barabara kuu," alisema Jafo.

Kutokana na hali hiyo, Jafo, aliwaagiza viongozi wa Wilaya ya Chamwino ambako hospitali hiyo inajengwa kuhakikisha vifaa kwa ajili ya ujenzi huo vinapatikana muda wote ili ujenzi ukamilike kwa wakati.

"Mkuu wa wilaya pamoja na timu yako ya ofisi ya mkurugenzi hakikisheni kuwa vifaa vyote vinapatikana mkandarasi asipate shida ili kukamilisha ujenzi huu katika kipindi kilichopangwa na mimi nitakuwa napita muda wote kukagua," alisema.

Mkandarasi wa ujenzi wa hospitali hiyo kutoka Suma JKT, Omary Jafari, alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika Mei 25, mwakani kwa gharama ya Sh. bilioni 3.99.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo (kulia), akihojiwa na Mtangazaji wa EATV/Radio, Ian Dialo, jijini Dar es Salaam, katika kampeni ya "Kibiashara Zaidi" inayoendeshwa na EATV/Radio, ambapo alieleza kuwa wao kama Yara wanahakikisha wakulima wanapata mazao ya kutosha na wanafaidika kiuchumi. **PICHA: EATV/RADIO**

# Lukuvi awavaa wakurugenzi hati ardhi

**Na Munir Shemweta, IRINGA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewataka wakurugenzi wa halmashauri kuanza kujitathmini katika idadi ya hati wanazotoa kwa wamiliki wa ardhi kwenye halmashauri zao.

Lukuvi alisema hayo jana katika mkutano wake wa kusikiliza na kutatua kero za ardhi kwa wananchi wa Mkoa wa Iringa kupitia programu ya 'Funguka kwa Waziri', uliyofanyika ukumbi wa Siasa ni Kilimo mjini hapa.

Alisema wizara yake itaanza kutangaza wilaya itakayoongoza katika upangaji, umilikishaji na utoaji hati za ardhi kwa wananchi ili kubaini hamashauri ambazo ziko nyuma katika kutoa hati za ardhi kwa wananchi.

''Mkurugenzi ajione fahari kuwawezesha wananchi kwa kupima na kuwapatia hati. Kama mkurugenzi huwezi kutoa hati miliki hata 100, basi wewe hufai," alisema.

Kwa mujibu wa Lukuvi, kumilikisha na kumpatia mwananchi hati ya ardhi ni kumwezesha kiuchumi kwa kuwa anaweza kuitumia kwenye shughuli za kimaendeleo na kusisitiza kuwa wakurugenzi wa halmashauri wahakikishe wanapanga na kuwamilikisha maeneo wananchi.

Lukuvi pia alisema kwa sasa wizara yake imejipanga kuhakikisha inasogeza huduma za ardhi karibu na wananchi kwa kuanzisha ofisi za mikoa zitakazokuwa na watendaji wote wa sekta ya ardhi kama vile wapimaji, wathamini, wataalamu wa mipango miji na wasajili.

''Sasa wapimaji, wathamini na wapangaji watakuja hapa Iringa. Muundo unaanza mwezi ujao lengo ni kuwapunguzia usumbufu wananchi katika kupata huduma za ardhi," alisema.

Waziri alisema katika kuboresha huduma za sekta ya ardhi, wizara yake itatumia mifumo unganishi itakayorahisisha utendaji kazi kwa wataalamu wa sekta ya ardhi. Kazi kubwa, alisema itakuwa ikifanyika kielektroniki badala ya kutumia makaratasi aliyoaeleza kuwa wakati mwingine husababisha tamaa kwa maofisa ardhi.

Alitolea mfano Mkoa wa Dar es Salaam kuwa umeshaanza kutumia mfumo unganishi na sasa wamiliki wa ardhi katika mkoa huo wanapatiwa hati za kielektroniki na kubainisha kuwa lengo la kuwa na mfumo unganishi ni kuondoa urasimu na kurahisisha utendaji kazi.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alisema mkoa wake umejitahidi kupunguza kero na migogoro ya ardhi iliyokuwapo miaka ya nyuma kwa kuanzisha utaratibu wa kuwafuata wananchi kwenye maeneo yao kupitia programu ya Iringa Mpya.

Alimweleza Waziri Lukuvi kuwa, kama angekuja mwaka mmoja na nusu uliopita, basi ukumbi aliofanyia mkutano wa 'Funguka kwa Waziri' ungekuwa umejaa wananchi wenye kero lakini jitihada za mkoa wake zimesababisha mkutano huo kutokuwa na idadi kubwa ya wananchi wenye migogoro ya ardhi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.



## HABARI KITAIFA



Gari lenye namba za usajili T 439 CVD, likiwa limetumbukia kwenye mtaro wa maji ya mvua, baada ya kumshinda dereva wake, katika Barabara ya Sewa, eneo la Mikocheni Viwandani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Shida maji yawaamsha usiku wa manane

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WAKATI Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Morowasa) ikipandisha ankra ya maji kwa matumizi ya nyumbani kutoka 1,070 hadi 1,600 kuanzia Desemba Mosi mwaka huu, baadhi ya wananchi wa maeneo kadhaa wamelalamikia kukosekana kwa huduma hiyo.

Baadhi ya wananchi waliolalamikia kukumbwa na adha hiyo ni Mazimbu Relini, Modeko, Area 5, Kichangani kwa Mchuma, Maghofa ya Reli, Mfalme Sulemani na Kilakala. Wananchi hao wamedai kukosa huduma hiyo kwa zaidi ya wiki mbili sasa.

Kwa mujibu wa wananchi hao, wamekuwa wakiamka saa 9:00 usiku hadi 10:00 alfajiri kusaka maji, huku baadhi wakisema wamekuwa wakipata mara mbili kwa wiki au kutopata kabisa.

"Kwa kweli tumekuwa tukipata sana adha ya maji. Tunaacha vitanda saa 9:00 au saa 10:00 alfajiri kulingana na umbali kusaka maji na wakati mwingine tunarejea nyumbani saa 1:00 au 2:00 asubuhi," alisema Jalia Kavindi, mkazi wa Mazimbu Relini.

Ndaki Mosha, mkazi wa Modeko, alisema wanashangazwa na Moruwasa kutangaza kupandisha bei ya maji kupitia matangazo mbalimbali yanayorushwa katika vyombo vya habari wakati hakuna huduma hiyo.

Alisema katika eneo hilo, hakuna huduma ya maji kwa wiki mbili sasa na kulazimika kununua maji kwa watu wanaoleta na maboza kwa kuuza kwa Sh. 100 kwa ndoo.

"Tunashangazwa na Moruwasa kupandisha bei ya maji, huku kwa wiki mbili sasa maji hatuyaoni. Wanapopandisha gharama kuendane na upatikanaji wa huduma," alisema Mosha.

Naye Mtumwa Marcus, mkazi wa Area 5, alisema kwa muda mrefu wana tatizo la maji lakini wanashangazwa na ankra za maji zimekuwa zikiletwa kila mwezi licha ya kufikisha malalamiko hayo katika ofisi za Moruwasa na kushindwa kupatiwa majibu.

Andrew Kimaro, mkazi wa Kilakala alisema tatizo la maji katika eneo hilo kwa sasa limekuwa sugu na kulazimika baadhi ya watu kutumia maji ya mito yanatokana na mvua zinazoendelea kunyesha mjini Morogoro.

Akizungumzia tatizo hilo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Moruwasa, Mhandisi Tamimu Katakweba, alisema tatizo la baadhi ya maeneo kukosa maji linatokana na miundombinu katika maeneo hayo kuwa katika hali ya uchakavu na kuhitajika kufanyiwa ukarabati mkubwa ili kurudisha huduma hiyo.

Katakweba alisema Moruwasa imeshapata Sh. bilioni 180 kutoka Shirika la Maendeleo la Ufarasa kwa ajili ya kuboresha miundombinu na ujenzi wa matangi mapya katika maeneo yote kwa sasa yenye matatizo ya maji na tayari mtaalamu mshauri ameshapatikana.

Kaimu mkurugenzi huyo alisema wataalamu wengine wameshaanza kutafuta vyanzo vya chini vya maji kwa ajili ya kusaidia maeneo mengine ambayo hayajafikiwa na mtandao huo na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu.

# Mfumo wadhibiti mimba gerezani

**Na Joseph Mwendapole**

MFUMO madhubuti uliowekwa katika magereza mbalimbali nchini umefanikisha kudhibiti mimba kwa wafungwa na mahabusu.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Magereza nchini, Amina kavirondo, kwenye kikao cha siku mbili cha tathmini ya Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

Mkutano huo ambao ni mwendelezo wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zilizozinduliwa hivi karibuni mkoani Dodoma, umebeba kaulimbiu 'Kizazi Chenye Usawa: Simama Dhidi ya Ubakaji'.

Amina alitoa ufafanuzi huo wakati akijibu hoja ya mjumbe wa mkutano huo aliyedai kuwa kuna wanawake wanapata mimba wakiwa magerezani.

Alisema kutokana na udhibiti huo haijawahi kutokea hata siku moja mahabusi au mfungwa akapata ujauzito akiwa kwenye gereza lolote nchini.

"Hakuna wakati ambapo kwenye gereza lolote Tanzania mfungwa au mahabusi aliwahi kupata mimba. Nina miaka 24 kazini nazungumza kitu ambacho ninauhakika nacho haijawahi kutokea na haiwezi kutokea kama mnavyodhani," alisema.

Alifafanua kuwa mfungwa anapoingia gerezani siku ya kwanza anapimwa vipimo vingi ikiwamo ujauzito kama ni mwanamke na iwapo atabainika kuwa na mimba taarifa huwasilishwa kwa viongozi wote wa juu wa jeshi hilo.

Amina alisema kama mfungwa wa kike ataingia gerezani akiwa hana ujauzito hawezi kuupata akiwa ndani kwa kuwa wameweka utaratibu mzuri ambao hakuna nafasi kwa mfungwa huyo kuonana na mwanaume awe askari wa kiume au mfungwa wa kiume.

Akifungua mkutano huo, Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Ofisi ya Rais Tamisemi, Mwajina Lipinga, alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa asasi zisizo za kiserikali katika utekelezaji wa Mtakuwwa.

Alisema wakati serikali ikiandaa mpango huo ilishirikisha asasi binafsi hivyo utekelezaji wake unahitaji ushirikiano wa pande zote mbili ili kufikia malengo yake mwaka 2022 ya kupunguza ukatili huo angalau kwa asilimia 50.

Aliipongeza WiLDAF kwa namna inavyoratibu mashirika 63 kwenye utekelezaji wa mpango huo na kwamba hiyo ni dalili njema kuwa jukumu hilo halijaachwa kwa serikali pekee.

Mkurugenzi wa WiLDAF, Anna Kulaya, alisema mkakati huo ni matokeo ya kazi kubwa ya ushawishi wa asasi binafsi baada ya kuona matukio ya ubakaji na unyanyasaji wa wanawake na watoto umeshika kasi.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi nne duniani zinazotelekeza mpango wa Mtakuwwa na kwamba baadhi ya nchi zitakuja kujifunza namna ilivyofanikiwa kuutekeleza na changamoto zake.

"Mpango huu usipofanikiwa haitaangaliwa serikali bali itaangaaliwa nchi hivyo sisi wadau wa asasi binafsi lazima tukae pamoja tuseme wapi tumefanikiwa na wapi kuna changamoto," alisema.


**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**MNADA WA UUZAJI WA VIWANJA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la uuzaji wa Viwanja kwa njia ya Mnada litafanyika tarehe **14 Disemba, 2019** siku ya Jumamosi. Mnada utafanyika katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 4:00 Asubuhi.

Viwanja vinavyouzwa ni Maeneo ya:

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| IYUMBU (New Town Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Viwanda Vidogo |
| NALA (Industrial Area) | • Viwanja vya Viwanda vya aina mbalimbali |
| NJEDENGWA (Investment Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara |
| NZUGUNI (Jirani na Uwanja wa Mpira, Soko Kuu na Stendi kuu mpya ya mabasi) | • Viwanja vya Hoteli<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Maduka makubwa (Shopping Malls) |

**NB**:

- Asilimia 50 ya Malipo italipwa siku ya Mnada
- Asilimia 50 inayobaki italipwa ndani ya siku 14 baada ya Mnada.

Tangazo hili limetolewa na:
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Halmashauri 16 zichukue hatua kujinusuru na njaa

TAARIFA kwamba halmashauri takribani 16 nchini zina upungufu wa chakula, zinapaswa kuchukuliwa kwa uzito wa pekee.

Imeelezwa kuwa taarifa hizo zimebainishwa na tathmini ya hali ya chakula iliyofanywa na Wizara ya Kilimo katika maeneo kadhaa nchini, huku serikali ikisema imejipanga kukabiliana na changamoto hiyo.

Halmashauri hizo zimetajwa ni Kongwa, Mpwapwa, Chamwino, Bahi (Mkoa wa Dodoma); Simanjiro Mkoa wa Manyara); Longido (Mkoa wa Arusha na Musoma (Mkoa wa Mara). Nyingine ni Same na Mwanga (Mkoa wa Kilimanjaro); Rorya (Mkoa wa Mara); Manyoni (Mkoa wa Singida); Kishapu na Shinyanga (Mkoa wa Shinyanga); Korogwe na Mkinga (Mkoa wa Tanga) na Nzega (Mkoa wa Tabora).

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu na Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kanali Matamwe Said, wakati akifungua mafunzo ya wataalamu wa uchambuzi na tathmini ya usalama wa chakula na lishe nchini (Mchali) wiki iliyopita mkoani Morogoro.

Alisema kila mwaka Wizara ya Kilimo imekuwa ikitoa taarifa ya hali na usalama wa chakula nchini na kwa mwaka huu tathmini hiyo awali ilifanywa kwenye halmashauri 46 ambazo zilikuwa na viashiria vya upungufu wa chakula hata hivyo, baada ya mvua kunyesha halmashauri 16 ndizo zilionekana bado zina chagamoto ya uhaba wa chakula.

Alivitaja vigezo vilivyotumika katika kufanya tathmini ya hali ya chakula kwa halmashauri hizo 16 zenye changamoto ya chakula ni kuangalia upatikanaji wa chakula, soko na usalama wa chakula.

Mkurugenzi huyo alisema tathmini hiyo ililenga kujua sababu za halmashauri hizo kuwa na upungufu wa chakula ili kuangalia namna ya kukabiliana na changamoto hiyo.

Ni jambo jema na lenye tija kwa Wizara ya Kilimo kuwa na utaratibu wa kufanya tathmini ya hali ya chakula na usalama wa chakula, kwa kuwa inasaidia kujua hali halisi ilivyo katika maeneo yote nchini.

Tunalisema hili kutokana na miaka ya nyuma kukosekana kwa takwimu za usalama wa chakula hususan wanasiasa kuficha ukweli pale maeneo yao ya kiutawala yanapokuwa na upungufu wa chakula.

Kutokana na serikali kuwabana wakuu wa wilaya na mikoa kuwa wahakikishe maeneo yanakuwa na chakula kwa kuhimiza wananchi kuzalisha, imekuwa vigumu kwao kueleza hali ya chakula, kiasi kwamba wakati mwingine hata kama maeneo yao yana njaa, hawasemi ukweli kwa kuogopa kutumbuliwa.

Ikumbukwe kwamba miongoni mwa vigezo vya viongozi hao kuendelea kuwa madarakani ni maeneo yao kujitosheleza kwa chakula.

Baada ya tathmini hii, viongozi wa halmashauri 16 zilizotajwa kuwa na upungufu wa chakula wakiwamo wakurugenzi, wakuu wa wilaya na mikoa hawanabudi kuchukua hatua haraka kabla hali haijawa mbaya.

Miongoni mwa hatua za kuchukua ni kuwahimiza wananchi wao walime mazao ya muda mfupi, ambayo pia yanavumilia ukame. Hii ni kwa kuwa serikali imeshasema na imeendelea kusisitiza kuwa haitatoa fedha kwa ajili ya kununulia chakula kwa maeneo ambayo yatakuwa na uhaba wa chakula.

Tunaelewa jinsi mabadiliko ya tabianchi yanavyosababisha athari nyingi ikiwamo ukosefu wa mvua kwa muda mwafaka na wakati mwingine kusababisha mafuriko, hivyo kuharibu mashamba na mazao.

Tunashauri halmashauri zetu kuwatumia wataalamu wa kilimo kuelimisha wakulima kulima kwa kutumia mbinu za kisasa za kilimo himilivu ambacho kinaweza kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ili pamoja na mambo mengine, kuwapo na chakula cha uhakika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mary Geofrey

# Siku za kupinga ukatili ziripoti rushwa ya ngono

**RUSHWA** inatafsiriwa kuwa ni matumizi mabaya ya mamlaka ili kujinufaisha na kujipatia maslahi binafsi.

Miaka ya nyuma rushwa zilizokuwa zimekithiri ni zile zilizotolewa ili kupata stahili iwe kazini, kwenye huduma muhimu na hata ili kupata upendeleo kwenye siasa.

Zama hizi kumekuwa na kukithiri kwa rushwa ya ngono, ambayo imekuwa mwiba mkali kwa wanawake.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, George Mkuchika, akiwa bungeni mwaka huu, wakati wa bajeti, anakiri wazi kuwa rushwa bado ni tatizo kitaifa licha ya jitihada zinazoendelea katika serikali ya awamu ya tano.

Anasema rushwa ndogondogo ndiyo mwiba kwa Watanzania wengi kwa kuwa inawagusa wanyonge moja kwa moja huku akitaja ya ngono kwamba inaendelea kutamalaki katika maeneo mengi hususani kazini.

Analiambia bunge kuwa mapambano dhidi ya rushwa sharti yaangalie kundi la chini na nguvu ielekezwe huko baada ya upande wa juu kuonyesha mafanikio.

Kundi kubwa ambalo linakutana na changamoto hiyo ni wanafunzi wa vyuoni na kumekuwa na tuhuma kuwa baadhi ya wanavyuo wa kike wanalazimika kutoa rushwa ya ngono ili waweze kufaulu masomo yao.

Wahadhiri nao wanalaumiwa kwa kuwanyanyasa kijinsia wanafunzi wa kike kwa kutaka ngono au kuwajengea mazingira ya kuwataka kimapenzi kwa nguvu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wa kike vyuoni nao wanalaumiwa kwa kutumia jinsia yao kama kishawishi cha kuwategea wahadhiri wa kiume kwa lengo la kupata alama bora.

Upatikanaji wa taarifa kamili kuhusu rushwa ya ngono ni tatizo kubwa kutokana na jambo hilo kuonekana kuwa la usiri katika jamii.

Mkurugenzi wa Mfuko wa Uhifadhi Wanawake Tanzania (WFT), Mary Rusimbi, akiwasilisha mada katika kongamano la kujadili masuala ya rushwa ya ngono ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, anasema utoaji taarifa ni tatizo.

Kongamano hilo liliandaliwa pia na Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) na mabalozi wa nchi za Ireland na Uholanzi likiwa na kaulimbiu 'kataa rushwa ya ngono jenga kizazi chenye usawa'.

Rusimbi anasema ni vema mapambano ya rushwa ya ngono kuongozwa na utafiti ili kujua ni wapi wanaweza kuanzia katika kupambana na rushwa hiyo ambayo ni jambo la kikatili.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), katika kushughulia tatizo hili imeanzisha elimu na kitengo cha kushughulika na rushwa za ngono.

Lengo ni kuhakikisha tatizo hili linapungua kama si kumalizika kabisa ndani ya jamii zetu na taifa kwa ujumla.

Vyanzo vya rushwa ya ngono vinavyotajwa ni mmomonyoko wa maadili, tamaa za mwili, kutokujua haki na wajibu, kutojiamini kutokana na kukosa sifa na kama za kupata au kujihakikishia huduma haraka.

Katika muktadha huo wanaothirika na rushwa ya ngono ni wanawake, wanafunzi na watumishi wa ngazi za chini.

Athari ambazo zinatokana na rushwa hii ni ukiukwaji wa haki za binadamu, ukiukwaji wa utawala wa sheria na taratibu za kazi na kuajiriwa watu wasiyo na sifa.

Aidha kunazorotesha utendaji kazi wa taasisi, kupatikana kwa wasomi wenye uwezo duni, kukatisha masomo hasa kwa wasichana wa shule na vyuo.

Kadhalika kumekuwapo na kuongezeka kwa maambukizi ya magonjwa ya ngono hasa Ukimwi, mimba zisizotarajiwa hali inayochangia kuongezeka kwa watoto wa mitaani.

Kutokana na madhara hayo kuna kila sababu ya kila muhusika kujiepusha na rushwa ya ngono kwa sababu zozote zile kwa sababu kwanza unalinda heshima na utu.

Pia kunasaidia kuwajengea ujasiri wanawake wasiendelee kukubali kudhalilika na haki kutolewa kwa usawa.

Ili kuondokana na changamoto hii ambayo imetawala maeneo mbalimbali nchini, jamii inapaswa kutofumbia macho vitendo hivi.

Waathirika hawana budi kuwa mstari wa mbele kukemea na kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola ikiwamo Takukuru.

Takukuru inapokea taarifa nchi nzima kwa walalamikaji kupiga simu ya bure namba 113.

# BARUA & MJADALA

## Takataka zinatupwa kila mahali

***MHARIRI***

*NITOE kilio changu kwa serikali kupitia kwako. Sisi wakazi wa maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam tumekuwa na matatizo ya kutupiwa takataka nyumbani kwetu kila wakati.*

*Kila mara ukiamka unakutana na viroba vya takataka zinazotupwa ama kwenye mlango wa kuingilia nyumbani, kwenye ukuta wa ua, au hata uwanjani.*

*Tunaziomba mamlaka za halmashauri kuona shida yetu na kutusaidia kwa kupanga utaratibu wa kuzoa takataka mitaani. Mbona viongozi wanajisahau.*

***Mkazi wa Kawe- Ukwamani***
***Dar es Salaam**.*

## Kufungua mbolea muda mrefu kunaipunguza nguvu?

***ASALAMU Alyeikum Mhariri.***

*Mimi ni mkulima na mara nyingi natumia mbolea, lakini sijafahamu ukweli kuhusu uuzaji wa pembejeo hii.*

*Naomba kuwauliza wataalamu mbolea ya chumvi chumvi ikifunguliwa muda mrefu bila kufunikwa si inapungua nguvu? Kama jawabu ni ndiyo kwanini serikali isitengeneze mazingira ya mbolea hiyo kupimwa kwenye vipimo vidogo kuuzwa kwa utaratibu unaoeleweka?*

*Ikumbukwe mara nyingi nimekuwa nikiuziwa mbolea hii lakini sioni kuwa inarutubisha mazao yangu. Nitoe mfano wa DAP.*

*DAP inayoaminika kunenepesha mazao haijawa na tija kwa wakulima wengi.*

*Ndiyo maana pamoja na kuomba ufafanuzi huo, tunaomba pia serikali itusaidie kupata maofisa ugani jijini Dar es Salaam kwani kuna wakulima na wafugaji wengi.*

***Barnabasi Lukwalo***
***P.O.BOX 1577***
***Dar es Salaam.***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Halmashauri zinazosuasua kuhama zinajikwamisha

**Na Sabato Kasika**

HIVI karibuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliagiza halmashauri zenye ofisi nje ya maeneo ya utawala kuhama mara moja na kuonya kuwa zitakazopuuza zitafutwa.

Baadhi ya halmashauri, ambazo zilikuwa zinafanyakazi nje ya maeneo ya utawala ni Halmashauri ya Musoma mkoani Mara, ambayo baada ya agizo hilo, ilihamia kwa muda Mugango.

Hatua ya kuhamishwa kwa halmashauri hizo inatokana na Rais John Magufuli kubaini kuwa nyingi hazifanyi kazi katika maeneo yao ya utawala na kusababisha utoaji wa huduma kwa wananchi kusuasua, lakini umbali ulikuwa chanzo cha kuongeza gharama za uendeshaji.

Aidha, ilibainika kuwa mkurugenzi wa halmashauri zilizo nje ya eneo la kazi, hutembea kilomita takribani 95 kwenda na kurudi ili awahudumie wananchi wakati kama angekuwapo karibu na wananchi, adha zote wanazopata zisingekuwapo.

Uamuzi huo wa kuhamishwa kwa halmashauri umepongezwa na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, ambaye anasema usumbufu kwa watumishi wa kusafiri umbali mrefu utakuwa umepungua.

Anasema, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma makao makuu yake yalipangwa kuwa eneo la Kata ya Murangi, karibu kilomita 56 kutoka Musoma Mjini. Hata hivyo, wafanyakazi wote walikuwa wanaishi mjini na mara chache wanatembelea wananchi huko vijijini kutatua matatizo na kero zao.

Mkuu huyo wa wilaya, anasema, hali hiyo ilimsumbua kwa muda mrefu, kwa vile kila alipozunguka na Kamati ya Usalama ya Wilaya alikutana na migogoro, ambayo inapaswa kutatuliwa na watumishi wa halmashauri.

Aidha, anasema kwamba hali hiyo ilisababisha yeye mkuu wa wilaya atembelee vijiji mbalimbali kila wiki, kutatua migogoro ya ardhi na kuhamasisha shughuli za maendeleo.

Anabainisha kuwa halmashauri ilikuwa inakwama kuwafikia wananchi, kwa sababu gharama za uendeshaji zinaongezeka, kutokana na umbali uliopo kati ya halmashauri na wananchi.

Dota Anney anaitolea mfano Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kuwa ilikuwa katika eneo la manispaa, na kukifikia kijiji cha Mwisho ni lazima kusafiri kilometa 92, na kwamba uamuzi wa kuhama umefuta machozi ya wananchi wanyonge ambao sasa watafikiwa kwa urahisi.

Matarajio ya mkuu huyo wa wilaya ni wananchi kupata huduma kwa haraka na kupunguza gharama za usafiri, usimamizi wa shughuli za maendeleo utaongezeka kwa vile wafanyakazi wa halmashauri watafika kwa wakati kutembelea miradi ya maendeleo.

Anatarajia pia ukusanyaji wa mapato ya serikali hasa ya ndani ya halmashauri utaongezeka, matumizi ya halmashauri yatapungua kwa sababu posho za madiwani na gharama za mafuta na ukarabati wa magari vitapungua kwa vile vikao vitafanyia katika maeneo yao ya utawala na hakuna safari ndefu za mara kwa mara.

Mbali na hayo, matarajio ni gharama za utengenezaji wa magari na mafuta zitapungua kwa kila halmashauri na pia malengo ya kugawanywa halmashauri ya kuhudumia wananchi yametimizwa.

Hata hivyo, anasema suala la mgawanyo wa mipaka utawala halmashauri za wilaya upo karibia kila halmashauri za wilaya mfano na unatakiwa kuangaliwa kwa umakini na kwamba kabla ujenzi wa majengo ya kudumu haujaanza ifanywe tathmini mgawanyo wa mipaka ya halmashauri.

"Nashauri mamlaka zichukue hatua haraka, ili mgawanyo uangaliwe upya na uakisi mahitaji ya wananchi. Naamini changamoto kubwa katika kufikia maamuzi ya kutazama upya mipaka ya halmashauri ni wanasiasa maana baadhi ya kata au majimbo na kata zake zitamegwa kuunda mipaka mipya ya halmashauri," anasema Dk. Anney.

Anaeleza kuwa baadhi ya wanasiasa wanaamini kwamba wao ni wa kudumu na hivyo mambo ya msingi huwa wanapinga kwa maslahi ya kisiasa na anadai baadhi ya mipaka ya awali iligawanywa kwa maslahi ya kisiasa.

Vile vile anasema, mgawanyo ukirekebishwa kwa kutumia busara na ukweli, huku ubinafsi ukiachwa, watakuwa wamewasaidia wananchi wanyonge anaowasemea kila siku Rais Magufuli.

"Wanasiasa tukumbuke sisi nafasi zetu si za kudumu ila wananchi ni wa kudumu. Tunashukuru Rais kwa busara zako za kuwajali wananchi maskini. Hivyo, sisi mamlaka za mikoa na wilaya tusaidie katika mchakato wa kushauri Ofisi ya Rais Tamisemi kuhusu namna bora ya kugawa upya mipaka ya halmashauri za wilaya," anasema.

Anaeleza kuwa tatizo la umbali na mgawanyo wa mipaka ya utawala halmashauri za wilaya lipo karibia kila kona kuanzia Mbeya, Kondoa, Babati, Bunda na Tarime, hivyo ni muhimu busara zikatumike katika mgawanyo huo.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Reli ya kisasa kuunganisha Tanzania, Burundi, Congo

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI za Tanzania, Congo na Burundi zimeingia makubaliano ya kujenga reli ya kisasa kwenda kwenye nchi hizo, ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo na kukuza uchumi wa nchi husika.

Mradi huo wa SGR utaunganisha Bandari ya Tanzania na nchi hizo, kupitia Uvinza (Tanzania), Msongati na Gitega (Burundi) na Mashariki ya Congo.

Mawaziri wa nchi hizo walikutana jana na kuhuisha mkataba uliokuwapo ambao ulisainiwa wakati wa serikali ya awamu ya tano, lakini haukutekelezeka, na mwingine uliosainiwa mwaka 2015 utakaohuishwa na kuwa na chombo kitakachowapa nguvu ya utekelezaji.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwele, alisema upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa mradi utakamilika mwishoni mwa mwezi Januari, na kwamba mawaziri wamesaini makubaliano yaliyorejewa ili kwenda kwenye hatua ya utekelezaji.

"Tumepata Mhandishi mshauri kampuni HP Gulf ya Ujerumani na baada ya kazi kukamilika Januari, mawaziri watakutana kupokea matokeo ya uchambuzi wa mradi yatapelekwa kwa wakuu wa nchi zote," alisema.

Kwa hatua ya awali mawaziri wa nchi hizo wameunga mkono mradi huo, na kwamba utaanzia Uvinza hadi Msongati na baadaye Gitega na kuunganishwa na Congo, na kwamba ili mradi uwe na manufaa kiuchumi ni lazima nchi hiyo iunganishwe.

"Tuna madini zaidi ya tani milioni 150 ya Nicol eneo la Msongati, tukiunganisha na Congo mradi utajilipa kirahisi zaidi," alifafanua.




Mkurugenzi wa Huduma ya T-Pesa, Lulu Mkudde (kulia), akionyesha jinsi ya kufanya muamala wa kifedha kutoka katika akaunti ya Benki ya NBC kupitia huduma ya kifedha kupitia T-Pesa ya Kampuni ya TTCL, katika uzinduzi wa ushirikiano wa huduma za kifedha ya T-Pesa na NBC jijini Dar es Salaam jana, ambapo wateja wa NBC wataweza kutoa na kutuma pesa katika simu zao za mkononi kupitia huduma ya T-Pesa. Kushoto ni Mkuu wa Huduma za Kibenki Kidigitali wa NBC, Deogratius Mosha. **MPIGAPICHA WETU.**

## Mnyika adai kumlalamikia Mkurugenzi NEC

INATOKA UK 2

mkuu akanijibu kwamba ameshatoa maelekezo kwa msimamizi wa uchaguzi agawe nakala za barua kwa mawakala wote, lakini hawakupewa barua hizo mpaka usiku," alidai Mnyika.

Akihojiwa na Wakili Nyantori kuhusu kufukuzwa Chuo Kikuu Dar es Salaam, shahidi huyo alidai kuwa hakufukuzwa bali aliandika barua kuahirisha mwaka.

Alidai tangu ameahirisha mwaka wa masomo Chuo Kikuu mpaka leo (jana) hajarudi tena kuendelea na masomo hayo anaendelea na siasa.

Mbali na Naibu Katibu Mkuu Chadema, Tanzania Bara, Mnyika, washtakiwa wengine ni Mwenyekiti Chadema Taifa, Freeman Mbowe, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche washtakiwa wengine ni Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji, Mbunge wa Bunda Ester Bulaya na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, Heche, Katibu Mkuu Taifa, Dk. Vicent Mashinji na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama, wote wanadaiwa kuwa, Februari Mosi na 16, mwaka jana, Dar es Salaam walikula njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko kutawanyika.

## Ubakaji, ulawiti vyashika kasi Dar

INATOKA UK 2

kampeni hizo, aliwataka wanaume ambao wanapigwa na wake zao, wasiogope kutoa taarifa kwenye madawati hayo ya jinsia kwa kuwa hayajawekwa kwa ajili ya wanawake na watoto peke yao.

"Unakuta askari anapigwa, lakini anaogopa kuripoti au mtu mwenye misuli mikubwa anapigwa na mke wake, anaona aibu, mjitokeze kwa sababu matukio ya ukatili wa kijinsia huwaathiri zaidi watoto, mwisho wa siku wanakimbia familia zao kutokana na kuyashuhudia.

"Kama mtaogopa kwenda kwenye madawati haya ambayo wanaosikiliza hizo kesi ni wanawake, mje hata kwetu," alisema.

Msafiri aliwataka wazazi kutowahusisha watoto wakati wa kutatua migogoro yao ikiwa ni mbinu ya kuepuka kuwaathiri kisaikolojia.

Pia aliwataka madereva wa bajaji, daladala, pikipiki na utingo kuwa sehemu ya kutoa taarifa ya matukio ya ukatili wa kijinsia yanapotokea mitaani.

## Hatima CD ya Zitto kuhusu uchochezi leo

INATOKA UK 3

Pia alidai shahidi huyo ameshindwa kuonyesha mashine iliyotumika kurekodi na kama ilikuwa inafanya kazi vizuri na kuomba mahakamani isipokee kielelezo hicho.

Akipinga hoja hizo, Wakili wa Serikali Mwandamizi Nassoro Katuga alikiri kuwa kielelezo ambacho shahidi anataka kipokewe na kitumike kama ushahidi mahakamani ni cha kielektroniki.

Katuga alidai kuwa kitu ambacho shahidi alikuja kukielezea mahakamani hapo ni kuhusu uchunguzi walioufanya katika video kama ni halisi au la.

Alidai hakuna kifungu ambacho upande wa utetezi wamekielezea kwamba aliyerekodi video ndiye anayepaswa kutoa kielelezo hicho.

Kutokana na mabishano hayo, Hakimu Shaidi alisema atatoa uamuzi leo kama kielelezo hicho kipokewe au la.

Awali, shahidi wa 14 ambaye ni Mtaalamu wa Uchunguzi wa Kisayansi kutoka Makao Makuu ya Polisi, Sajent James (52), alidai alipata barua iliyoambatanishwa na CD kutoka kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni ikielekeza kufanya uchunguzi wa picha iliyomo kwenye kielelezo hicho.

Alidai barua hiyo ilipewa namba OB/IR/8291/2018 ya Oktoba 10, 2018 ililetwa na Koplo Faraji na baada ya kuipokea mkuu wake wa kazi, Mrakibu wa Polisi (SP) Tumaini, alimpa jukumu la kufanya uchunguzi.

James alidai kuwa baada ya uchunguzi aligundua kuwa video iliyohifadhiwa kwenye CD ni halisi hivyo aliandaa hati kwa mujibu wa kifungu cha 202 (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA).

Alidai ripoti ya uchunguzi wa kielelezo hicho aliandika Desemba 6, 2018 na kuiomba mahakamani ipokee kielelezo hicho na kioneshwe kilichomo ndani ya CD.

Katika kesi hiyo, Zitto anadaiwa Oktoba 28, mwaka jana akiwa katika mkutano na waandishi wa habari, uliofanyika katika Makao Mkuu ya ACT-Wazalendo, alitoa maneno ya uchochezi yenye kuleta hisia ya hofu na chuki.

Inadaiwa kuwa alisema: "Watu ambao walikuwa majeruhi katika tukio la mapambano baina ya wananchi na polisi wakiwa wamekwenda hospitalini kupata matibabu katika kituo cha afya Nguruka, Polisi wakapata taarifa kuwa kuna watu wanne wamekwenda hospitalini kituo cha afya Nguruka kupata matibabu wakawafuata kule wakawaua."

HABARI KITAIFA

## Utafiti kuvifikia vituo vya maji 13,824 nchi nzima

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inafanya utafiti wa vituo vya maji nchini kote ili kubaini hali halisi ya vituo hivyo kupitia mradi wa Malipo kwa Matokeo (Payment by Result) uliofadhiliwa na Shirika la Misaada ya Watu wa Uingereza (DFID), ikiwa ni awamu ya nne ya mradi huo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika siku ya kuhitimisha mafunzo ya watafiti yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, mwakilishi wa Wakala wa Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Bahati Joram, alisema utafiti huo unafanywa na Kampuni ya Kitanzania ya DataVision International ambayo mwaka 2019 ilishinda tuzo ya 'East Africa Brand Leadership 2019' kama kampuni bora katika utoaji wa huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), utafiti pamoja na utengenezaji wa mifumo ya malipo ya kielektroniki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo itaungana na washirika wake ambayo ni kampuni ya WEMA Consult.

Alisema kuwa utafiti huo unafanyika kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara. Utafikia halmashauri 181, vijiji/mitaa 1,529 na vituo vya maji 13,824.

"Hii ni awamu ya nne ya mradi huu, ambapo tumelenga kuhimiza utunzwaji wa vituo vya maji na kuviendeleza. Hivyo, kupitia mradi huu unaofadhiliwa na DFID kila kituo ambacho kilijengwa na kikakutwa kinafanya kazi, halmashauri husika itashikwa mkono kuisaidia kujenga vituo zaidi," alisema Joram.

Alisema mradi huu unaolenga kuboresha utunzaji wa vituo vya maji na kuongeza upatikanaji wa majisafi unafanyika kwa kipindi cha miaka minne na unatarajiwa kukamilika Machi 2022.

Joram alieleza ingawa ukaguzi wa vituo hufanywa na serikali kila mwezi kupitia CDMT ambalo ni eneo analolisimamia yeye akiwa mtaalamu wa Tehama, serikali imeona ni vyema ikaweka jicho lingine huru kufanya utafiti ili kuona ni kwa kiasi gani taarifa hizo za kila mwezi zina uhalisia.

Bwigane Mulinda ambaye ni Meneja wa Uendelezaji wa Biashara (Business Development Executive) wa kitengo cha Utafiti na Takwimu cha DataVision International, alisema kuwa watafiti walipewa mafunzo ya siku tano; na kwamba baada ya kufanya utafiti wa kwanza jijini Dar es Salaam wameona watafiti wana uwezo mzuri wa kukusanya taarifa kwa usahihi kwenye mikoa yote 26 iliyokusudiwa.

"Tumekusanya taarifa katika wilaya zote za Dar es Salaam na tumemaliza, tumepata taarifa nzuri na safi zinazoonesha watafiti wetu wamefaidika na mafunzo. Sasa tunakamilisha mikoa mingine 25 ili kutekeleza hii awamu ya nne ya mradi wa Malipo kwa Matokeo," alisema Bi. Bwigane.

Naye Zawadi Said ambaye ni mtafiti kutoka DataVision alieleza kuwa walipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wananchi wa maeneo ya Mkoa wa Dar es Salaam walipofika, na kwamba hii inaonesha kuwa watafanikisha vizuri kazi yao.

Machi 2019, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema serikali imebaini kuwa kati ya vituo 131,000 vilivyojengwa kwenye maeneo ya vijijini takribani 46,000 havifanyi kazi. Hata hivyo, serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imeshajenga na kukarabati vituo kadhaa katika kipindi cha miezi nane hadi sasa. Hivyo, utafiti huu unaofadhiliwa na DFID utakuwa chachu ya kukarabati na kujenga vituo vingine vingi zaidi nchini.




Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Ofisi ya Rais Tamisemi, Mwajina Lipinga (kulia), akizungumza kwenye mjadala wa tathmini ya Mpango wa Kutokomeza Ukatili kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), jijini Dar es Salaam jana, anayefuata ni Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo (WiLDAF), Anna Kulaya na Mratibu wa Mtakuwwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Happiness Mugyabuso. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Tanzania, Namibia kuimarisha ushirikiano

**Na Beatrice Moses**

TANZANIA na Namibia zimekubaliana kutumia ushirikiano uliopo kati yao kujikomboa kiuchumi na kuimarisha diplomasia kwa kufungua ofisi za ubalozi.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam.

Alisema katika kufanikisha makubaliano hayo, Tanzania inajiandaa kufungua ubalozi wake Namibia hivi karibuni ili kufungua fursa zaidi kupitia diplomasia.

Prof. Kabudi aliyasema hayo wakati wa mkutano wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano, ambayo ilikutana kwa mara ya pili jana tangu mwaka 1999 ilipokutana mara ya kwanza.

Alisema hatua hiyo ya kufungua ubalozi Namibia pia ni utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli aliyoitoa alipofanya ziara nchini humo mwaka huu.

"Kabla ya mwaka huu haujakwisha, balozi wetu atakwenda Namibia na tunaamini na wa Namibia atakuja kuanza kazi hapa," alisema Prof. Kabudi.

Katika mkutano huu wa pili wa Tanzania na Namibia zimetiliana saini hati ya makubaliano (MoU) kwenye sekta kadhaa ikiwamo za utalii, madini, kuwawezesha vijana na biashara kwa ujumla.

Prof. Kabudi alisema kuna mambo ambayo Tanzania inapaswa kujifunza kutoka Namibia katika sekta ya utalii kutokana na kuwa nchi hiyo inafanya vizuri.

Alisema nchi hiyo kupitia sekta ya utalii imetumia jangwa kama fursa ya kuvutia watalii.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Namibia, ambaye ni Naibu Waziri Mkuu, Netumbo Nandi-Ndaitwa, alisema nchi hiyo imenufaika na ushirikiano na mchango iliyotoa Tanzania wakati wa kupigania uhuru.

Alisema Namibia inaamini kwa utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa utazingatiwa kwa manufaa ya nchi zote mbili.

Aliishauri Tume hiyo kukutana mara kwa mara kuangalia utekelezaji wa makubaliano hayo kila baada ya robo mwaka.

Inaishukuru Tanzania kwa mchango wake wakati wa kupigania ukombozi wa Taifa lake mpaka lilipopata uhuru mwaka 1990. Alisema Waziri Nandi-Ndaitwa kuwa Namibia nayo imejipanga kufungua ubalozi wake nchini.

## Stendi mpya Dar yakamilika kwa 50%

**Na Juster Prudence**

UJENZI wa stendi mpya ya mabasi ya mikoani inayojengwa jijini Dar es Salaam katika eneo la Mbezi Mwisho, imekamilika kwa asilimia 50.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alisema stendi hiyo kubwa na ya kihistoria ambayo itagharimu Sh. bilioni 50.9, na kwamba itakua na manufaa makubwa kwa nchi.

Alisema stendi hiyo itakuwa na jumla ya maegesho ya magari madogo zaidi ya 400, mabasi 216, na kwamba kila gari litapaswa kukaa kituoni humo kwa saa moja na kuondoka ili kuwawezesha abiria wengi kutumia muda mfupi zaidi.

## Washauriwa kujiunga CHF

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

WANANCHI mkoani Ruvuma wameshauriwa kuona umuhimu wa kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (CHF) ili kuondokana na adha ya kukosa huduma ya matibabu kutokana na uhaba wa fedha za matibabu.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christine Mdeme, wakati akizindua mfuko huo ulioboreshwa na utambulisho wa wadau wa maendeleo wa Shirika la Misaada la Kimataifa la Marekani (USAID) Boresha Afya mkoni Ruvuma Manispaa ya Songea na kuhudhuriwa na wananchi na viongozi mbalimbali wakiwamo wakuu wa wilaya, wenyeviti wa halmashauri na wakurugenzi watendaji pamoja na viongozi wa dini.

Mdeme alisema kila mwananchi anapaswa kuwa mhamasishaji wa mfuko huo ambao utaleta tija kubwa kwenye jamii pale watu watakapokumbwa na maradhi.

**Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christine Mdeme, wakati akizindua mfuko huo ulioboreshwa na utambulisho wa wadau wa maendeleo wa Shirika la Misaada la Kimataifa la Marekani (USAID) Boresha Afya mkoni Ruvuma Manispaa ya Songea na kuhudhuriwa na wananchi na viongozi mbalimbali wakiwamo wakuu wa wilaya, wenyeviti wa halmashauri na wakurugenzi watendaji...**

# Wenye ulemavu waiomba serikali

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WANACHAMA wa Jumuiya za watu wenye ulemavu kisiwani Pemba, wameiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kuwawezesha kwa kuwapatia mitaji ili wafanye kazi za ujasiriamali zitakazowakwamua na maisha duni.

Walisema zipo shughuli mbalimbali za ujasiriamali ambazo wakizifanya zitawasaidia kupata fedha zitakazowasaidia kuendesha maisha yao, ingawa wanashindwa kuzifanya kutokana na kukosa mitaji.

Waliyasema hayo katika wakati wa kongamano la Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani katika Kuadhimisha Siku ya Kimataifa, walisema kuwa, ipo haja kwa serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma kwa kuwawezesha kifedha.

Aidha, walieleza suala la mikopo kwa wajasiriamali halijashughulikiwa kwa kuwapata watu wenye ulemavu, jambo ambalo linawasikitisha kukosa fursa hiyo.

Suleiman Massoud kutoka jumuiya ya watu wenye ulemavu wa uoni Wilaya ya Chakechake, aliwataka wanajumuiya hizo kutokaa kimya na badala yake watetee haki zao, ili kusaidia kukwamua changamoto zinazowakabili.

"Tusikubali kujidharau na kujidhalilisha kwani tunaweza kuwapa mwanya wanaotaka kutudhalilisha, tuwe mstari wa mbele kutetea haki zetu, ili na sisi tusidharaulike katika jamii," alisema Suleiman.

Akitoa ushuhuda katika kongamano hilo, Awena Khamis Rashid mwenye ulemavu wa ngozi, alieleza hali hiyo alizaliwa nayo ingawa alikumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo kuitwa majina mabaya, jambo ambalo lilikuwa likimkwaza katika jamii iliyomzunguka.

Akiwasilisha mada ya hali halisi ya watu wenye ulemavu Zanzibar Mwenyekiti wa Shirikisho la Jumuiya za Watu wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA), Mwandawa Khamis Mohamed, alisema, lengo la kongamano hilo ni kuwakomboa na kuwatetea watu wenye ulemavu juu ya upatikanaji wa haki na fursa sawa.

"Zanzibar tuna watu wenye ulemavu wa aina tofauti 16,696 sawa na asilimia 5.6, wanawake ni 7,663 na wanaume 9,033, ambapo kwa duniani ni asilimia 15 ya watu wenye ulemavu," alisema.

Naye Rashid Salim kutoka Idara ya Watu wenye ulemavu Pemba, wakati akiwasilisha mada ya mchango wa serikali kwa watu wenye ulemavu, alieleza kuwa serikali imeweka upatikanaji wa huduma za ushauri na kulinda haki pamoja na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu.

"Pia sera inatoa fursa na vipaumbele kwa watu wenye ulemavu, serikali ina mikakati yake kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki zao," alisema.

Mapema akifungua kongamano hilo Mkurugenzi wa Idara ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Abeida Rashid Abdalla, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kuchukua hatua muhimu za kuzitambua rasmi jumuiya za watu wenye ulemavu, ili ushiriki wao katika maendeleo ya jamii uonekane.

# Sera, sheria kulinda maeneo ya kilimo

**Na Ashton Balaigwa, MVOMERO**

WIZARA ya Kilimo inakusudia kufanya mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo kwa kutunga sera na sheria kwa ajili ya kuyalinda maeneo ardhi ya kilimo ili yasitumike katika mipango mingine ikiwamo makazi ya watu.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliyeambatana na Naibu Waziri wa Kilimo na Ardhi wa Venezuela, Jose'Aguilera Contreras, kwenye mawasilisho ya ukomo wa mradi wa ubia kwa maendeleo ya mifumo ya uzalishaji endelevu wa mpunga Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara unaotekelezwa nchini katika wilaya za Mvomero, Kilosa na Kilombero uliofanyika Mvomero mkoani Morogoro.

Alisema maeneo mengi ya ardhi ya kilimo yamegeuzwa kuwa makazi na kufanya maeneo ya kilimo kupungua wakati idadi ya watu wanaingia katika kushiriki kilimo ikiwa inaongezeka kwa kasi na hivyo kuhatarisha kupunguza masuala ya uzalishaji wa chakula nchini.

Waziri Hasunga alisema serikali itaanza kuratibu mchakato wa kutengeneza sera na sheria ya kulinda maeneo ya kilimo ili kuyafanya maeneo yaweze kuendelea kuongeza uzalishaji kupitia kilimo kwa kuwa mahitaji ya chakula nchini bado ni makubwa.

Naye Balozi wa Venezuela katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda, Jesus Manzanilla, alipongeza ushirikiano uliopo kati ya nchi yake na Tanzania, na kwamba wataendelea kusaidia katika nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya kilimo ili kuinua uchumi na kuongeza ajira.

Akizungumzia mradi huo wa ubia kwa maendeleo ya mifumo ya uzalishaji endelevu wa mpunga Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, alisema ni mradi wenye mafanikio na utasaidia nchi kuongeza uzalishaji kupitia mpunga, na kuipongeza Venezuela iliyofadhili mradi huo. Mratibu wa mradi huo, Diomedes Kalisa kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), alisema umesaidia jumla ya wakulima 2,600 wakiwamo vijana baada ya kuanza kutumia mfumo wa kilimo shadidi cha mpunga ikiwa ni matokeo ya mafunzo ya vijana 150.

Mwakilishi wa FAO nchini, Fred Kafeero, alisema watu wengi katika nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania mijini na vijijini wanaendelea kutegemea mpunga kuwa miungoni mwa chakula na Tanzania ni nchi ya pili kwa Afrika kwa kuzalisha wa zao hilo ikitanguliwa na Madagascar.



Washiriki na wanajumuiya za watu wenye ulemavu kisiwani Pemba, wakiwa kwenye kongamano la watu wenye ulemavu kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu Duniani, lililoandaliwa na Shirikisho la Jumuiya za watu Wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA) Chakechake Pemba. **MPIGAPICHA WETU**

# Zanzibar yapaisha huduma afya kimtandao

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

AZMA ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Ali Mohammed Shein ya kuviunganisha vituo vya afya visiwani hapa kwenye Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wagonjwa imetimia.

Akizungumza na waandishi wa habari waliokwenda kujifunza namna Tehama ilivyochangia kuboresha utoaji wa huduma ya afya visiwani hapa jana,

Mkurugenzi wa Mawasiliano katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Mzee Suleiman Mndewa, alisema tangu serikali ilipofanikiwa kujenga kituo cha Mkongo wa Taifa vituo 24 vya afya Zanzibar vimeshaunganishwa katika mfumo huo.

"Baada ya Mkongo wa Taifa, serikali sasa inaweka mitandao ambayo itaunganishwa moja kwa moja na vituo vya afya au hospitali hizo 24 hapa Zanzibar," alisema Dk. Mndewa, huku akielezea umuhimu wa Tehama katika kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za uchumi visiwani humo.

Mradi wa kujenga kituo cha data eneo la Mazizini hapa Unguja ulitekelezwa kwa msaada wa karibu wa Kampuni ya mawasiliano ya simu ya Multinational Telecommunications Equipment and Systems, ZTE Corporation.

"Tangu hapo serikali iliamua kuunda Wakala wa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Zanzibar ambayo moja ya majukumu yake ni kuratibu shughuli zote zinazohusiana na kituo hicho," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Zanzibar, Mhandisi Shukuru Awadhi Suleiman, alisema kazi ya kuviunganisha vituo vya afya 24 kwenye kituo cha mawasiliano imeshakamilika.

"Ninachoweza kusema ni kwamba tumefanikiwa na vituo vyote 24 vya afya vilivyopo Unguja na Pemba vimeshaunganishwa na tumeshapiga hatua kubwa ya kufunga mashine ya MRA kwenye Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja," alisema Mhandisi Suleiman.

Alisema hatua hiyo ina maana kuwa vituo vyote vya afya wilayani vinaweza kutuma picha za X-Ray moja kwa moja Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja zikapokelewa na kujibiwa papo hapo bila kuchelewa na kuokoa maisha wagonjwa.

"Kabla juhudi hizi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Shein, mgonjwa alikuwa anapaswa kuchukua picha kusafiri nayo mpaka mjini ikasomwe na kusubiria majibu kwa muda mrefu ambapo kwa sasa imebaki historia," alisema Mhandisi Suleiman.

## Watakiwa kupanda miti kukabili hewa ya ukaa

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

JAMII imetakiwa kupanda miti kwa kasi ili kufyonza hewa ya 'kaboni daiokside' inayozalishwa kwa wingi na viwanda vinavyoendelea kujengwa hapa nchini.

Wito huo ulitolewa jana na Mratibu wa Taasisi ya Jane Good hall, Yoronimo Rutta, wakati akizungumza na Nipashe kwenye mji mdogo wa Magugu mkoani Manyara wakati wa ziara ya balozi wa taasisi hiyo, Jacqueline Kyaruzi.

Mratibu huyo alisema wamejiita jina la Roots and Shoots kwa kuwa wanashughulika na miti ambayo ina mizizi na matawi na wamejikita kwenye uangaizi wa mimea, wanyama pamoja na jamii.

Alisema lengo lao ni kuitunza dunia ambayo imeharibika kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kupanda miti na kuitunza mazingira ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mtaalamu huyo wa miti alisema taasisi hiyo ilianza kazi mkoani hapa mwaka 2014 na tangu kuanzishwa kwake, wamepanda miti 500,000.

Alisema mbinu wanazozitumia ni kugawa miti kwa watu binafsi bila malipo, kugawa miti kwa taasisi, kutoa elimu kwa umma na kuwapatia miti wanafunzi kwenda kuotesha nyumbani kwao.

Rutta alisema taasisi hiyo, imekuwa ikitoa zaidi ya miti 10 kwa wanafunzi ambao wanaipanda wanapoanza darasa kwanza na wanapomaliza darasa la saba inakuwa tayari kwa ajili ya kuchanwa mbao.

Ameitaka jamii kutunza mazingira kwa kupanda miti kwa kuwa itawasaidia watabadilisha hali ya hewa na kuwainua kiuchumi sambamba na kulinda kwa viumbe hai.

Naye Kyaruzi alisema alianza kupenda mazingira baada ya kukutana na mwanamke mmoja kutoka Ulaya aliyekuwa anafundisha namna ya kuzijua tabia za wanyama na yeye akavutiwa.

Alisema amesoma Chuo cha Wanyamapori Mweka na anafahamu namna ya kuwafundisha wanyama kuishi na jamii.

Balozi huyo alifanya ziara yake katika shule za msingi Magugu na Kibaoni na kupanda miti pamoja na kutoa elimu kwa wanafunzi na walimu ili wawe mabalozi wa mazingira.

**Alisema mbinu wanazozitumia ni kugawa miti kwa watu binafsi bila malipo, kugawa miti kwa taasisi, kutoa elimu kwa umma na kuwapatia miti wanafunzi kwenda kuotesha nyumbani kwao.**

# Lowassa sasa aibuka kivingine

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

WAZIRI Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, ameibuka kwa mara ya kwanza hadharani tangu alipotangaza kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) akitokea Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Mwanasiasa huyo ambaye mwaka 2015 aligombea urais kupitia Chadema, ameibuka na kuwataka wanafunzi wa zamani kujenga tabia ya kuzitembelea shule walizosoma miaka ya nyuma na kuwajali walimu waliowafundisha kwa kuwa wana mchango mkubwa katika mafanikio waliyofikia.

Lowassa aliyazungumza hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea Shule ya Sekondari ya Arusha, jijini hapa. Lowassa ni miongoni mwa wanafunzi waliosoma shuleni hapo miaka ya 1960.

"Nimefurahi sana kuwaona baadhi ya wanafunzi wenzangu tuliosoma pamoja katika shule hii. Ni jambo la mfano kila mwanafunzi atembelee shule aliyosoma na kuona maendeleo yake," alisema Lowassa.

Naye Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) mkoani Arusha, ambaye ni miongoni mwa wanafunzi waliosoma shuleni hapo, Walter Maeda, alisema lengo la kutembelea shule hiyo ni kuwapa motisha wanafunzi wanaosoma kwa sasa kuona kuwa inawezekana wakafikia malengo endapo watatumia vizuri elimu walinayoipata.

"Kutembelea shule hii itawaongezea wanafunzi bidii ya kusoma ili waje kuwa kama Lowassa, (Daniel) Ole Njolay, Maeda na wengine wengi tulioambatana nao unaowaona hapa," alisema Maeda.

Alisema katika ziara yao, wameona bado ina mahitaji ya majengo na samani kwenye vyumba vya madarasa na mahitaji ya walimu.

Licha ya kuzungumza hayo alisema baada ya kuona mahitaji ya shule hiyo, watakwenda kujipanga ili kutatua baadhi ya matatizo waliyoyaona.

Mwenyekiti wa wahitimu hao, Sambai Nailejileji (70), alisema wamekutana ili kuwapongeza walimu hao ambao waliwafundisha miaka 50 iliyopita.

Mhitimu mwingine, Mathias ole Kisambo, alisema ni vyema wahitimu wengine wakarejea kwenye shule walizosoma na kushirikiama na jamii inayowazunguka ili kuboresha miundombinu na kuhamasisha vijana kujifunza kwa bidii.

"Tunaona sasa hivi walimu wetu wanastaafu wakifika miaka 70 au 80 hali zao si nzuri, hivyo sisi wanafunzi tulio na uwezo kiasi ni vyema tukawakumbuka kama tunavyowahudumia wazazi wetu kwa sababu walitulea tukiwa shuleni," alisema Ole Kisambo.

Mwalimu Materu ambaye aliyeongoza shule hiyo kwa miaka 10 kuanzia mwaka 1962 mpaka mwaka 1972, aliwashukuru wanafunzi wake kwa kumkumbuka na kuwaombea kwa Mungu azidi kuwabariki.

Awali Mkuu wa Shule hiyo, Christopher Malamsha, aliwaeleza wanafunzi hao wa zamani kuwa shule hiyo ina upungufu wa jengo la utawala, hivyo kuwaomba wanafunzi hao kuchangia ujenzo wa jengo hilo ambalo hadi kukamilika kwake linahitaji Sh. milioni 250. Kwa sasa, alisema wana Sh. milioni 50.

Malamsha alisema shule hiyo imezalisha watu mashuhuri na viongozi wakubwa katika nchi, hivyo anaamini wakiamua nia ya kuchangia ujenzi huo utakamilika ndani ya muda mfupi.

Aliwataja baadhi ya viongozi hao kuwa ni Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Abdulrhman Kinana, Lowassa, Ole Njolay na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Agustine Mahiga.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega (katikati), akitoa taarifa ya matumizi ya zaidi ya Sh. bilioni 34.3 za mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF), zilizotumika kuwakwamua kiuchumi kaya 46,771 za mkoa huo, katika kipindi cha Agosti 2015 hadi Februari mwaka huu, mbele ya Kamati ya Uongozi wa TASAF Taifa, jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Hospitali yaomba serikali kuongeza uwekezaji

**Na Allan Isack, ARUSHA**

HOSPITALI ya Rufani ya Haydom wilayani Mbulu, Manyara, imeingiwa na hofu ya kushindwa kujiendesha baada ya ufadhili kutoka watu wa Norway kupitia Shirika la NCAA kupungua kutoka asilimia 65 hadi 25 na serikali ikifadhili kwa asilimia 19.

Hali hiyo ilisemwa juzi na uongozi wa hospitali hiyo wakati wa kikao cha wadau wa kutathmini hali ya utoaji wa huduma hospitalini hapo.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeombwa kuangalia uwezekano wa kuongeza ufadhili wake kutoka asilimia zilizopo sasa ili hospitali hiyo iliyo chini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mbulu, iendelee kutoa huduma kwa gharama nafuu kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali hiyo, John Nade, alisema hali si nzuri kwenye hospitali hiyo baada ya kupungua kwa ufadhili hali ambayo inaweza kusababisha kushindwa kutoa huduma kwa ufanisi.

"Ufadhili unajumuisha rasilimali fedha, watu ambao ni madaktari na watoa huduma wengine ndani ya hospitali pamoja na vifaa tiba, sasa ni vyema serikali ikaona walau namna ya kuongeza ufadhili wake kutoka asilimia 19," alisema Nadel.

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Emanuel Nuas, alisema ufadhili wa Norway ulipungua miaka 10 iliyopita na siku zinavyoendelea kusonga mbele ufanisi wa kazi unaendelea kupungua kutokana na hospitali hiyo kuhudumia eneo kubwa na watu wengi kulinganisha na uwezo wake wa kifedha.


Nuas alisema matokeo ya kupungua kwa ufadhili katika hospitali hiyo, umesababisha kupunguza baadhi ya wafanyakazi kwa kuwa hawana uwezo wa kuwalipa.

"Naiomba serikali iangalie jambo hili ili tuendelee kutoa huduma kwa ufanisi na tuongeze idadi ya watumishi tunaiomba sana serikali itusaidie ufadhili wake wa kifedha na vifaa tiba," alisema Nuas.

Wadau waliohudhuria kikao hicho cha watumiaji wa huduma za hospitali. walishangazwa kuona serikali ikifadhili hospitali hiyo kwa asilimia 19 kitendo kinachosababisha wananchi kutopatiwa huduma stahiki kama walivyozoea awali.

"Kwa kweli inashangaza sana kuona serikali ikifadhili hospitali kwa asilimia ndogo kiasi hiki. Nikiwa madau na mwananchi ninayepata huduma hapa Hydom, ningeiomba serikali iangalie uwezekano wa kuongezea ufadhili," alisema James Kitonge.

Hospitali ya Rufani ya Hydom ilianzishwa mwaka 1955 chini ya KKKT na kufadhiliwa na serikali ya Norway na kwa sasa inatoa huduma za upasuaji, ikiwa na vifaa mbalimbali vya kisasa.





# Waona fursa ya utalii kuhimiza umoja Afrika

**Na Woinde Shizza, MOSHI**

WADAU sekta ya utalii kutoka nchi za Uganda, Zimbabwe na Tanzania wamewashauri Watanzania kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vikubwa vya utalii vilivyopo barani Afrika kama njia mojawapo ya kuunga mkono utalii wa ndani.

Wamesema kuna haja makundi ya vijana katika nchi zao kutumia vivutio hivyo kama njia ya kuhamasisha umoja wa Afrika na ushirikiano katika nyanja muhimu za maendeleo ikiwamo fursa za utalii.

Wakizungumza baada ya safari ya siku sita ya kuelekea kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro, wajumbe watatu kutoka nchi za Uganda, Tanzania na Zimbambwe, walisema licha ya mlima huo kuwa katika orodha ya maajabu saba ya dunia na kuwa mlima mrefu kupita yote barani, bado vijana wengi hawajautembelea.

Emanuel Motta, mhamasishaji kutoka Tanzania ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Origin Trail, alisema lengo la kupanda mlima huo ni kuhamasisha vijana kutoka nchi zote 55 za Bara la Afrika, kupanda mlima huo ili kutimiza agenda ya Afrika Tunayoitaka 2063 pamoja na kutimiza Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

"Mei mwakani, tutakuwa na tukio kubwa la vijana kutoka nchi zote za Afrika watapanda Mlima Kilimanjaro, hii ni fursa tunaomba vijana waungane na sisi, wako watakaopanda kwa miguu na wengine watatumia vyombo vya usafiri.

Mkurugenzi wa Great Africa Art Banner kutoka Zimbabwe, Munyaradzi Muzenda, alieleza kufurahishwa na vivutio vilivyoko katika mlima huo ambao mtu yeyote akifanikiwa kuupanda na kulifa kileleni ni ishara ya ushujaa na kuvishinda vikwazo katika upandaji wa mlima na maisha kwa ujumla.

Muzenda alisema wanahamasisha vijana kuchora mabango makubwa ya Afrika Tunayoitaka na kupeleka mabango hayo katika kilele cha mlima huo.

Mkurugenzi wa Sister Organization, Ayaa Musuya, kutoka Uganda, alisema mlima huo utatumika kama kiunganishi kwa vijana wa Bara la Afrika kwa kuwaleta pamoja na kuweka mpango wa pamoja na kutekeleza agenda za Afrika Tunayoitaka.

**"Mei mwakani, tutakuwa na tukio kubwa la vijana kutoka nchi zote za Afrika watapanda Mlima Kilimanjaro, hii ni fursa tunaomba vijana waungane na sisi, wako watakaopanda kwa miguu na wengine watatumia vyombo vya usafiri.**

# DC Sabaya amkosha RC Mghwira mapato

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amempongeza Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kwa kubuni na kuboresha vyanzo vya mapato wilayani humo.

Dk. Mghwira alitoa pongezi hizo jana alipozungumza na watumishi wa halmashauri ya wilaya hiyo, akisisitiza kuwa halmashauri yoyote haiwezi kujiendesha pasi na mapato.

Alitaja baadhi ya maeneo ambayo serikali wilayani humo imeboresha kuwa ni pamoja na upatikanaji wa mapato katika eneo la utalii la chemchemi ya maji moto, maarufu Chemka na stendi kuu ya mabasi Bomang'ombe.

Akiwa katika Kijiji cha Mijongweni, Dk. Mghwira aliwataka maofisa kilimo na mifugo wa wilaya kupiga kambi ya siku 15 kijijini huko ili kuwaelimisha wananchi namna bora ya kulima kilimo chenye tija na ufugaji wa kisasa.

Ole Sabaya kwa upande wake, aliwatahadharisha viongozi wa serikali ya kijiji hicho kuhusu matumizi ya mali za wananchi.

Katika taarifa yake kwa Dk. Mghwira, Ole Sabaya alikitaja kijiji hicho kuwa ni kati ya vilivyopokea fedha za miradi mikubwa ukiwamo wa Sh. milioni 200 zilizotolewa na Shirika la Maendeleo ya Japan (JICA).

Awali, akitoa taarifa ya halmashauri, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Jacob Muhumba, alimweleza Dk. Mghwira kuwa halmashauri hiyo ipo mstari wa mbele kutekeleza maagizo ya mkoa katika kuwahudumia wananchi.



Wahamasishaji kutoka nchi za Zimbabwe, Uganda na Tanzania, wakishuka kutoka katika lango kuu la Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, wikiendi, baada ya safari ya siku sita ikiwa ni uzinduzi wa kampeni ya uhamasishaji wa kiafrika kupanda mlima huo, na kutimiza agenda za Afrika tunayoitaka 2063. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Waanza kuona matokeo mradi tokomeza ukatili

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

MATOKEO ya utekelezaji wa mradi wa hamasa kuhusu mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia hususani kwa watoto wa kike, yameanza kuonekana baada ya walimu kugundua matukio tofauti ya ukatili wa kingono katika Kata ya Nasai wilayani Siha.

Jana, Mratibu wa Elimu Kata ya Nasai, Justina Ngolinda, alisema wiki iliyopita alipokea taarifa za mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Sanya Juu kufukuzwa shule kutokana na kupata ujauzito.

Alikuwa akizungumza wakati wa kikao cha tathmini ya mradi huo kwa kada ya walimu na viongozi wa umma wanaotoka katika Kata za Sanya Juu, Nasai na Livishi ambazo zimelengwa na mradi huo.

"Kwa ujumla wake, sisi tumepokea matukio ya ukatili wa kingono na tumeyafanyia kazi, kuna attempt (jaribio) la ulawiti wa mtoto wa darasa la nne. Ingawa halikufanikiwa, tulimkamata mtuhumiwa na taratibu nyingine zinaendelea kwa sababu alikuwa ameshampaka mafuta.

"Jambo lingine ni mwanafunzi wa kidato cha tatu kukatisha masomo yake wiki mbili zilizopita kutokana na kupata ujauzito. Wakati tunafuatilia tukio hilo, tuligundua wazazi wanashiriki kumlinda mtuhumiwa," alisema.


Diwani wa Kata ya Nasai (CCM), Solomon Mmari, akizungumzia matukio hayo, alisema kutokana na kuchomoza kwa kasi kwa ukatili huo dhidi ya watoto, Baraza la Maendeleo ya Kata limeridhia kuitishwa mikutano ya hadhara ya wananchi vijiji vyote vya kata hiyo kufikia Desemba 30, mwaka huu ili kujadili matukio hayo.

Mradi huo wa hamasa unatekelezwa katika kata tatu za Wilaya ya Siha na Shirika la Kwieco kwa ufadhili wa Foundation for Civil Society.

Mratibu wa mradi huo, Peter Mashingia, akizungumza katika kikao hicho cha tathmini, alisema jamii inataka kuona muda mfupi ujao wadau wote waliolengwa na mradi huo wanaibua taarifa za namna walivyofanikiwa kuwashawishi mangariba kuacha kazi ya ukeketaji.

Alisema kuna haja jamii kuacha woga na kujitokeza mashuhuda ambao wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kingono ili kuishinikiza serikali kuchukua hatua.

"Kimsingi tunataka kuona kiongozi wa serikali wamefanya nini, wangapi wamesaidiwa kuondoka katika ukatili wa kiuchumi? Je, tunapaza sauti zetu kwa namna gani?" Alihoji.



Ukurasa 14

**Miaka 56 kifo cha Kennedy Tanzania bado inamkumbuka**

Ukatili kijinsia, rushwa unaondoa wanawake anga za siasa, uchumi



Ukurasa 18




Ukurasa 19

**Ninavyoikumbuka siku ya uhuru kijijini kwetu**

siasa

JUMATANO DESEMBA 4, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 15

**Bashir aongezewa vikombe zaidi vya mateso**

# Ulivyokamilishwa uchaguzi kanda: Chadema ya 'milima na mabonde'

• Ni miezi 11 kuelekea uchaguzi 'baba lao'

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI ndani ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), unaendelea katika nafasi mbalimbali za uongozi ambazo zinalenga kuimarisha mifumo ya chama.

Mchakato huo unafanyika ikiwa imesalia miezi 11 kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Chadema kwa takribani miaka minne kama ilivyo kwa vyama vingine vya upinzani imejikuta katika wakati mgumu baada ya agizo la Rais John Magufuli, kuwa huu ni muda ni wa kufanyakazi na siyo kufanya siasa.

Hatua hiyo iliondoa mikutano ya kisiasa katika ngazi za kitaifa lakini iliwaruhusu wabunge kufanya mikutano kwenye majimbo

INAENDELEA UK.16



Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji. **PICHA: MTANDAO**

**Miaka 24 ya Moi alivyoitumia 'kuwashughulikia' wasaidizi** Ukurasa 20

# Miaka 56 kifo cha Kennedy Tanzania bado inamkumbuka



Kennedy wakati wa uhai wake. Mwaka huu anatimiza miaka 56 baada ya kuuawa Novemba 22, 1963. **PICHA: MTANDAO**

**Na Anil Kija**

NOVEMBA 22 ni siku ya kumbukumbu ya kuuawa kwa kupigwa risasi kwa Rais John Kennedy wa Marekani, mwaka 1963, wakati Tanzania inakaribia miaka miwili ya uhuru na mwaka mmoja kama jamhuri, ikiwa nchi changa sana.

Rais Kennedy aliyeuawa miaka 56 iliyopita, alikuwa mmoja wa watu waliokuwa na mchango mkubwa katika kukamilika, wengine watasema ni kukua kwa fikra ya kisiasa ya Mwalimu Nyerere,wakati huo akiwa amefika miaka 41.

Kimsingi fikra yake ilishakaa vyema kwa mfano inavyoonekana katika insha muhimu baada ya uhuru, kuhusu Ujamaa wa Kiafrika' aliyoitoa akifungua Chuo cha TANU, Kivukoni Januari 1962 na kwa maana hiyo Kennedy aliongeza vitu vingine vichache.

Kumbukumbu ya Kennedy ambayo Mwalimu aliirudia mara kadhaa ni ile aliyoitaja katika mazungumzo na waandishi wa habari Machi 1995 jijini Dar es Salaam akisema 'miaka ya 1960 mwanzoni rais kijana wa Amerika anawaambia Waamerika, 'usiulize Amerika imekufanyia nini ila wewe umeifanyia nini Amerika,' akiainisha uzalendo wa hali ya juu. Ndiyo hisia ambayo Mwalimu alijitahidi kuijenga nchini baada ya uhuru, akajiuzulu uwaziri mkuu ili apite kila mahali akijenge chama na kwa kiasi alichoweza afafanue maadili yake.

Haikuwa rahisi kumuelimisha kila mtu suala la kutokuwa na matabaka, kuondoa kasi ya kugombania matunda ya uhuru na hisia kuwa wako wanaopendelewa katika hili au lile.

> Ni Ghana pekee na Tanzania ndiyo waliotekeleza hatua hiyo, Uingereza ikawezesha kiongozi wa Ghana Dk. Kwame Nkrumah kupinduliwa Februari 1966 wakitumia kampuni kubwa kukwamisha uchumi wa Ghana.

Unaweza kusema kuwa kuuawa kwa Rais Kennedy na kuingia madarakani kwa aliyekuwa makamu wake, Lyndon Johnson kulisaidia kubadili mwelekeo wa Tanzania kuegemea zaidi nchi za Mashariki hasa China na pia Urusi.

Hiyo inaonekana licha ya tofauti ambazo hata hivyo zingeibuka katika uhusiano wa Tanzania na Amerika kwa mfano suala la Cuba ambako Amerika ilipania kukwamisha mapinduzi yake, irudi kama zamani.

Ni mwelekeo uliokuwa unakinzana na sera ya uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe aliyoifuata Mwalimu, na kuieleza bayana baada ya kukosana na Ujerumani Magharibi mwaka 1964,walipotaka Tanzania iache kuitambua Ujerumani Mashariki, iliyokuwa rafiki wa Zanzibar.

Ndiyo jambo la ajabu wakati huo, kwani Tanzania haikuwa karibu na Urusi, na hata siasa ya ujamaa ilipotangazwa mwaka 1967 ilikuwa nii baada ya Waziri Mkuu wa China, Zhou Enlai kufika nchini kwa ziara mara mbili, na Mwalimu kuitembelea China mara moja. Halafu Tanzania ikawa kinara wa kufanya kampeni Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kutaka Jamhuri ya Watu wa China ichukue nafasi yake kama mwanachama na pia katika Baraza la Usalama badala ya Taiwan iliyokuwa inatumiai jina la 'Jamhuri ya China.'

Ndiyo mwanzo wa Tanzania kuwa na nafasi ya kipekee katika diplomasia duniani, ikiongoza diplomasia ya ukombozi kusini mwa Afrika na kurekebisha kasoro dhidi ya Jamhuri ya Watu wa China kufuatia mapinduzi ya 1949 mambo ambayo yasingekubaliwa na Amerika.

Ina maana kuwa wakati Muungano unafikiwa, ambao kwa kiasi kikubwa ulichochewa na maofisa wa ngazi za juu wa Wizara ya Mambo ya Nje huko Washington, tayari mwelekeo wa Tanzania na Amerika ulikuwa umeingia katika sintofahamu.

Rais Johnson hakuwa na simile na Vietnam ya Kaskazini ikijaribu kuunganisha nchi kwa misingi ya utawala wa kikomuniti na kwamba ilifaulu mwaka 1975 majeshi ya Marekani yalipoondoka nchini humo. Wakati huo huo Urusi ilifurahia sana msimamo wa Mwalimu wa kuvunja uhusiano na Ujerumani Magharibi kuliko kulazimishwa kuondoa kuitambua Ujerumanii Mashariki ambayo iliitambua Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hatua hiyo iliongeza Urafiki.

Ukizungumza na wanafunzi wa Kitanzania waliowahi kusoma nchini Urusi miaka hiyo unapata picha ya jinsi Tanzania ilivyokuwa inaheshimika na kuwekwa katika ngazi ya kipekee katika hisia za kitaasisi nchini humo.

Mwanahabari mkongwe aliyekwenda kusoma huko akitokea Idara ya Habari-Maelezo, kuwa alikuwepo mwanafunzi mmoja tu mwingine aliyekuwa pia anasoma uandishi wa habari, lakini akaitwa katika mkutano na wanafunzi takriban 15 wa Kiafrika waliokuwa wanasema nao ni Watanzania.

Alipowaeleza kuwa anafahamu yuko mmoja tena msichana aliyekuwa anasoma eneo hilo, wakamwambia wanajitaja kuwa Watanzania ili wasifuatiliwe kwa nguvu kokote walipo, ili waaminiwe pia.

Nguvu ya kihisia ambayo Rais Kennedy alikuwa nayo kwa Rais Nyerere mwaka wake wa kwanza kama rais na akapigwa risasi akiwa Dallas, Novemba 22, 1963 kabla Nyerere hajamaliza mwaka mmoja madarakani.

Huwezi kusema Rais Johnsonn alifuata sera tofauti na Rais Kennedy, kwani Kennedy alisimamia uvamizi wa Cuba Aprili 1961 ila walikuwa askari wa kukodiwa wa makundi ya kumpinga kiongozi wa kimapinduzi Fidel Castro, na siyo uvamizi halisi wa Marekani. Ina maana kuwa alipokuwa anajenga uhusiano na Rais Kennedy, ilibidi hata hivyo Rais Nyerere asiangalie kila kitu ili mahusiano yasiingie doa, lakini haikupita muda mapinduzi Zanzibar yakaileta Tanganyika katika dira ya serikali ya Marekani, mabalozi wake wakafuatilia kwa nguvu suala la kuunganisha nchi hizi mbili ili kupunguza nguvu ya Urusi na marafiki zake Zanzibar, na nguvu za mwanamapinduzi Abdulrahman Mohamed Babu ndani ya serikali ya Zanzibar .Alihamishiwa serikali ya Muungano.

Wakati Nyerere amevunja uhusiano na Ujerumani Magharibi kutokana na kukataa kuondoa hatua ya Serikali ya Mapinduzii ya Zanzibar kuitambua Ujerumani Mashariki, mara ukaibuka mgogoro mwingine na Uingereza kuhusu uhuru bandia wa Zimbabwe.

Walowezi walijitangazia uhuru kivyao bila wananchi walio wengi kushiriki, na Uingereza ikashindwa kukomesha uasi huo kwani ilikuwa haipigani vita vya kikoloni au kuwazuia walowezi kokote kujichukulia uhuru wao.

Wakati huo Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) ukiwa bado mchanga ukakubaliana kuwa wanachama wa OAU wavunje uhusiano na Uingereza kutokana na kushindwa kuchukua hatua dhidi ya walowezi wakijichukulia uhuru Zimbabwe ila zikakwama.

Ni Ghana pekee na Tanzania ndiyo waliotekeleza hatua hiyo, Uingereza ikawezesha kiongozi wa Ghana Dk. Kwame Nkrumah kupinduliwa Februari 1966 wakitumia makampuni makubwa kukwamisha uchumi wa Ghana.

Wanafunzi walipoandamana hapa nchini kupinga sera za kuwaingiza Jeshi la Kujenga Taifa na kukatwa mshahara kwa miezi 18 baada ya kukaa kambini miezi sita ili kujenga hisia za uzalendo na mshikamano, wakiwa na mabango 'Colonialism Was Better',Nyerere akatafsiri 'afadhali mkoloni' ikawa tusi kwake. Sera zake za kuanzia uhuru zilikuwa zimefikia kikomo. Akauacha ujamaa wa njozi wa kupinga matabaka, kujenga usawa kihisia, akaufanya ni ujamaa wa kisayansi, akataifisha mashamba, mabenki na biashara kubwa za kutoa na kuingiza bidhaa nchini.

Lengo lilikuwa ni kuzuia Uingereza na wengine kutenda yale waliyofanya Ghana ili kumwondoa Nyerere ambaye wakati huo alishakuwa rafiki wa karibu na China. Ndiyo hapo unaweza kusema ilizaliwa Tanzania halisi yenye sura hii iliyodumu sasa kwa miongo mitano.

UCHAMBUZI

# Tanzania kuridhia mkataba wa ACDEG ni kuvuna faida lukuki

Na Gaudensia Mngumi

SEPTEMBA mwaka huu baada ya Kongamano la Kimataifa la Uchumi 'World Economic Forum' lililofanyika huko Uswizi, viongozi wa Afrika walikutana kujadili hatma ya nchi zao kiuchumi. Wakakubaliana kuwa ni wakati wa kuridhia Mkataba wa Afrika wa Biashara Huru.

Mkataba huo maarufu kama 'Africa Continental Free Trade Area (AfCFTA),' ambao kwa miongo kadhaa ya majadiliano bila mafanikio mwaka huu mambo yamebadilika. Umoja wa Afrika (AU) umekubali kuondoa vikwazo vya kibiashara, kuinua uchumi wao na kuiunganisha Afrika kibiashara.

Kwa miongo kadhaa kumekuwa na uhusiano mkubwa wa kibiashara na Ulaya, Amerika na Asia, China hata kuliko mataifa wanachama wa AU.

Rais wa Afrika ya Kusini Cyril Ramaphosa, akitoa taarifa hizo ambazo viongozi wa Afrika wameziridhia anasema, ni afya na tumaini jipya kwa bara hilo.

"Mbele yetu mambo ni makubwa. Yajayo yanafurahisha ni Afrika angavu. Hakuna wakati Afrika inaweza kutamba kama sasa . Hii ni fursa ya kuinuka na kuangaza," anasema Ramaphosa.



Waziri wa Mambo ya Nje, Profesa Palamagamba Kabudi, wizara yake ndiyo yenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa mkataba huo. **PICHA: MTANDAO**

### WAKUMBUSHWA ACDEG

Licha ya kwamba ni vyema Afrika au wanachama wa AU, kuridhia na kuanza kutekeleza mkataba wa Biashara Huru lakini pamoja na hilo mafanikio ya kuondoa vikwazo vya forodha, kodi, ushuru na tozo za aina mbalimbali na kufanyabiashara zote bila kukwamishwa kutafanikiwa iwapo itasaini Mkataba wa Africa wa Demokrasia, Uchaguzi na Uongozi Bora 'African Charter for Democracy, Election and Governance (ACDEG).

Kama ambavyo mwaka huu imejikita kwenye AfCFTA, Januari mwaka 2007 Rais Jakaya Kikwete, akiwa Mwenyekiti wa AU kwa bashasha kubwa alilitangazia Bara la Afrika makubaliano ya kuanza kutekeleza mkataba wa ACDEG.

Sababu ya kuanzisha mkataba huo ilikuwa ni kuwapo hoja kadhaa na mojawapo ni Afrika kuwa na majaliwa mengi hasa rasilimali za kutosha, lakini bara limekuwa makao makuu ya umaskini na ufukara, uongozi duni, rushwa, vita na mauaji na la mwisho kimaendeleo duniani.

Kwa mujibu wa andiko la mkataba huo, ACDEG inalenga kudumisha demokrasia, haki za binadamu, utawala wa sheria na uongozi bora.

Taarifa kutoka Idara ya Siasa ya AU Addis Ababa, inaeleza kuwa nchi nyingi za Kusini mwa Afrika ikiwamo Tanzania hazijaridhia wala kugusa mkataba huo.

Ndiyo maana wadau mbalimbali wanaona kuwa kabla ya kuingia kwenye AfCFTA, taifa liridhie kwanza ACDEG kwani imefanya mambo mengi yaliyomo kwenye mkataba huo.

Wanaona kuwa Tanzania inatambulika kama kisiwa cha Amani, imefanikisha harakati za ukombozi, pia inaheshimika kwa kusimamia utawala wa sheria, uongozi bora ikiwa ni kuheshimu muda wa uraisi madarakani, haki za binadamu na demokrasia, mambo yayotajwa na mkataba huo.

> Mbele yetu mambo ni makubwa. Yajayo yanafurahisha ni Afrika angavu. Hakuna wakati Afrika inaweza kutamba kama sasa . Hii ni fursa ya kuinuka na kuangaza.

Tanzania inaheshimu haki za binadamu na hili linathibitika katika ibara ya 13 ya katiba. Aidha, haki za kiraia na kisiasa zinalindwa kwa mujibu wa ibara ya 12 hadi ya 29 na masuala yote yanayohusu utawala bora yapo kwenye ibara ya 4,21 (1) 46( 2), 46 A na 53. Kadhalika mingi yote ya demokrasia inalindwa kikatiba kuanzia ibara za 5,8,20 na 21.

### FAIDA ZA ACDEG

Wadau mbalimbali wakiwamo vijana, wanahabari, wanasheria na mashirika ya kiraia kama ActionAid, wanaokutana Dar es Salaam kuishauri Tanzania kuridhia, wanasema kuuridhia na kuanza utekelezaji mkataba huo kuna tija.

Mosi unaongeza thamani kwenye katiba yake inayoheshimu demokrasia utawala bora na haki za binadamu.

Pia, unazidi kukubaliana na kuimarisha mipango ya maendeleo , mikakati na jitihada mbalimbali zinazofanywa na nchi kujiletea maendeleo.

Aidha, ni kuimarisha nafasi ya Tanzania kwenye Umoja wa Afrika hasa utawala wa sheria na demokrasia. Taifa limefanya kazi kubwa ya ukombozi kabla ya uhuru wa bara hilo kwa kuuondoa ukoloni mkongwe lakini pia kukabiliana na mapinduzi haramu yanayokwamisha demokrasia.

Kwa mfano iliisaidia Komoro Machi 2008, kuuondoa utawala wa kiimla uliokuwa umekiuka maelekezo ya ACDEG yanayoharamisha mapinduzi na utawala wa kidikteta.

Kwa hiyo wadau hawa wanasema kuwa kuridhia mkataba huo kunaipa Tanzania uhalali wa kutoa msaada huo, hata kama Komoro siku za usoni italalamikia hatua hiyo.

Faida nyingine za kujiunga na ACDEG ni kupata misaada ikiwamo kugharamia shughuli za uchaguzi, elimu ya uraia zinazotolewa kwa vyama vya siasa. Kutolewa kwa fedha hizo kutaisaidia nchi kugharamia uchaguzi ambazo unahitaji fedha nyingi za walipa kodi.

Ushirikiano wa kikanda kupambana na uovu na uhalifu kama rushwa, ufisadi, utoroshaji wa fedha za umma, mihadarati na ujangili na mambo yatakayofanikiwa zaidi baada ya kusaini mkataba wa ACDEG.

Vile vile mkataba huo unahimiza ushirikiano katika kupambana na kulaani rushwa, uhaini na ulinzi wa watu wenye hatia wanaojiona kuwa wapo juu ya sheria (impunity). Matendo yote ya kihalifu, ukiwamo uhaini na utoroshaji wa fedha za nchi kwenda kwenye benki za ughaibuni yanadhibitiwa kwa pamoja.

### KULANDANA NA KATIBA

Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora , unalandana na katiba ya Tanzania kwenye maeneo mengi kama ulinzi wa haki za binadamu, tunu za kidemokrasia, utawala wa sheria, uhuru wa mahakama, ushiriki na ushirikishwaji.

Aidha, Tanzania imeridhia mikataba mingi ya kimataifa kama ule wa Haki za Kisiasa na Kijamii (ICCPR) Mkataba wa Afrika Haki za Binadamu na Watu na Mkataba wa Umoja wa Afrika ambayo yote imesheheni maudhui (contents) ya ACDEG.

Aidha, Mpango mkakati wa maendeleo wa miaka mitano wa 2016/17-2020/2021 unaelezea utayari wa Tanzania katika kutekeleza Mpango wa AU wa Agenda 63 au Afrika Tunayoitaka unaohusika na kuwa na mtangamano madhubuti wa Afrika, inayokuwa imeungana na kuwa na shirikisho kisiasa, sarafu, sheria, katiba, uchumi na uongozi mmoja ifikapo mwaka 2063.

Kadhalika ACDEG inazungumzia maendeleo ya watu, huduma za kijamii kama maji , afya elimu, ajira, vijana, kulinda mazingira na uzalishaji viwandani pamoja na mazingira wezeshi kwa ajili ya maendeleo ya sasa na vizazi vijavyo.

Masuala hayo yameibuliwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 inayoainisha kuwa kujitegemea kiuchumi, amani, uthabiti wa nchi, usalama wa raia na mali zao ni msingi wa maendeleo ya nchi, ambayo pia ndani ya mkataba wa Afrika yanatajwa kuwa ni nguzo ya maendeleo ya bara hilo.

Wadau wanaona kuwa Tanzania imeanza kutekeleza mambo mengi yaliyo kwenye mkataba huo kama kuzuia na kupambana na rushwa kupitia Takukuru na kuanzisha mahakama za ufisadi na uhujumu uchumi, ina taasisi za umma za kusimamia haki za binadamu na uongozi bora -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), yote haya ni kuhakikisha utawala wa kisheria , ulinzi wa rasilimali na uwajibikaji.

Masuala ya maisha bora kwa kila Mtanzania na kutumia mali ya asili ya kwa maendeleo ya nchi na kuwainua raia kutoka umaskini na maisha ya kati ni ajenda kuu ya taifa, kadhalika kuiondoa Afrika kwenye umaskini ndicho kinachosisitizwa na mkataba wa ACDEG.

Wadau wanaiomba serikali iuridhie mkataba huo kwa kuwa unalandana na mipango yote ya maendeleo ya watu, uchumi na ya kisiasa yanayofanyika Tanzania leo.

# Ulivyokamilishwa uchaguzi kanda: Chadema ya 'milima na mabonde'

INATOKA UK.13

yao na pia madiwani kufanya mikutano ya kisiasa kwenye kata zao.

Uchaguzi uliomalizika hadi sasa ni kwenye kanda mbalimbali za chadema, kanda ya Pwani uchaguzi ulifanyika Novemba 28, mwaka huu, ambayo mgombea pekee alikuwa ni Frederick Sumaye, ambaye alipigiwa kura ya ndiyo na hapana.

Sumaye ambaye alikuwa Waziri Mkuu wakati wa serikali ya awamu ya tatu, alibwagwa nafasi hiyo kwa kupata kura 28 za ndiyo na kura 48 za hapana, huku kura moja ikiharibika. Kanda nyingine ni ya Kanda ya Serengeti, alichaguliwa Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko aliyepata kura 44 dhidi ya Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, aliyepata kura 38.

Heche alikuwa Mwenyekiti wa Kanda ya Serengeti tangu mwaka 2014.

Kanda ya Kati aliyeshinda ni aliyekuwa waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii, Larazo Nyalandu, aliyepata kura 60 ikiwa ni asilimia 66.8 kati ya kura 86 zilizopigwa.

Kiongozi wa Kanda ya Kaskazini ni Godbless Lema aliyepata kura 78 dhidi ya Joseph Selasini aliyepata kura 27, huku kwenye Kanda ya Nyasa, akichaguliwa Peter Msigwa aliyepata kura 66 dhidi ya wapinzani wake wawili.

Kanda ya Kusini, Suleiman Matthew aliibuka mshindi kwa kura 53 akiwabwaga wapinzani wake watatu, huku kanda ya Victoria akishinda Ezekia Wenje, aliyepata kura 50 na kuibuka kidedea baada ya kuwabwaga wapinzani wake kadhaa.

Kanda ya Unguja mshindi ni Said Mzee Said na kanda ya Pemba ni Hafidh Saleh, wote wakitarajiwa kuongoza vyema Chadema katika michakato muhimu hadi kuifikisha kwenye uchaguzi Mkuu wa 2020.

Aidha, viongozi hao ndiyo wanaunda Kamati Kuu ya Chadema, ambayo Mwenyekiti na viongozi wengine wa kitaifa watachaguliwa katika uchaguzi utakaofanyika wakati wowote kuanzia wiki ijayo.

Uchaguzi huo wa ndani ya chama unapanga safu ya uongozi wa chama hicho kwa miaka mitano ijayo, ikiwa ni pamoja na kujiandaa na uchaguzi mkuu kwa kuwa kamati kuu ndiyo itakuwa na mamlaka ya kuchuja majina ya wagombea wa chama hicho kwenye nafasi mbalimbali.

Kwa maneno mengine Chadema inapanga safu yake ya kupambana 2020, ambayo huenda ukawa uchaguzi mgumu kwa vyama vya upinzani hasa chama hicho ambacho ni chama kikuu cha upinzani nchini.

Safu hiyo ya uongozi wa kanda na kamati kuu ya chama hicho ndiyo itaonyesha mwelekeo kutokana na aina ya viongozi waliopo, kwa kuwa sasa watakwenda kuimarisha chama na kuchambua watakaojitokeza kuwania nafasi za uongozi kuanzia udiwani hadi urais.

Chadema ikumbuke inaingia kwenye uchaguzi mkuu mwakani



Wanachadema kwenye kampeni za uchaguzi mkuu 2015. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Kwa mtaji huo, Chama Cha Mapinduzi kimekuwa na wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa kwa zaidi ya asilimia 99.9 wanaotokana na chama hicho.

ikiwa na mgombea urais mpya baada ya mgombea wao wa mwaka 2015, Edward Lowassa, kukihama chama na kurudi CCM alikokuwako mwanzoni.

Aidha, kwa sasa kutendawili kikubwa kitakuwa ni nani atapewa ridhaa ya kupeperushwa bendera ya chama hicho katika wakati ambao mgombea wa CCM atakuwa ni rais aliyeko madarakani anayetetea kipndi chake cha pili cha uongozi.

Ni wakati wa kufahamu kazi itakuwa ngumu zaidi kwa kuwa mgombea wa CCM tayari amejenga msingi kupitia uongozi wake wa miaka mitano kwa kufanya mambo mbalimbali ambayo yanagusa maisha ya Watanzania, na huenda akawa hana kazi kubwa sana ya kujinadi majukwaani wakati wa kampeni.

## SERIKALI ZA MITAA

Lakini pia viongozi hao wanakumbuka kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa ulikuwa na sarakasi nyingi kiasi cha vyama vya upinzani kujiondoa dakika za mwisho, na



Freeman Mbowe



Ester Matiko



Frederick Sumaye

wagombea wengi wa CCM kupita bila kupingwa.

Kwa mtaji huo, Chama Cha Mapinduzi kimekuwa na wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa kwa zaidi ya asilimia 99.9 wanaotokana na chama hicho.

Huo ni mtaji wa kisiasa ambao kama ni mkulima mvua imenyesha ameandaa shamba na pembejeo kinachosubiriwa ni mavuno.

Duru za siasa zinasema kwamba safu ya uongozi inayopangwa sasa, ikiwamo nafasi ya mwenyekiti ambayo bado aliyekuwa mwenyekiti Freeman Mbowe, anaitetea, ni kwa ajili ya kujipanga kwa uchaguzi mkuu ujao ambao umejaa changamoto nyingi.

Kwa sasa wapinzani hawaruhusiwi kufanya mikutano kwenye ngazi za kitaifa huku nguvu kubwa ya dola ikitumika kuwadhibiti huku wengi wao wakikabiliwa na kesi mbalimbali dhidi yao ni mambo yanayowataka kutafakari njia zao.

Kwa sasa viongozi wote wa kitaifa wa upinzani wanakabiliwa na kesi mbalimbali kwenye maeneo yao na wengine nje ya majimbo yao ya uchaguzi.

Wapo baadhi wanaokabiliwa na kesi zaidi ya moja. Aidha wabunge wengi wa upinzani na madiwani walihama vyama vyao na kujiunga na CCM yote hayo ni mambo yanayotakiwa kupimwa na kupatiwa ufumbuzi.

Aidha, Mwanasheria na Mnadhimu wa Bunge, Tundu Lissu, ambaye alianza kutangaza nia ya kugombea nyadhifa mbalimbali, amegoma kurudi nchini kwa madai kuwa anahofia usalama wake.

Kutokana na mambo hayo lukuki Chadema inajiwajibika kujipanga upya katika kipindi ambacho inakabiliwa na changamoto ya mashambulizi kwenye mitandao ya kijamii, huku nguvu kubwa ikielekezwa kwa mwenyekiti aliyemaliza muda wake na anayegombea tena, Freeman Mbowe, kuwa

> Umoja wa vyama ni muhimu na ushirikiano na serikali ni jambo lisilokwepeka.

amekaa muda mrefu anapaswa kuachia madaraka.

Kama walivyojipambanua kwenye uchaguzi wa viongozi wa kanda, cha msingi ni kujiamini na kufahamu kuwa umoja ni ushindi na utengano ni mfarakano.

Umoja wa vyama ni muhimu na ushirikiano na serikali ni jambo lisilokwepeka. Lengo ni kuweka na kuimarisha demokrasia na kuongeza kasi ya ukuaji uchumi na hamasa za mabadiliko ya kisiasa yanayolenga kuipandisha chati Tanzania ili kuyafanya maisha ya raia kuwa bora zaidi.

Chadema chama kikuu cha upinzani, kina nafasi ya kuhamasisha uwajibikaji na kwa ujumla kutimiza majukumu yake yaliyoanishwa katika katiba.

## Omar al Bashir aongezewa vikombe zaidi vya mateso



Kiongozi wa zamani wa Sudan, Omar al Bashir.

ULE msemo kuwa mwosha huoshwa unadhihirika hivi karibuni baada ya aliyezoea kunyanyasa, kuumiza na kutesa kiongozi wa zamani wa Sudan Omar al Bashir naye kuanza kuoshwa.

Wiki iliyopita chama tawala cha zamani NCP alichokuwa akikiongoza Bashir kilipigwa marufuku Sudan, hatua inayochukuliwa na viongozi wapya wa Sudan.

Wameamuru chama cha rais aliyeng'olewa madarakani Omar al Bashir kivunjwe na " kukongolewa" mabaki ya utawala wake wa karibu miaka 30.

Kwa kufanya hivyo viongozi hao wapya wameitika wito wa waandamanaji ambao kilio chao kilipelekea kupinduliwa, al Bashir na chama chake cha itikadi kali cha National Congress-NCP wameitawala nchi hiyo ya kaskazini mashariki mwa Afrika tangu mwaka 1989 kabla ya wimbi kubwa la maandamano kupinga kote nchini na kuwang'oa madarakani mapema mwaka huu.

Halmashauri huru ya uongozi wa taifa na baraza la mawaziri linaloongozwa na Waziri Mkuu Abdallah Hamdok , ilipitisha uamuzi wa kukivunja chama hicho na kupitisha sheria ya "kung'olewa utawala wa Juni 30 mwaka 1989."

"Chama cha National Congress kimevunjwa na kimefutwa katika madaftari ya vyama vya kisiasa vilivyosajiliwa nchini Sudan" sheria hiyo inasema na kuongeza kamati maalum itaundwa ili kuwapokonya milki yote waliyonao.

"Hakuna yeyote anaejitambulisha na chama hicho atakayeruhusiwa kujishughulisha na siasa kwa kipindi cha miaka 10 inayokuja.

"Umauzi wa kukivunja chama siyo kisasi dhidi ya watawala wa zamani, anajitetea Hamdok kupitia mtandao wa twitter."

Anasisitiza kuwa umelenga kulinda hadhi na matakwa ya wananchi wa Sudan. Lakini pia sheria hiyo imelengwa kurejesha mali ya wananchi iliyoporwa wakati wa uongozi wa al Bashar.

Aidha, wanaharakati wanaopigania mageuzi wanasifu sheria hiyo, Wajdi Salah msemaji wa vuguvugu la waandamanaji wanaopigania Uhuru na Mageuzi, anasema katika ukurasa wake wa Facebook kwamba "chama tawala cha zamani kitavunjwa moja kwa moja."

Jumuiya ya Wasomi wa Sudan, kundi la wanaharakati walioanzisha maandamano dhidi ya al Bashir wameusifu uamuzi huo."Ni hatua muhimu katika kulifikia lengo la mapinduzi na kufungua njia ya kuunda taifa linaloheshimu demokrasia ya raia., inasema jumuia hiyo katika taarifa yake.

Halmashauri huru ya uongozi wa taifa na baraza la mawaziri wamebatilisha pia sheria inayobishwa iliyokuwa ikibana haki za wanawake chini ya utawala wa Omar al Bashir. Maelfu ya wanawake waliteswa, walitozwa faini au hata kufungwa chini ya sheria hiyo ambayo wanaharakati wanasema iliwalenga wanawake kwa misingi ya sheria kali za dini ya Kiislam.

Chama cha Bashir aliyepinduliwa cha NCP kimelaani uamuzi wa viongozi wapya wa Sudan wa kukipiga marufuku na kusema hawatishiki na amri yoyote au sheria kwakuwa wanatambua wao wana nguvu na fikra zao zitadumu. **DW**

SIKU 16 KUPINGA UKATILI

# Ukatili kijinsia, rushwa unaondoa wanawake anga za siasa, uchumi



Baadhi ya washiriki wa maadhimisho hayo wakifuatilia kwa umakini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

TANZANIA ya Viwanda, wanawake ni msingi wa mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi, hivyo, wakati wanawake zaidi ya asilimia 30 wanaendelea kufanyiwa ukatili wa kijinsia, ni vigumu kwao kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya viwanda na uchumi wa taifa.

Jambo la msingi linalotakiwa hapa, ni mgawanyo bora wa rasilimali wenye usawa na haki kwa wanawake na wasichana ili wafikie fursa za kiuchumi na maarifa, kwani itawasaidia kufanya maamuzi mazuri katika familia.

Si tu katika familia, bali pia kwenye jamii na kuongeza kasi ya maendeleo, kwa vile kuna mahusiano makubwa kati ya haki za kiuchumi, maamuzi, mila na mitazamo potofu na ukatili wa kijinsia.

Haya yanabainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, kwenye maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyofanyika jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

Maadhimisho hayo yenye mada kuu isemayo: "Athari za Ukatili wa Kijinsia Katika Maendeleo ya Tanzania ya Viwanda".

"Ninaamini kukiwa na mgawanyo mzuri wenye usawa na haki wa rasilimali, wanawake na wasichana wataweza kufikia fursa za kiuchumi na maarifa, hii itawasaidia kufanya maamuzi mazuri katika familia," anasema Liundi.

Liundi anasema, ukatili dhidi ya wanawake una athari kubwa si tu kwa wanawake bali pia katika uchumi wa nchi na maendeleo na ustawi wa jamii kwa ujumla, hivyo ni muhimu kuupiga vita.

"Utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia unaonyesha kuwa upotevu wa uzalishaji unaosababishwa na ukatili wa jinsia unakadiriwa kuwa kati ya asilimia 1.2 ya pato la taifa la Brazili na Tanzania na asilimia mbili kwa upande wa nchi ya Chile. Vile vile nchi za Afrika zinapoteza zaidi dola za Marekani milioni 105 kwa kutokuzingatia usawa wa jinsia," anasema.

> Katika kuhakikisha kuwa usalama wa wanawake na watoto nchini, serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa mpangokazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto 2017/2018-2021/22.

Pamoja na mambo mengi ambayo leo, tunajadili hapa, rushwa ya ngono pia imekuwa aina mojawapo ya ukatili wa kingono unaosumbua wanawake katika maeneo mbalimbali ya ya kikazi," anasema.

Vile vile anasema tatizo la rushwa ya ngono kwa jamii linarudisha nyuma jitihada za serikali za kuhakikisha inajengwa Tanzania ya Viwanda kwa kuwezesha wananchi wengi zaidi hasa wanawake kujipata fursa za ajira.

"TGNP Mtandao, tunapenda jamii yote ya Watanzania ielewe kwamba, rushwa ya ngono ni ukatili wa kijinsia, ni kosa kama yalivyo makosa mengine ya rushwa yaliyoainishwa kwenye sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa namba 11 ya mwaka 2007," anasema.

Anasema, utafiti na ushuhuda vinavyotolewa na wanawake, hasa wasichana, tatizo la rushwa ya ngono lipo zaidi kwenye sehemu za kazi, kwa wanaoomba ajira, wanaopanda vyeo, wanaotaka haki zao au wanafunzi kwa walimu wao.

"Tunasisitiza juu ya uboreshaji mazingira ya ajira na mahusiano kati ya mwajiri na mwajiriwa, hasa katika maeneo ya viwanda na sehemu za kazi kwa ujumla ili kutokomeza ukatili wa kijinsia sehemu za kazi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wenye tija kwa maendeleo endelevu," anasema.

Anasema, hatua hiyo itasaidia kukuza na kulinda utu wa mwanamke kwa kutokomeza ukatili wa kijinsia na kuongeza ujasiri kwa wanawake, kukuza maendeleo ya kiuchumi, kupunguza siku sizizo na malipo na kuongeza nguvu katika ongezeko la Tanzania ya viwanda na kutokomeza rushwa ya ngono, kuondoa kabisa vitendo vya kudai rushwa ya ngono, ili kumpatia mwanamke haki zake mahali pa kazi.

**SHERIA KANDAMIZI**

Kwa upande wake Ofisa Mwandamizi wa TGNP Mtandao, Shakila Mayumana, anasema ukatili wa kijinsia unakwamisha maendeleo ya viwanda, kwamba kuwapo kwa sheria kandamizi kumewafanya wanawake kutopata haki zao kikamilifu, ingawa katiba imeainisha kuwapo kwa haki sawa kati ya wanawake na wanaume.

"Bado usawa huo haujafikiwa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wanawake wanajengewa uwezo wa kisheria na kupata haki zao, baadhi ya sheria zimetungwa na zingine kufanyiwa marekebisho," anasema Mayumana.

Anataja baadhi yake kuwa ni Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, the Sexual Offences Special Provisions Act (SOSPA) ya 1998, ambayo imefanyiwa marekebisho na kuhuishwa kwenye Kanuni ya Adhabu.

"Sheria za Ardhi na Ardhi za Vijiji ya mwaka 1999 serikali iliendelea kuzirekebisha mwaka 2004 iliifanyia marekebisho sheria ya utatuzi wa migogoro ya ardhi pamoja na mambo mengine uwakilishi wa wanawake katika mabaraza yanayoamua migogo ya ardhi uliwekwa kisheria ili yawe na sura na uwakilishi kamili wa kijinsia," anasema.

Mayumana anataja Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini namba 6 ya mwaka 2004, ambayo imetoa fursa sawa katika ajira na likizo ya uzazi na pia Sheria ya Utumishi ya mwaka 2002, nayo imetoa fursa sawa za ajira serikalini kwa wanawake na wanaume na kuwapa wanawake kipaumbele katika ajira.

"Sheria kama ya kuzuia usafirishaji binadamu, ya Ukimwi (2008), Sheria ya Mtoto (2009) zimelenga kumpunguzia mwanamke mzigo wa matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa," anasema na kwamba juhudi hizo zote zinaonyesha kuwa kuna utashi wa kisiasa na kuna juhudi za serikali na wadau wengine zinaendelea, ambazo ni muhimu kuzitambua na kuzipongeza.

"Pamoja na mafanikio hayo bado changamoto ni nyingi ndiyo maana leo tuko hapa kuendelea kutafakari na kupanga mikakati ya namna ya kutatua changamoto hizo kwa pamoja," anasema Mayumana na kwamba kauli mbiu ya kitaifa mwaka 2019 katika kuadhimisha siku hizo 16 ni "kizazi cha usawa, simama dhidi ya ubakaji!

**HAKI ZA BINADAMU**

Katika maadhimisho hayo, mgeni rasmi alikuwa ni Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Kamishina Nyanda Shuli na wawakilishi kutoka taasisi mbalimbali, zikiwamo za umma na wadau wa Maendeleo.

Shuli anasema, ili kuwa na maendeleo endelevu kwa wote ni lazima kuzingatia na kuheshimu haki za binadamu na kwamba ili kila mmoja aweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ni lazima awe huru au asikumbane na vitendo vya ukatili, kwamba usalama wa wanawake na watoto dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia ni jambo la msingi kwa maendeleo na ustawi wa taifa lolote.

"Nimeelezwa malengo ya warsha hii ni kuimarisha uelewa wa miongozo mbalimbali katika sekta ya viwanda na uwezeshaji wanawake kiuchumi na kuweka mikakati ya kuwa na sauti ya pamoja na jinsi ya kushughulikia ukatili wa kijinsia katika kukuza Tanzania yenye uchumi pamoja," anasema Shuli.

Anasema, kwa Tanzania wanawake na watoto wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ukatili na kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2015/2016, inakadiriwa kuwa asilimia 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 wamefanyiwa ukatili wa kupigwa au kingono katika kipindi cha maisha yao.

"Kadhalika, asilimia 22 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 walifanyiwa vitendo vya kingono kinyume na matakwa yao, kwa ujumla taarifa hiyo inaonyesha hakuna tofauti kubwa ya mabadiliko katika jamii kuhusu mitazamo na matendo yao kuhusiana na ukatili wa kijinsia," anasema Shuli.

Anasema, katika kuhakikisha kuwa usalama wa wanawake na watoto nchini, serikali kwa kushirikiana na wadau imeandaa mpangokazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto 2017/2018-2021/22.

"Mpango umeshaanza kutekelezwa kwa lengo la kutokomeza ukatili dhidi ya watoto kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022, hivyo nitoe rai kwa wadau wote kutumia mpango huu katika shughuli zao kama sehemu ya kuweka nguvu za pamoja za mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia," anasema.

# Ninavyoikumbuka siku ya uhuru kijijini kwetu

**Na Hilal K. Sued**

JUMATATU ijayo ni Sikukuu ya Uhuru wa Tanzania, uliopatikana Desemba 9, 1961. Ni jambo lilishuhudia kushushwa bendera ya Uingereza au Union Jack na kupandishwa bendera ya Tanzania, saa 6:00 usiku Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mwandishi mbobezi Hilal Sued, alikuwa shuhuda ambaye Tanzania inapokaribia kuadhimisha miaka 59 ya kumuondoa mkoloni, anasimulia mambo yalivyokuwa kijijini kwao.

Ikiwa imetimia miaka 58 tangu tukio hilo ni wakati wa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai kushuhudia hatua (milestone) hii muhimu katika historia ya Tanzania.

Na si tu naikumbuka siku hiyo, bali pia nakumbuka kwa kiasi cha kutosha jinsi ukoloni ulivyokuwa katika miaka michache niliyojaliwa kupata akili kushuhudia hali hiyo kabla ya kuondoka kwa watawala hao wa Kizungu. Ni vigumu kwa Watanzania wengi wa leo kufikiria namna gani ilikuwa kutawaliwa na wageni hao.

Nimezaliwa Oktoba 1946 katika Kijiji cha Usinge, kilichokuwa katika Wilaya ya Tabora (wakati huo) Jimbo la Magharibi, ni mtoto wa sita kuzaliwa kwa mama yangu.

Elimu yangu ya msingi niliipata Shule ya Msingi ya Sopa huko Sumbawanga darasa la kwanza hadi la nne na shule ilikuwa mali ya Kanisa la Katoliki na 1959 niliingia darasa la tano katika Shule ya Kati ya Sumbawanga (Sumbawanga Middle School) ambayo ilikuwa ya bweni na iliyokuwa inamilikiwa na halmashauri ya wilaya ya Sumbawanga, na baadaye mwaka 1963 nilikwenda kwenye Sekondari Wavulana ya Tabora.

Hivyo siku ya uhuru nilikuwa nyumbani Usinge wakati wa likizo baada ya kumaliza darasa la saba.

Ingawa vijijini watawala wa kikoloni au Wazungu hawakuonekana sana nilikuwa na bahati ya kuwaona nikiwa katika shule hizo za kati ambazo zilikuwa katika makao makuu ya wilaya.

Wakuu wa Wilaya au Ma DC na wakuu wa utawala -ma-DO - District Officers) walikuwa Wazungu, ingawa katika miaka ya mwishoni ya ukoloni walikuwapo Waafrika wachache walioshika nyadhifa hizo.

Na vivyo hivyo ilikuwa kwa wakuu wa idara mbalimbali wilayani.Kadhalika katika ngazi za majimbo walikuwa Provincial Commissioners Ma-PC na wasaidizi wao na hakuwahi kuwapo PC Mwafrika.

Kitaifa Gavana alikuwa akimwakilisha Malkia wa Uingereza akisaidiwa na wakuu wa idara mbalimbali ambazo baada ya uhuru zikawa wizara zikiongozwa na mawaziri.

Kijijini Usinge utawala wa kikoloni uliwakilishwa na watemi (machifu) wa maeneo mbalimbali waliokuwa chini ya mtemi mkuu. Eneo letu la Unyanyembe mtemi mkuu ulikuwa ni wa ukoo wa Fundikira.

Watemi hao walilipwa mishahara na serikali ya kikoloni na jukumu lao kuu lilikuwa kuwaunganisha wananchi kuitii serikali ya kikoloni.




Mwalimu Nyerere na hati ya Uhuru Kamili wa Tanzania mwaka 1961. **PICHA: MTANDAO.**

> “Hata zilipoanza harakati za kudai uhuru, sikuelewa maana yake,eti Waafrika wanataka kujitawala wenyewe? Haikuingia akilini hata kidogo.

Kwa ujumla nilikuwa naamini kwamba uwepo wa watawala wa Wazungu ni kitu cha kawaida, sikujua kutawaliwa ni jambo baya. Niseme kwamba wengi wetu wakati huo, hasa wa umri wangu walikuwa wanalikubali hili kwamba ni halali kutawaliwa na Wazungu, kwani wao kwanza ni wasomi, waliostaarabika na wenye ujuzi mkubwa wa kutengeneza mambo mengi, kama vile treni, magari, ndege na meli. Mwanzoni nilifikiri Wazungu walitokea humu nchini ila tu kwa sababu ya rangi yao wakawa watawala.

Hata zilipoanza harakati za kudai uhuru, sikuelewa maana yake,eti Waafrika wanataka kujitawala wenyewe? Haikuingia akilini hata kidogo. Watawezaje kujitawala wakati hawana chochote cha kuwawezesha kufanya hivyo?

Halafu hawa Wazungu wangewaachia nchi na vitu vyote walivyoleta au kuvijenga kama vile treni, viwanja vya ndege, bandari, simu, majengo ya serikali? Tena kwa bure tu? Bado haikuingia akilini wananchi Waafrika wangepata wapi pesa za kuvilipia vitu hivyo kwa namna ya kuvinunua.

Nilikuwa na nawazo haya hasa baada ya kusikia wakubwa wakiyazungumza. Aidha hapo (katika miaka ya mwishoni ya 50) nilianza kusikia habari za Julius Nyerere akihamasisha kudai uhuru, nami niliimuona ni kama vile anafanya dhihaka kubwa. Kitu gani alichokuwa nacho cha kumuwezesha kuwaondoa Wazungu? Yumkini akili zake hazikukaa kisawasawa!

Na wakati huo tulikuwa tunapata habari ya vita ya Mau Mau nchini Kenya ambapo wazalendo walikuwa wanapambana na Wazungu ili waondoke. Baba alikuwa na redio nadhani kati ya mbili au tatu katika kijiji chetu nazo zilikuwa kama sufuria na betri yake ya ukubwa kama tofali.

Kila jioni tukawa tunasikia taarifa ya habari ya redio ya Kenya wakati huo ikiitwa KBS mtangazaji akiwa Stephen Kikumu akitangaza mwenendo wa vita ya Mau Mau nchini Kenya, jinsi wazalendo walivyokuwa wanakamatwa na Wazungu akiwemo kiongozi wao Jomo Kenyatta na mwingine akiitwa Dedan Kimathi. Pia ilinishangaza kusikia kuna wengine katika viongozi hao wa MauMau wakiita Jenerali Tanganyika na Jenerali China.

Nikawa nawaza: Hivi kweli Nyerere na chama chake cha TANU wana majeshi ya kupigana na Wazungu ili waondoke na kuacha vitu vyao vyote walivyovileta na kuvijenga?

Lakini jinsi miaka ilivyokuwa ikienda, ndivyo jinsi nilivyokuwa nikayaelewa mambo haya, hasa habari zilipoanza kutufikia kwamba Uganda pamoja na nchi nyingine za jirani kama vile Congo, Rwanda na Burundi walikuwa wakidai uhuru.

Mwaka 1960 ikaja Serikali ya Madaraka na baadaye ikatangazwa rasmi kwamba Waingereza wamekubali kutoa uhuru tarehe 9 Desemba mwaka 1961. Nikaona haya makubwa sasa! Lakini tusubiri. Shauku yangu ilikuwa huu uhuru utakuja vipi?

### SIKU YA UHURU

Mwanzoni mwa Desemba 1961 tukafunga shule na kurejea kijijini kuusubiri uhuru. Pale kijijini alama pekee ya mamlaka ya utawala wa kikoloni ilikuwa ni mahakama ya mwanzo wakati huo ikiitwa Baraza na hakimu wake aliitwa Mkuu wa Baraza.

Walikuwa Waafrika ambao angalau walikuwa wanajua kusoma lakini bila shaka hawakupata elimu yoyote ya sheria kuendesha mahakama.

Walitumia zaidi sheria za kimila na za kijadi, kwani kesi za jinai pamoja na wahalifu husika hupelekwa wilayani ambako kulikuwa Mahakimu wa Wilaya (District Magistrates) ambao walikuwa ni ma-DO, yaani Wazungu.

Ilitangazwa kwamba sherehe za uhuru kitaifa zitafanyika Dar es Salaam ambapo saa 6:00 usiku bendera ya Waingereza au Union Jack - itateremshwa na ile ya Tanganyika kupandishwa katika Uwanja wa Taifa ambao ulijengwa maalum kwa sherehe hizo.

Sherehe hizo za kuteremsha na kupandisha bendera pia zilipangwa kufanyika katika ngazi za majimbo, wilaya, miji na vijiji pia na serikali ya kikoloni ilitenga fungu la pesa ambazo zilitumwa katika mamlaka husika kufanikisha sherehe hizo. Kijiji chetu kilipata sh 1,500/ kwa ajili ya sherehe hizo.

Hili la kutolewa pesa za sherehe lilitangazwa kijijini na huyo Mkuu wa Baraza ambaye alituarifu kuwa watu wote kijijini pale wakusanyike katika eneo la Baraza (mahakama) kuanzia saa 4:00 usiku wa tarehe 8 Desemba.

Hakukuwa na bendera ya Mwingereza ila mahakamani kulikuwapo picha ya Malikia Elizabeth II iliyokuwa ukutani ndani ya ukumbi wa mahakama nyuma ya kiti cha hakimu.

Hivyo siku chache kabla ilitangazwa kwamba bendera zote mbili - ya kikoloni na ile ya Tanganyika huru zingewasili kwa ajili ya tukio la kupandisha na kushusha bendera.

# Miaka 24 ya Moi alivyoitumia 'kuwashughulikia' wasaidizi



Moi enzi za uongozi wake, uliosifika kwa ubabe na unyanyasaji wanasiasa wengine. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mashaka Mgeta**

KAMA kuna wakati Kenya ilikuwa na utawala uliokabiliwa na matukio yenye taswira tofauti ikiwamo vitisho kwa umma, Agosti 22, 1978 na Desemba 30, 2002 ni kipindi ambacho lazima kingetajwa, zikiwa ni zama za utawala wa Daniel arap Moi.

Zipo hekaya nyingi zinazomzungumzia Moi katika kipindi cha miaka 24 ya utawala wake, miongoni ni ile ya namna alivyotumia mbinu ya kuonyesha imani kwa wasaidizi wake, lakini akiwa hawaamini hata kidogo.

Gazeti la Daily Nation la Kenya limechapisha makala kuhusu Moi na jinsi alivyokuwa kigeugeu kila alipokuwa akiwatumia wasaidizi hao.

Makala hayo yanaelezea kwa nini Moi hakumwamini yeyote katika utawala wake.

Inakumbusha kuwa mwaka 2002, akiwa nyumbani kwa waziri wa zamani katika serikali ya Moi, Dk Munyua Waiyaki, mwandishi alimuona aliyewahi kuwa Katibu Mkuu katika utawala huo, Balozi Bethuel Kiplagat, wawili hao walikuwa marafiki wa karibu wanaotajwa kufanana kwa hulka.

Wakati huo, Dk Waiyaki na Balozi Kiplagat walikuwa wamestaafu kitambo, lakini wakateuliwa na kamati ya ukaguzi wa mishahara ya wabunge nchini humo.

Miongoni mwa mambo yanayofananisha wawili hao ni kuwahi kuitumikia Wizara ya Mambo ya Nje, ingawa kwa nyakati tofauti na mmoja akiwa Waziri na mwingine Katibu Mkuu.

Katika mazungumzo yao, makala inakumbusha kuwa Dk. Waiyaki alielezea namna Balozi Kiplagat, alivyokuwa mmoja wa watu wachache walioaminika kwa Moi.

"Kwa kweli, nilifanya kazi kwa karibu na Moi. Lakini hajawahi, kumuamini kabisa mtu. Niamini, hakuna mtu hata kidogo, " Balozi Kiplagat anakaririwa.

Anaendelea, "uliaminika tu na Moi wakati ulikaa naye. Wakati umetoka, aliye adui yako angeweza kukaa mahali ulipokuwa na kubadili yote mliyoyaongea na kukubaliana na Rais. "

> Unajua rafiki yangu, kosa langu kubwa wakati nikiwa Mnikulu, nilidhani nilifanya kazi kwa taasisi inayoitwa Ikulu na serikali. Nilipofukuzwa kazi, nikagundua nilikuwa nikifanya kazi kwa kampuni inayoitwa Moi.

Balozi Kiplagat anasema aliyekuwa mshauri mahiri wa Moi, ni yule aliyekuwa anaongea naye mwisho, anatoa mfano unaomhusu wakati alipokuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje, Moi, alimteua kuwa mjumbe maalum wa usuluhishi wa vyama hasimu nchini Msumbiji - Frelimo na Renamo.

Anasema katika utekelezaji wa majukumu yake, alibaini kuwa moja ya vikwazo vikubwa kwa amani nchini Msumbiji, ni ushawishi na kuingiliwa na bilionea wa Uingereza, Tiny Rowland, aliyekuwa anafadhili moja ya vyama hivyo ili kulinda masilahi ya biashara zake Afrika Kusini.

Mfanyabiashara bilionea Rowland, akatajwa pia kuwa mtu aliyekuwa na urafiki wa karibu na Moi, kutokana na uwekezaji wake mkubwa Kenya.

Kwa mujibu wa Daily Nation, uwekezaji wa Rowland Kenya ulikuwa chini ya uangalizi wa Mark Arap Too, aliyeaminiwa kwa kiwango kikubwa na Moi.

Kutokana na hali hiyo, Balozi Kiplagat alibaini kwamba asingeweza kufanikisha kuleta suluhu nchini Msumbiji kutokana na muingiliano wa maslahi kati ya Moi na Rowland, hivyo akapata ujasiri wa kumuomba Moi, amuondoe kwenye jukumu hilo.

Tofauti na matarajio yake, Balozi Kiplagat anasema Moi hakulikubali ombi lake na kumshangaa kwa hatua hiyo wakati taarifa zilizomfikia kutoka Msumbiji zilieleza kwamba alikuwa anafanya kazi nzuri.

Kuamini Rais akimaanisha alichosema, Balozi Kiplagat akamimina moyo wake na kumwambia Moi jinsi Tiny Rowland na Mark Too walivyokuwa wakikatisha tamaa katika harakati zake za kuleta amani nchini Msumbiji.

Kutokana na kutoamini ukweli unaotokana na kile kilichosemwa na Rais, Balozi Kiplagat alimjulisha Moi namna ambavyo Rowland na Mark Too walivyokuwa wanamkwamisha kutekeleza majukumu yake.

Balozi Kiplagat anasema Moi alimtazama kwa 'macho makavu' na kuwambia, "sahau juu ya Tiny Rowland. Pia Marko Too. Wanajua nini kuhusu diplomasia? Wapuuze tu na ufanye kazi ambayo nimekupa uifanye. "

Jibu hilo la Moi lilimfanya Kiplagat kuondoka Ikulu akiwa amedhika na kuamini kwamba kiongozi huyo wa nchi alimwamini kikamilifu. Anasema baadaye alikutana na Mark Too aliyemsalimu huku akitoa 'kicheko cha mashaka'.

Siku tatu baadaye, Kiplagat alisikia kupitia Redio ya Taifa kuwa Moi 'alimtumbua' kutoka nafasi ya Katibu Mkuu na kumpeleka kuwa mwenyekiti wa moja ya mashirika ya umma.

Mtu mwingine aliyewahi kuwa Waziri katika utawala wa Moi, Joseph Kamatho, anasema katika vuguvugu la 'vigogo' wa KANU kukihama chama hicho mwaka 2002, wakiongozwa na aliyekuwa Makamu wa Rais, George Saitoti, Moi alimwalika kwenye chakula cha jioni, nyumbani kwake na kumshawishi asiondoke.

Kamotho anamkariri Moi alipomhoji, "kwanini umfuate huyo Saitoti, wewe ni mtu wangu ninayekuamini lakini si Saitoti.

Hata hivyo, Kamotho anaelezea kumhoji Moi, "lakini Saitoti amekuwa makamu wako wa muda mrefu na mwaminifu?"

Moi "Ndiyo, lakini haimaanishi kwamba ninamtegemea. Tazama, ninawezaje kumwamini mtu ambaye hajawahi kutujulisha kuhusu asili yake?

"Tena, nasikia ana fedha nyingi sana na hakuna mtu anayejua amezipata wapi? Unawezaje kumwamini mtu kama huyo"

Kamotho anasema alishangazwa kwa kauli hiyo ya Moi kuwa na Makamu wa Rais asiyemwamini kwa miaka 12 licha ya katiba ya wakati huo kumpa mamlaka ya kumtumbua makamu.

Kamotho anakumbusha tukio jingine, kwamba alipochaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa KANU, Moi alimruhusu kushika nafasi yake ya Mwenyekiti wa tawi la Murang'a licha ya kuwa ni kinyume na katiba ya chama hicho.

Lakini hatima ya yote, aliyekuwa Mwenyekiti wa Taifa wa KANU kwa wakati huo, Peter Oloo Aringo, alimtaka Kamotho ajiuzulu moja ya nafasi hizo.

Kutokana na hisia kwamba Aringo asingefikia uamuzi huo pasipo kumhusisha Rais wa nchi, aliwasiliana na Moi kabla ya kuchukua uamuzi.

Kamotho anamkariri Moi akimjibu, "Aringo anaongea sana. Nitamwambia afanye kazi yake na kukuacha ufanye zako."

Lakini Aringo hakuacha kumtaka Kamotho atekeleze wajibu huo wa kikatiba kwa KANU. Kamotho, akiwa 'amechanganyikiwa', alitaka kujua undani wa kinachoendelea, akawasiliana na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais aliyekuwa na nguvu za ushawishi, Hezekia Oyugi.

Oyugi, akamueleza Kamotho, "Ndugu kama ningekuwa wewe, ningeenda kwa Rais na kumwambia nataka kujiuzulu nafasi ya Mwenyekiti wa KANU tawi la Murang'a. Hilo ndilo kusudio la Moi lakini hatakuambia. Anamtuma Aringo kupitisha ujumbe huo."

Kamotho alielewa na kutekeleza ushauri aliopewa, akajiuzulu nafasi hiyo. Hatua hiyo inaelezwa kumfurahisha sana Moi.

Katika siku hizo, Oyugi alikuwa mtu wa kuaminika sana kwa Moi - kwa kiwango aliruhusiwa kuanzisha mtandao wa kukusanya taarifa za kiintelijinsia na kufanya kazi pamoja na taasisi za upelelezi.

Ukaribu wake na Moi ulifikia hatua kwamba alipokuwa akizungumza, Moi hakuna mtu yeyote aliyeruhusiwa kuingia, akiwamo Mkuu wa Huduma za Umma (aliyekuwa bosi wa Oyugi).

Lakini katika hali isiyotarajiwa, siku moja utawala wa Moi ulimkamata Oyugi na kumuweka ndani kwa wiki mbili, akihusishwa na mauaji ya aliyekuwa Waziri, Robert Ouko.

Baada ya kuachiwa huru, Oyugi aliugua ghafla na kupelekwa hospitalini jijini London, Uingereza alipofariki dunia.

Moi hakutuma salamu za rambirambi na pole, na pia hakuhudhuria mazishi ya 'wa karibu yake' huyo, Oyugi!

Aliyekuwa Mnikulu wa muda mrefu katika serikali ya Moi, Abraham Kiptanui, ni miongoni mwa mashuhuda wa kusimulia habari za kwamba, kwa mstaafu huyo wa Kenya, faida ilikuwa wakati mkikaa pamoja na baada ya kuachana, akili yake ilijiekeleza kwa masuala mengine.

Kiptanui alijiaminisha kuwa mwaminifu kwa Moi, akatumika kuwapeleleza watu wengine walokuwa waaminifu kwa Moi .

Siku moja Kiptanui alifika ofisini kwake, Ikulu jijini Nairobi na kujulishwa kuwa Rais (Moi) alisafiri kwenda Nakuru, jambo ambalo hakulijua licha ya kuwa ndiye mtunza kumbukumbu za kiongozi huyo wa nchi.





# Uwekezaji Saut wamkuna waziri

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amesema serikali itaendelea kushirikiana na taasisi binafsi vikiwamo vyuo vikuu vinavyomilikiwa na taasisi za dini katika kuboresha sekta ya elimu.

Ndalichako alisema hayo jijini hapa alipokuwa anazindua majengo ya kisasa ya ofisi za wahadhiri na hosteli za wanafunzi wa Chuo cha Mtakatifu Augustine (Saut) Tawi la Mbeya na alifurahishwa na uwekezaji wa chuo hicho.

Alisema uwekezaji unaofanywa na chuo hicho kwenye miundombinu ina tija na ni moja ya utekelezaji wa vitu ambavyo serikali inasisitiza katika kuweka mazingira bora ya utoaji elimu kwa Watanzania.

Sekta binafsi, alisema ni muhimu sana katika kuwaletea maendeleo na kwamba ndio maana serikali inashirikiana na taasisi binafsi kwenye utekelezaji wa mambo mbalimbali yakiwamo maendeleo ya elimu ambayo alisema ni sekta muhimu.

"Uwekezaji wenu ni wa hali ya juu sana. Nawapongeza kwa kazi nzuri na niwahakikishie kwamba serikali itaendelea kushirikiana nanyi kwa sababu mambo mnayoyafanya yanaonekana. Mnatekeleza yale ambayo tunayahitaji kwa ajili ya Watanzania," alisema Prof. Ndalichako.

Alisisitiza kuwa serikali inataka mazingira ya kutolea elimu yawe bora na miundombinu iliyopo ni sehemu ya mazingira yanayotakiwa.

Pia alisema chuo hicho kimeweka mazingira bora kwa ajili ya watoto wa kike kwa madai kuwa hosteli zilizojengwa zitawasaidia kutoka jirani na mazingira ya chuo badala ya kutoka maeneo ya mbali ambako watakuwa wanatumia muda mwingi kusafiri.

Mkurugenzi wa Saut Tawi la Mbeya, Prof. Romuald Haule, alisema jengo la ofisi ya wahadhiri limegharimu Sh. milioni 800.8 kukamilika na jengo la hosteli ya wasichana imegharimu Sh. bilioni 1.531.

Alisema hosteli iliyojengwa chuoni hapo kwa ajili ya wasichana, ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 420 kwa wakati mmoja na huduma zote muhimu zinapatikana na hivyo wanafunzi hawatalazimika kwenda nje wakati wa usiku.

**"Uwekezaji wenu ni wa hali ya juu sana. Nawapongeza kwa kazi nzuri na niwahakikishie kwamba serikali itaendelea kushirikiana nanyi kwa sababu mambo mnayoyafanya yanaonekana. Mnatekeleza yale ambayo tunayahitaji kwa ajili ya Watanzania," alisema Prof. Ndalichako.**

# Rungwe walia na mgawo wa maji

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

VIONGOZI wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wameuomba uongozi wa Wakala wa Maji Mijini na Vijijini (Ruwasa), kuelekeza fedha nyingi kwenye miradi ya wilaya hiyo kwa madai kuwa kuna vyanzo vingi vya huduma hiyo, lakini bado kuna mgawo.

Walitoa ombi hilo wakati wa kikao cha wadau wa maji kilichowashirikisha viongozi mbalimbali wa mkoa wakiwamo wakuu wa wilaya, wakurugenzi, wenyeviti wa halmashauri na watendaji wa Ruwasa.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema wilaya hiyo ina vyanzo vingi vya maji, lakini katika mji wa Tukuyu kuna uhaba mkubwa hali inayowafanya wananchi waendelee kuteseka kutembea umbali mrefu kufuata huduma.

Alisema kuna mgawo wa maji na baadhi ya maeneo katika mji huo wanapata huduma hiyo mara mbili kwa wiki, hivyo kuendelea kupata shida licha ya kuwapo vyanzo vingi.

"Mji wetu wa Tukuyu umezungukwa na vyanzo vingi vya maji, lakini wananchi wanapata maji kwa mgawo. Sasa mmesema mna pesa nyingi kwa ajili ya miradi, tunaomba mzielekeze huko ili kukamilisha miradi hiyo," alisema Chalya.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Ezekiel Mwankota, alisema miundombinu iliyopo katika mji huo ilijengwa enzi za wakaloni, hivyo imechakaa na haina uwezo wa kusambaza huduma kwa ufasaha.

Alisema miundombinu hiyo iliwekwa mwaka 1933 wakati watu walikuwa wachache, lakini kwa sasa idadi ya watu ni kubwa na miundombinu hiyo haiwezi kuwatosheleza tena.

Mwakota alisema vyanzo vya maji vilivyokuwa vinatumika kwa wakati huo mpaka sasa vipo vizuri isipokuwa kinachotakiwa kuboreshwa ni mabomba ya kupeleka maji kwa wananchi.

"Mabomba yaliyokuwa yanatumika kwa wakati huo yana kipenyo kidogo, lakini kwa sasa kutokana na mahitaji kuongezeka, tunatakiwa kubadilisha mabomba ili yatosheleze mahitaji," alisema Mwakota.

Alisisitiza kuwa baadhi ya miradi ambayo ilikuwa inatekelezwa na serikali wilayani humo mpaka sasa haina ufanisi kutokana na makandarasi na baadhi ya wasimamizi kutotekeleza wajibu wao ipasavyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Mbeya (Mbeya-WSSA), Ndele Mengo, aliwataka wananchi kuwa na vifaa vya kuhifadhia maji ya ziada kwenye makazi yao ili kuepuka kupata shida inapotokea hitilafu.

Alisema vyanzo vingi vya maji vinavyotumika mkoani humo vinatumia nishati ya umeme na kwamba wakati mwingine huwa inatokea shida ya kukatika umeme, hivyo kusababisha huduma ya maji kukatika pia.

Mengo alisema endapo mtu ana tangi la kuhifadhi maji nyumbani kwake inakuwa rahisi kuendelea kuyatumia wakati hitilafu ya umeme iliyotokea inashughulikiwa.



Vibarua wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), Mkoa wa Mbeya, wakishirikiana kuvuta mti kwa kutumia kamba ili usiangukie ukuta wa Shule ya St. Agrey ya jijini humo, wakati wa zoezi la kupunguza miti kwenye njia ya umeme, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ulevi watajwa chanzo ukatili kijinsia

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

IMEELEZWA kuwa ulevi uliopindukia ni miongoni mwa vyanzo vya kukithiri kwa ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto pamoja na maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya na Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Mkoa wa Mbeya, Janeth Masangano, alipokuwa anatoa elimu kuhusu masuala ya ukatili ikiwa ni mwendelezo wa siku 16 za kupinga ukatili.

Alisema mara nyingi watu ambao wanalewa kupita kiasi, wanakuwa hawawezi kujizuia kufanya jambo lolote, hivyo baadhi ya mambo ambayo wanayafanya inakuwa ukatili wa kijinsia.

Masangano alisema mtu aliyelewa haoni hatari kubaka au kulawiti watoto, hivyo akawataka wananchi kuepuka kulewa kupita kiasi ili kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia.


"Lakini mtu aliyelewa hawezi kukumbuka kutumia kondomu wakati wa tendo la ndoa na hivyo kuwa rahisi kupata maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kisha kuwaambukiza wengine. Kwa hiyo lazima tuwe makini sana," alisema Masangano.

Alisema ofisi yake inaendelea kutoa elimu kupitia vyombo vya habari, mikutano ya hadhara na kupita kwenye maeneo hatarishi kutoa elimu kwa makundi yanayoshinda huko.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kwa sasa wanaingia hata kwenye vilabu vya pombe kwa ajili ya kutoa elimu hiyo ili kila kundi lifikiwe na elimu hiyo muhimu ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

Alisisitiza kuwa wanaingia vilabuni kwa sababu baadhi ya watu wanaotumia pombe ndio mahali pekee huwa rahisi kuwafikia na kuwapatia elimu.

Hata hivyo alisema baadhi ya wazazi huwa wanaingia vilabuni kunywa pombe wakiwa na watoto wao wachanga na kwamba kitendo hicho kinahesabika kuwa ni unyanyasaji wa watoto lakini baadhi ya watu wanafanya hivyo kwa sababu hawajui.





# Sheria ndogo utunzaji mazingira zaandaliwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, amesema wapo kwenye mchakato wa kuandaa sheria ndogo mbili za utunzaji wa mazingira, ambazo zitawaelekeza wakazi wa Dodoma rangi za mabati wanazotakiwa kutumia katika ujenzi pamoja na upandaji wa miti kila kaya.

Kunambi aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa mradi wa miaka mitatu wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira ambapo miti 3,400 imepandwa katika eneo la Medelii.

Alisema kuifanya Dodoma kuwa kijani ni lazima sheria hizo zianzishwe ili kusaidia kuwasukuma watu kuhamasika kupanda miti katika maeneo tofauti.

"Tupo kwenye mchakato wa kuandaa sheria mbili moja kwa ajili ya mipango miji iwaelekeze wananchi rangi gani wanatakiwa kuzitumia kwenye mabati, aina gani ya nyumba wanatakiwa kujenga pamoja na upandaji miti kuanzia mitano kulingana na ukubwa wa kiwanja chake bila kujali ni miti gani," alisema Kunambi.

Hata hivyo, alisema kumekuwa na changamoto kubwa ya kupanda miti mingi bila kuisimamia ambapo baada ya muda ukifanya tathmini miti mingi inakuwa imekufa, hivyo miti hiyo ni lazima isimamiwe kwa ukaribu.

Meneja Mradi huo wa Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF), Savinus Kessy, alisema yapo mambo matatu ambayo yamepewa kipaumbele katika mradi huo, kusafisha mazingira hasa kwenye taka ngumu kama vile plastiki, kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya Jiji.

Alisema suluhisho la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ukame pamoja na maporomoko ni upandaji wa miti na ndio maana wameamua kuanzisha mradi huo Dodoma ili kusaidia juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais.

Alisema WWF wameanza kushirikiana na sekta binafsi katika kampeni za uboreshaji na utunzaji mazingira.

Alifafanua zaidi ya kuwa wamejipanga kuhakikisha mazingira ya upandaji miti yanaimarishwa na kuangaliwa kwa ukaribu ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.



Washiriki wa maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu, wakisikiliza watoa mada (hawapo pichani), kwenye kongamano la kujadili changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu lililofanyika kimkoa wilayani Kondoa, mkoani Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wito kutoficha watoto wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila, KONDOA**

WAZAZI na walezi wenye watoto walemavu wilayani Kondoa, wametakiwa kuacha vitendo vya kuwaficha majumbani badala yake wawapeleke shuleni ili kupata haki ya msingi ya elimu.

Rai hiyo imetolewa na wadau wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) yakiwamo mashirika, taasisi, viongozi wa dini walipokuwa wakijadili changamoto zinazowakabili wenye ulemavu kwenye Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu.

Maadhimisho hayo yaliyofanyika kimkoa wilayani Kondoa, ambapo wadau hao walisema vitendo vya kuwaficha watoto majumbani vinawakosesha haki sawa katika kupata elimu na ni ukatili.

Wadau hao wakiwamo Plan International, Umati, Marie Stopes, LHRS, Tanzania Cheshire Foundation na Jeshi la Polisi, walisema pia kitendo hicho kimekuwa kikichangia ongezeko kubwa la umaskini kwenye familia husika zinazowaficha watoto hao.

Kadhalika, wadau hao walikemea ukatili wanaofanyiwa watu wenye ulemavu, ukiwamo mauaji, ubakaji na ulawiti, hivyo wameitaka serikali kuwachukulia hatua za kisheria ili kukomesha vitendo hivyo.

Kwa upande wake, Shivyawata imeziomba halmashauri kuongeza asilimia mbili zinazotolewa kwa ajili ya mikopo kutoka mbili na kuwa nne kwa kuwa haitoshelezi kujikwamua kiuchumi.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Mkoa wa Dodoma, Yusuph Mloli, alisema asilimia mbili zinazotolewa kwa ajili ya watu wenye ulemavu haikidhi mahitaji yao, na kwamba hata hizo mbili hawapewi.

Naye Katibu wa Shivyawata Mkoa wa Dodoma, Justus Ng'wantalima, alisema maadhimisho hayo kwa mwaka huu kwa upande wa wadau wao wametoa elimu kwa ajili ya kuwawezesha watu wenye ulemavu kuzitambua haki zao za msingi.

## Sababu mimba utotoni yatajwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

BAADHI ya mila na tamaduni za kabila la Wagogo zinadaiwa kuwa chanzo cha mimba katika umri mdogo, kutokana na wazazi kuwajengea watoto nyumba za peke yao wanapofikia umri wa balehe, imeelezwa.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Manchali Wilaya ya Chamwino, Hawa Lissu, wakati wa mkutano wa hadhara katika kijiji cha Wilunze.

Mkutano huo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa 'Sauti Yangu' unaoratibiwa na Shirika la Woman Wake Up (Wowap) kwa ufadhili wa Shirika la Child Fund Korea kupitia Jukwaa la Haki za Watoto.

Lissu alisema kwa mujibu wa tamaduni za Wagogo, binti au kijana anapofikia umri wa balehe hatakiwi kuishi nyumba moja na wazazi wake, hivyo wanajengewe nyumba kando.

"Watoto wakikua wanajengewa nyumba pembeni, jambo hilo limekuwa likitoa uhuru mkubwa kwa watoto wa kike kujiingiza kwenye mapenzi kulingana na mazingira waliyopo," alisema.

Alisema ni muhimu kwa jamii kubadilika na kuwa na jukumu la malezi kwa watoto wanapofika umri huo kwani ni kipindi ambapo kijana anapitia mabadiliko mbalimbali kwenye mwili wake.

Pia alisema tatizo la mimba kwa wanafunzi linatokana na changamoto ya mazingira na uchumi wa kaya kwa ujumla.

Alisema wazazi wengi hawana muda wa kufuatilia watoto wao wako wapi, na katka maeneo mengine watoto wanaambiwa wajiongeze ili waweze kupata mahitaji.

Lissu alisema tangu Januari hadi sasa kuna wanafunzi tisa wameshafukuzwa shuleni hapo kutokana na kupata ujauzito.

"Tunajitahidi sana kuelimisha wanafunzi wasiingie kwenye ngono katika umri mdogo, walimu tumekuwa tukikaa na watoto wa kike na kuwaeleza athari za ngono," alisema.\Diwani wa Manchali, Mary Mazengo, alisema suala la ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto limekithiri sana kwenye kata hiyo.

Alisema ulifika wakati ilipitishwa sheria ndogo iwapo mzazi mtoto wake akipata mimba katika umri mdogo atatozwa faini ya Sh. 400,000.

"Tulipanga mkakati wa kutoza faini ya Sh. 400,000 kwa mzazi wa mtoto wa kike aliyepata mimba, lakini tukaona lile suala la simjui aliyenipa mimba linazidi kuongezeka na wazazi wakawa wanamudu gharama za kulipa faini, tunatafuta mbadala mwingine sasa," alisema.

Alisema mwaka huu kuna wanafunzi tisa wa shule ya sekondari waliopata ujauzito na kuna jumla ya wanafunzi 53 wa shule za msingi na sekondari waliofukuzwa shule kwa sababu mbalimbali ikiwamo utoro.

"Lazima kuwa na mkakati wa kusaidia watoto wa kike, ukifikiria hao mabinti tisa waliopoteza dira za maisha yao wanakwenda wapi alihoji Lissu. Mratibu wa Wowap, Nasra Suleiman, alisema jamii ina wajibu wa kuhakikisha inakuwa na dhamira ya kulinda watoto wa kike ili kufikia ndoto zao.

# Utafiti mafuta, gesi wafikia pazuri

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema matokeo ya utafiti wa nishati ya mafuta na gesi bado haujakamilika na uko katika hatua za mwisho za kusoma mistari ya picha zilizopigwa.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Nishati, Salama Aboud Talib, alisema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi kuhusu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliotaka kupewa taarifa za matokeo ya utafiti wa mafuta na gesi.

Salama alisema mkataba wa mgawanyo wa mafuta na gesi ulitiwa saini Novemba 23, mwaka jana, na baada ya hapo kazi ya utafiti ilianza mapema.

Alisema kampuni ya Rakgas kutoka Rasilkhema iliipa kazi ya kufanya utafiti kampuni ya BGC kutoka China kwa kupiga picha za angani na kufanya mitetemo ardhini na baharini.

Kwa mujibu wa waziri, kazi inayofanyika ambayo inahitaji uangalizi wa hali ya juu ni kutafsiri mistari ya picha zilizopigwa katika maeneo mbalimbali vikiwamo vitalu vya mafuta vilivyoko Unguja na Pemba.

Alisema serikali inafuatilia kwa karibu sana utafiti huo na matokeo yake yatakapokuwa tayari wananchi watajulishwa.

"Hivi karibuni nilikuwa Malaysia kwa ajili ya kufuatilia matokeo ya utafiti wa mafuta na gesi kazi iliyofanywa na kampuni ya BGC kutoka China," alisema.

SMZ kwa kushirikiana na Rakgas kutoka Rasilkhema zimeingia makubaliano ya kufanya utafiti wa nishati na gesi katika vitalu vilivyoko Unguja na Pemba.



Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani, Salum Ali Salum (kushoto), akizungumza na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yussuf Masauni aliyefika katika Baraza la Wawakilishi kusikiliza uendeshaji wa baraza hilo, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Shein ataka uvuvi wa kisasa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kwa muda mrefu wavuvi wa Zanzibar wamekuwa wakivua katika maeneo ya bahari yaliyo karibu ambayo tayari yameashiria upungufu wa upatikanaji wa samaki.

Amesema hatua hiyo imesababishwa na shughuli za uvuvi za kila siku katika maeneo hayo kuwa tishio kubwa kwa mazingira ya bahari.

Dk. Shein aliyasema hayo juzi mjini Zanzibar wakati wa uzinduzi wa boti mpya ya uvuvi (Sehewa 02) inayomilikiwa na Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (Zafico), sambamba na uzinduzi wa boti tatu za doria zinazomilikiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Alisema mipango ya kuimarisha uchumi wa bahari inaendelea vizuri ikiwa ni pamoja na jitihada za kununua vyombo vipya vya baharini vilivyo na ubora na kuwashajihisha wawekezaji kuwekeza katika eneo hilo.

Alisema Serikali ya Zanzibar inakusudia kuunda idara itakayokuwa katika Wizara ya Fedha na Mipango kusimamia uchumi wa bahari.

Dk. Shein alisema serikali imepata ufadhili wa Dola za Kimarekani milioni 8.8 kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), ambazo zitatumika katika kuimarisha sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Pia alisema fedha hizo zitatumika kwa kujengea viwanda vidogo vya kusarifu samaki na mazao mengine ya baharini Unguja na Pemba.

Alisema ili boti hizo zifanye kazi zake vizuri lazima kuhakikishwe kwamba wako wataalamu wazuri wa kuziendesha na kuzishughulikia.

"Lazima kutumiwa vizuri boti hizi za doria kwa ajili ya kulinda maeneo ya bahari, fukwe na rasilimali za bahari ambazo baadhi yao ni muhimu kwa sekta ya utalii ambayo ni muhimu mkuu wa uchumi," alisema.

Alisema uvuvi katika eneo la bahari kuu kwa sasa unafanyika kupitia meli kubwa za kigeni ambazo huwa zimepatiwa leseni za uvuvi kutoka Mamlaka ya Bahari Kuu na hadi sasa wastani wa meli 100 zinavua katika ukanda huo kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Dk. Shein, tani 12,276.2 za samaki wa aina ya jodari na jamii zake zimevuliwa na meli kutoka Taiwan, Oman, Shelisheli, Korea, Thailand, China, Ufaransa, Hispania, na Mauritius ambazo zimepewa leseni ya uvuvi wa bahari kuu.

Alisema kuna haja ya wananchi kuongeza bidii katika kuzitumia rasilimali za bahari ili kufaidika moja kwa moja na matunda yake badala ya kusubiri kupokea faida kutoka mkono wa pili.

Naye Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema serikali imetumia fedha nyingi katika ununuzi wa boti hizo hatua ambayo ni miongoni mwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020.

Alisema mafanikio ya ununuzi wa boti hizo sambamba na kuifufua upya Zafico, yote hayo yanatokana na usimamizi imara wa Dk. Shein katika kuhakikisha sekta ya utalii inaimarika.

## SMZ, AfDB zateta ukarabati wa uwanja

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ZANZIBAR imesema mazungumzo yanaendelea kati yake na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya kuufanyia matengenezo makubwa uwanja wa ndege wa Karume ulioko Pemba.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud Mohamed, alisema jana alipokuwa akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati inayochukuliwa na serikali katika kuimarisha uwanja huo.

Alisema AfDB imeonyesha nia ya kuufanyia matengenezo makubwa uwanja wa ndege wa Karume ili ufikiye kiwango cha hadhi ya kimataifa.

Aboud aliyataja maeneo ambayo yatafanyiwa matengenezo makubwa kuwa ni ya kuruka ndege na kutua pamoja na jengo la abiria.

"Katika mikakati ya kuimarisha viwanja vya ndege nchini, Uwanja wa Ndege wa Karume ulioko Pemba, tutaufanyia ukarabati mkubwa na kuwa na hadhi ya kimataifa. Wenzetu Benki ya Maendeleo ya Afrika wameonyesha nia ya kutupatia fedha," alisema.

Alisema hatua ya ukarabati wa uwanja huo kwa kiasi kikubwa itasaidia kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea kisiwa hicho.

Waziri alisema hivi sasa serikali iko katika mchakato wa kutathmini wananchi fidia ya mazao yao ambayo yataathirika na upanuzi wa uwanja huo.

"Tumekutana na wananchi mara tatu kuzungumzia kuhusu suala la fidia kwa wale watu ambao mali zao au mashamba yao yataathirika na upanuzi mkubwa wa uwanja wa ndege wa Karume," alisema.

Aidha, Aboud alisema mazungumzo yanaendelea kwa ajili ya kulifanya Shirika la Ndege nchini (ATCL) ndege zake kutua Pemba.

Naye Mwakilishi wa Chake-chake, Suleiman Sarhani, alisema kisiwa cha Pemba kinakabiliwa na tatizo la usafiri wa ndege baada ya Kampuni ya Precision Air, iliyokuwa ikitoa huduma kusitisha safari zake.

**"Katika mikakati ya kuimarisha viwanja vya ndege nchini, Uwanja wa Ndege wa Karume ulioko Pemba, tutaufanyia ukarabati mkubwa na kuwa na hadhi ya kimataifa. Wenzetu Benki ya Maendeleo ya Afrika wameonyesha nia ya kutupatia fedha," alisema.**

# Serikali yaanika ukweli wakimbizi wa Burundi

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imepinga tuhuma zinazoelekezwa kwamba Tanzania imekuwa ikiwafukuza wakimbizi kutoka Burundi wanaoishi katika makazi na kambi mbalimbali katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, katika kikao kilichojumuisha serikali ya Burundi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) na Tanzania yenyewe.

Katika mkutano huo, kumesainiwa mkataba maalumu uliohusisha pande zote tatu lengo likiwa ni kuwezesha urejeshwaji wa wakimbizi walioomba kurejea makwao baada ya amani kurejea.

"Ni vyema tukaliweka hili wazi ili jumuiya za kimataifa na mataifa mengine yajue kwamba tunaposema tunawarejesha wakimbizi wa Burundi, nchi hizi mbili tunafanya uhamasishaji kwa walio na hiari warudi Burundi.

"Tunapofanya hivi, wenzetu wanatafsiri kwamba tunawafukuza wakimbizi, hii siyo sahihi, Tanzania na wananchi wake kwa ujumla wamekuwa wakipokea wakimbizi kutoka nchi mbalimbali na hatujaanza leo tumekuwa tukiwahifadhi na amani inaporejea wanaomba warejee katika nchi zao."

Naye Waziri wa Mambo ya Ndani kutoka nchini Burundi, Pascal Barandagiye, alisema kwa sasa Burundi ina amani na wameona ipo haja ya raia wake warejea ili kuweza kuijenga nchi yao.

"Tunawahakikishia kama nchi tuna uwezo wa kupokea Warundi 2,000 kwa wiki na tutahakikisha wote wanarejea nyumbani, tutawafuata popote walipo, tunawahitaji warudi nyumbani ili tukajenge nchi yetu pamoja," Barandagiye alisema.

Naye Kamishna Msaidizi wa Shirika UNHCR, George Okoth, alisema wameshirikiana na nchi mbili za Tanzania na Burundi katika kuhakikisha yanakuwapo mazingira salama na yenye utu katika uendeshaji kazi hiyo.

"Tanzania imekuwa nchi rafiki ya wakimbizi, mawaziri wote wawili wamekubaliana suala la kurudi Warundi nchini kwao, tuko hapa kuhakikisha urudishaji huo unakwenda salama kwa kuzingatia ustawi wa pande zote tatu," alisema.

Mwezi mmoja umepita tangu Rais John Magufuli kufanya ziara ya kikazi Mkoa wa Katavi na kuagiza pande zote zinazohusiana na masuala ya wakimbizi wakutane ili kuweza kujadili suala la Warundi wanaojiandikisha kwa hiari kurudi nchini kwao.

# Washauriwa kilimo himilivu

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WAKULIMA na wadau wa kilimo Wilaya ya Wete Pemba, wameshauriwa kuendeleza mbinu bora za kilimo himilivu ili kuongeza uzalishaji wa mazao kwa faida yao na Taifa.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Mkuu Idara ya Kilimo Pemba, Amour Juma Muhammed, wakati akifungua mkutano wa siku moja wa kutoa marejesho kwa wakulima kuhusiana na shamba darasa msimu wa kilimo 2018/2019, katika ukumbi wa Jamhuri Wete.

Amour alisema kuwa iwapo wakulima watatumia fursa katika kuyatumia mashamba darasa pamoja na kueneza taaluma walionayo kwa wenzao, uzalishaji utakuwa mkubwa.

"Ni imani yetu kuwa mmepata maelekezo mazuri na wenyewe mnajua hakika kuwa mbinu ya kilimo himilivu ambayo mmeelekezwa katika uoteshaji wa mazao ina faida, nawasihi muwe mabalozi msiwe wachoyo kwa wenzenu," alisema Amour.

Msaidizi Mkurugenzi Baraza la Mji wa Wete kwa upande wa kilimo, Makame Hamad Said, alisema kwa kiasi kikubwa imesaidia ongezeko la uzalishaji kupitia mbinu zinazoendana na mabadiliko ya mazingira kwa msimu uliopita.

Makame alieleza kuwapo kwa ushirikiano mkubwa wa wadau wa kilimo mafanikio yamepatikana kupitia mbinu bora na hata kwa wakulima ambao hawakuwa na mashamba darasa pia walikuwa na mwelekeo kupitia taarifa za hali ya hewa.

Ofisa tathmini kutoka Taasisi ya Kilimo ya Kimataifa (IITA), Raymond Francis, alisema kupitia ushiriki mkubwa wa kinamama mashambani, iko haja ya kutoa miongozo inayohitajika ili waweze kujikomboa kupitia kilimo.

Mmoja wa washiriki, Muhammed Suleiman Muhammed, alisema serikali na wahisani wamefanya jambo zuri kwa wakulima katika kuwaelekeza namna na kufahamu misimu na njia zinazoweza kuhimili mazingira ambayo itapunguza hasara kwa wakulima kwa upande wa mazao.

Saum Ali Hamad, aliwashauri wakulima wenzake kuwa na mabadiliko kwa kuacha kilimo cha mazoea badala yake walime kwa kufuata mbinu za wataalamu ambazo ndio utakaokuwa mkombozi mkubwa kwao.

Mshiriki wa mkutano huo, Biamu Abdi Gulamu, aliipongeza Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kuwaandalia mafunzo yanayoelewesha mwelekeo wa misimu kwa shughuli za kilimo, huku akiomba kusogezewa kuduma karibu ili kupunguza matatizo katika upatikanaji wa pembejeo kila zinapohitajika.



Mkuu wa wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu (wa pili kushoto), akimkabidhi cheti cha kuhitimu mafunzo ya ujasiriamali, mmoja wa wasichana waliokimbia ukeketaji na kulelewa na nyumba salama ya taasisi ya Hope for Girls and Women Tanzania iliyopo mjini Mugumu, katika mahafali yaliyofanyika wilayani humo, mkoani Mara juzi. Kulia ni Mchungaji Stephen Korokoni, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Rhobi Samwelly na Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Mwita Mseti. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wasaidizi wa sheria waonywa rushwa

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WASAIDIZI wa sheria mkoani Shinyanga kutoka Shirika la Paralegal Aid Centre (PACESH), wameonywa kutoendekeza masuala ya rushwa wanapotoa msaada wa kisheria kwa wananchi.

Wasaidizi hao wameelezwa kuwa kujiweka kando na vitendo vya rushwa kutawasaidia wananchi kupata haki zao kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalibainishwa juzi na msajili msaidizi wa watoa huduma za kisheria Mkoa wa Shinyanga, Tedson Ngwale, wakati akifungua mafunzo ya kuwajengewa uwezo wa sheria wasaidizi wa sheria 64 kutoka halmashauri sita za mkoa huo ambazo ni Msalala, Ushetu, Kahama Mji, Kishapu, Shinyanga Manispaa na Vijijini.

Alisema wasaidizi wa sheria wana umuhimu mkubwa hasa kwa wananchi wa hali ya chini katika kuwasaidia kupata haki zao kwa mujibu wa sheria, kutokana na idadi kubwa ya wananchi kutozijua sheria, na wengine kukosa fedha za kuweka mawakili kusimamia kesi zao, hivyo hatarajii kusikia kuwapo mianya ya rushwa.

"Napenda kutoa tahadhari kwenu nyie wasaidizi wa sheria, mafunzo haya yakawe chachu ya mabadiliko ndani ya jamii, kwa kusaidia kupata haki zao wale wananchi wa hali ya chini ambao hawazijui sheria, mkawapatie huduma stahiki ili kuwatatulia matatizo yao na siyo kwenda tena kuanza kuomba rushwa," alisema Ngwale.

"Kumbukeni watu ambao mnakwenda kuwahudumia ni wale ambao hawana uwezo wa kifedha wala kuzijua sheria, ambao mara nyingi wamekuwa wakidhulumiwa haki zao kutokana na elimu duni ya sheria, hivyo nyie mkawe msaada kwao na mkiwaomba rushwa kazi yenu itakuwa haina maana tena," aliongeza.

Meneja mradi wa huduma wa msaada wa kisheria, John Shija kutoka Shirika la Pacesh mkoani Shinyanga, alisema watafundishwa namna ya kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi hususan kwenye masuala ya ardhi, jinai, mikataba, ajira, mahusiano kazini, sheria ya ndoa, mtoto, mirathi, pamoja na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Baadhi ya washiriki, Twaha Kiliza kutoka Manispaa ya Shinyanga, alise-

HABARI KIMATAIFA

# Boko Haram washambulia kituo cha jeshi

**NDJAMENA,** Chad

NGOME za jeshi la Chad imelengwa na mashambulizi ya kundi la Boko Haram juzi usiku katika Jimbo la Ziwa Chad.

Shambulio hilo ambalo mamlaka nchini Chad inalihusisha kundi la Boko Haram limeuwa askari 13, wakati maofisa wawili wa afya na dereva wao waliotekwa nyara na wanamgambo hao wa Kiislamu bado hawajapatikana.

**Shambulio hilo ni jipya ambalo limetekelezwa na tawi la kundi la Boko Haram...**

Shambulio hilo lilitokea kati ya Ngouboua na Baga Sola, katika eneo lenye watu wengi na kwamba Jeshi liliweka kambi siku za nyuma baada ya daktari, muuguzi na dereva wao kutekwa nyara kwenye barabara hiyo baada ya wanajihadi kufanya shambulio la kuvizia kwa kufyatua risasi dhidi ya askari.

Wakati huo huo, Jeshi la Chad lilijibu na kuwatimua washambuliaji, ambao walirudi nyuma na miili 13 ya wapiganaji wenzao. Askari wanne wa Chad waliuawa katika mapigano hayo na wengine watatu kujeruhiwa.

Shambulio hilo ni jipya ambalo limetekelezwa na tawi la kundi la Boko Haram, lenye mfungamano na kundi la Abu Musab al-Barnawi, ambalo linadhibiti eneo la Kaskazini mwa Ziwa Chad. **RFI**



Abiria wakiwa wamekwama kwenye barabara inayotokea Kapenguria, Jimbo la Pokot Magharibi mwa Kenya baada ya mvua kubwa kuharibu barabara hiyo. **PICHA: AFP**

## Nato yaadhimisha miaka 70 kuundwa kwake

**LONDON,** Uingereza

VIONGOZI wa nchi 29 wanachama wa jumuiya ya kujihami ya Nato wamekusanyika mjini London Uingereza jana katika mkutano wa kilele wa siku mbili ambao unajumuisha pia maadhimisho ya miaka 70 tangu kuundwa kwa jumuiya hiyo.

Rais wa Marekani, Donald Trump tayari amewasili mjini London kuhudhuria mkutano huo wa kilele, ambao kwa mujibu wa chanzo kimoja cha habari kutoka serikali ya Ujerumani, utakuwa muda wa kujitafakari kwa azma ya kuimarisha ushirikiano wa kisiasa miongoni mwa nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

Hayo yanaendana na pendekezo la Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas, ambaye ametoa wito wa kujadiliwa kwa matatizo ya ndani ya jumuiya hiyo.

Matukio ya hivi karibuni Kaskazini mwa Syria yameziacha baadhi ya nchi wanachama katika hali ya mshangao, iliyomfanya Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron kutoa kauli kali, ikiwamo ile kwamba jumuiya ya Nato imekufa kimawazo. **DW**

## Trump amshambulia Macron kisa Nato

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump amemkosoa vikali mwenzake wa Ufaransa, Emmanuel Macron kwa kusema Muungano wa Kujihami kwa mataifa ya Magharibi (Nato) ni ubongo uliyokufa na kuongeza kuwa tamko lake ni matusi.

Rais Trump yuko nchini Uingereza kuhudhuria mkutano wa Nato unaoadhimisha miaka 70 tangu ulipobuniwa.

Akiwa katika mkutano na wanahabari, Rais Trump alisema Nato, inajukumu muhimu na matamshi ya Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron ni matusi.

Rais Trump alisema anaona Ufaransa ikijiondoa kutoka kwa Nato, lakini hakuelezea sababu zake.

Nato uliundwa baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia kukabaliana na kitisho cha uwezekano wa kuendelea kuwapo kwa Soviet. Rais Macron alielezea muungano huo kama ubongo uliokufa, akisisitizia kile alichoiona akieleza kuwa anachokiona kama kutokuwa na utashi wa mdhamini mkuu wa Marekani.

Mkutano huo ulioanza jana tayari umekumbwa na mzozo mkali kati ya wanachama wake Ufaransa na Uturuki, pamoja na muendelezo wa suala la mchango wa mataifa mwanachama.

Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, alisema kwamba atapinga mpango wa Nato wa kiulinzi kwa nchi za Baltiki iwapo haitaiunga mkono Uturuki katika vita vyake dhidi ya kikundi cha Kikurdi ambacho inakichukulia kama kigaidi.



Macron



Trump

Mataifa wanachama wa Muungano huo 29 waliahidi kusaidiana iwapo mmoja wao atashambuliwa.

Lakini kulingana na mazungumzo ya Rais Macron mwezi uliopita, alilalamikia ukosefu wa wanachama wa Nato kwamba hawatoi tena ushirikiano katika masuala muhimu. Mwezi uliopita, Rais Macron aliitaja Nato kuwa muungano usio na maana akisema kuwa wanachama wake hawashirikiani kuhusu masuala muhimu.

Rais Trump ni miongoni mwa viongozi watakaohudhuria mkutano huo na kwamba aliwasili nchini Uingereza siku ya Jumatatu kabla ya hafla maalum itakayoandaliwa na malkia katika kasri la Buckingham Palace.

Rais Trump pia anajiandaa kufanya mazungumzo ya pembeni na viongozi wa Ujerumani, Ufaransa na Katibu Mkuu wa Nato.

Hali ya taharuki imekuwa ikiongezeka tangu Rais Trump, alipolalamika mara kadhaa kuwa mchango wa mataifa ya Ulaya ambayo ni wanachama wa Nato haukidhi mahitaji ya shirika hilo ambalo lilibuniwa kukabiliana na vitisho baada ya vita vikuu vya pili vya dunia ili kupanuka kwa ukomunisti baada ya vita vya pili vya dunia.

Mkutano huo unafanyika wakati ambapo Rais Trump anakabiliwa na uchunguzi kuhusu tuhuma dhidi yake huku akijiandaa kwa kampeini ya uchaguzi mwaka ujao. Kama mwenyeji wa kongamano hilo la siku mbili, Johnson anatarajiwa kutilia mkazo umuhimu wa umoja wa Nato, kama nguzo ya usalama katika kanda ya Euro-Atlantic ambayo inasaidia kuweka watu bilioni moja.

Kabla ya ziara yake, Rais Trump aliandika katika ukurasa wa mtandao wa kijamii wa Twitter kujipongeza kuhusu tamko la hivi karibuni la Katibu Mkuu wa Nato, Jens Stoltenberg la kuongeza bajeti.

Nato inakadiria kuwa kufikia mwaka 2019 ni mataifa manane miongoni mwao Marekani ndio yalioafikia viwango vya mchango uliowekwa kama ilivyokubaliwa na mataifa wanachama.

Mataifa hayo yalikubaliana kwamba yatumie asilimia mbili au zaidi ya pato la jumla la serikali kwa ulinzi.

Stoltenberg siku ya Ijumaa alisema kufikia 2020, washirika wa Ulaya na Canada watakuwa wamewekeza dola bilioni 130 tangu 2016, mwaka ambao Rais Trump alichaguliwa. **BBC**

# Rais Magufuli ataka mkandarasi kukamilisha machinjio Dec. 31

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemtaka mkandarasi anayejenga machinjio ya kisasa ya Vingunguti jijini Dar es Salaam ahakikishe anakamilisha ujenzi huo mwishoni mwa mwezi huu kama alivyoamriwa na Rais Dk. John Magufuli.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi huo jana, Waziri Mkuu amesema amefurahishwa na hatua ya mkandarasi huyo ambaye ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ya kuongeza idadi ya wataalamu na mafundi ili kuhakikisha kazi hiyo inafanyika haraka na kukamilika kwa wakati ulioamriwa na Rais Desemba 30, mwaka huu.

Alisema amefurahi pia kuona kwamba mkandarasi huyo ameamua kufanya kazi usiku na mchana, hatua ambayo imeongeza kasi ya ujenzi huo na anaamini kuwa kazi hiyo itakamilika kwa wakati.

Alimtaka Mshauri Mwelekezi wa mradi huo ambaye ni M/Scons Afrika Limited na FB Consultant wa Dar es Salaam, asimamamie kwa karibu ili kujiridhisha kuwa maelekezo yote yaliyopo kwenye michoro ya ujenzi huo yanazingatiwa na mkandarasi.

Waziri Mkuu, alisema serikali imeamua kujenga machinjio hayo ya kisasa ya Vingunguti baada ya kugundua wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake katika machinjio hayo, walikuwa wakifanya kazi zao kwenye mazingira duni na nyama iliyokuwa ikitoka kwenye machinjio hayo ilikuwa haikubaliki kwenye soko la nje ya nchi.

"Uamuzi wa serikali kujenga machinjio haya, utaifanya nyama inayotoka hapa ikubalike kwenye masoko ya nje ya nchi, hatua ambayo itaongeza mzunguko wa fedha kwenye eneo hili wakati serikali na manispaa watanufaika kwa kuwa kutakuwa na ongezeko la makusanyo ya kodi," alisema Majaliwa.

Pia ameuagiza uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Manispaa ya Ilala kufanya mazungumzo na uongozi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) ili ijengwe reli ya mchepuko kutoka reli ya kati kwenda kwenye machinjio ya Vingunguti ili mifugo iingizwe moja kwa moja kwenye machinjio hayo badala ya kuteremshiwa Pugu halafu ikapelekwa kwa magari.

Aliwahakikishia wafanyabiashara wote wanaoendesha shughuli zao kwenye machinjio hayo kuwa ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Vingunguti hautawafanya wapoteze fusa zao za biashara au kuajiriwa kwenye eneo hilo kwa kuwa machinjio hayo yatafungua fursa zaidi za biashara na ajira kwao.

Aliwaagiza Mkuu wa Wilaya ya Ilala na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala wahakikishe wanaushirikisha uongozi wa wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake wa Vingunguti ili wanachama wao wenye sifa za kuajiriwa, waajiriwe na pia wawaandalie mazingira ya kufanya biashara mbalimbali karibu na machinjio hayo.

Akizungumzia soko na bei duni ya ngozi za mifugo nchini, Waziri Mkuu amekemea tabia ya wafugaji ya kuweka alama kwenye ngozi za mifugo yao hasa ng'ombe kwa kuwa kufanya hivyo kunashusha thamani ya ngozi za Tanzania na badala yake amewataka waweke alama za hereni kwenye masikio ya mifugo yao ili kulinda ubora wa ngozi.

Vile vile, alisema serikali imempata mwekezaji kutoka Misri ambaye amekubali kuwekeza kwenye kiwanda cha ngozi cha Mwanza hatua ambayo italihakikishia taifa soko la ngozi.

Mapema, akitoa taarifa kwa Waziri Mkuu, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Jumanne Shauri amesema ujenzi wa machinjio hayo ulianza Julai 8, mwaka huu na mkandarasi alitakiwa akamilishe Januari 6, 2021. Amesema kufuatia agizo la Rais Magufuli alilolitoa Septemba 16, mwaka huu, ujenzi huo unatakiwa ukamilike ndani ya miezi mitatu yaani ifikapo Desemba 31, 2019.



Meneja Mwandamizi Serikali za Mitaa wa Benki ya CRDB, Suzan Shuma (wa pili kulia), akikabidhi madawati na viti 240 kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntimika katika kitongoji cha Lupa, jijini humo, mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya shule za sekondari na msingi zilizopo katika kata sita za kitongoji hicho. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wazalishaji bidhaa wanolewa masoko

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

WAZALISHAJI wa bidhaa mkoani Lindi, wamepatiwa elimu kuhusu masuala ya viwango hatua itakayowawezesha kupanua masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi.

Elimu hiyo ilitolewa na maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) wakati wa Maonyesho na Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Tanzania (MOWE) ambayo yalianza Novemba 27, mwaka huu na kumalizika juzi wilayani Ruangwa, mkoani Lindi.

Maadhimisho hayo yalienda sambamba na maonyesho ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na wanawake wajasiriamali na pia kutoa nafasi nzuri ya kuwaleta pamoja na Taasisi za serikali, sekta binafsi na wadau wengine.

Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, alisema mbali na kutoa elimu kwa wazalishaji, pia walitumia fursa hiyo kufafanua kuhusu majukumu mapya yaliyoongezwa baaada ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) kubadilishiwa majukumu yake.

"Tumeshiriki kuwafahamisha kuhusu fursa ya bure kwa wajasiriamali wadogo na wakati, kwani ni fursa inayolenga kumwinua mzalishaji kuweza kushindana na kuuza bidhaa zake ndani na nje ya nchi bila wasi wasi," alisema Mayugu.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, alisema amefarijika sana kufahamu jitihada zilizofanyika kuwahamasisha na kuwapa hamasa wanawake nchini kutumia vema fursa za kibiashara na rasilimali zinazopatikana.

Alisema maonyesho hayo yamekuwa sehemu ya kuwawezesha washiriki kubaini na kuzitumia vema fursa mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana kitaifa, kikanda na kimataifa.

Alisema wanatambua kwamba wanawake ni chachu ya maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote duniani, na wana uwezo mkubwa wa kuchangia pato la Taifa.

# Mawaziri 12, wawekezaji uso kwa uso

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MAWAZIRI 12 na Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali wanatarajia kukutana leo na wafanyabiashara na wawekezaji zaidi ya 500 kwa ajili ya kusikiliza, kupokea kero na changamoto.

Pia watapokea mapendekezo na kutoa ufafanuzi kwa lengo la kusaidia kukuza uwekezaji katika Mkoa wa Morogoro.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alisema jana kuwa mawaziri akiwamo yeye, watasikiliza wawekezaji na wafanyabiashara katika mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara kwa mkoa wa Morogoro.

Waziri hao ni wa Maji, Prof. Makame Mbarawa; Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi; Waziri Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango; Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla; Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene na Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo.

Wengine ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana, Sera, Uratibu na Bunge na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama; Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa; Waziri Kilimo, Japhet Husunga; Waziri wa Nishati, Dk. Mederd Kalemani na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina.

Alisema lengo la mkutano huo ni kusikiliza na kutatua changamoto, kuimarisha ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi na kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa maslahi ya uchumi wa nchi.

Waziri Kairuki alisema katika mkutano huo, mawaziri kwa pamoja watapata fursa ya kutolea maamuzi ya papo kwa papo kwa hoja zitakazojitokeza na zingine kuchukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Aliwataka wawekezaji na wafanyabiashara kutumia fursa ya mkutano huo kueleza changamoto walizonazo, kwani kuwapata mawaziri wote kwa wakati mmoja si jambo rahisi, na kwamba maamuzi mengi yatafanyika na hoja nyingine kuchukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**MATHEMATICS TUITION.** Mlete kijana wako tufuatilie msingi wake wa hisabati hadi pale shida ilipoanzia na kuanza kuujenga tena upya. Wahusika ni kuanzia darasa la tano hadi kidato cha sita.Tuitions za majumbani zinapatikana pia. Tupo Bunju Mwisho dsm. Simu 0655.0754 617987

## KAZI /AJIRA


**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA CHETI



**EZEKIELI ALIPHONSI MDEE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0731-0197 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MAKONGO HIGH SCHOOL mwaka 2015.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/MSI/RB/120386/2019.

215542902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No; 235/2019

Ombi la JAMES EXAVERY FRANCIS, LENATA LEONARD kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu EXAVERY FRANCIS.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/11/2019.

115542602

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SOCIETY OF THE PRECIOUS BLOOD inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 540 ADX NISSAN PATROL.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: WMB/RB/9265/2019.

115543102

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

AVITO KANUTI LESHABARI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 351 DDY STATION WAGON.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DSM/PHQ/RB/518178/2019.

115543602

---

### KUBADILI UMILIKI WA GARI

**BW.TYALLAMBULLA MPANDA MAKALLA** WA SLP.1464 DODOMA ANAFANYA UHAMISHO WA GARI NO.T 669 AYG TOYOTA MARK 11 GX 110 KUTOKA KWA KASSU HUSSEIN BACHU KUJA KWA TYALLAMBULLA MPANDA MAKALLA .

YEYOTE MWENYE PINGAMIZI ATOE NDANI YA SIKU 14 KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.

115543502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;236/2019
Ombi la MARIA MWANDU (2)ELIAMAN ELINEEMA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ELINEEMA M. MAHIMBA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/11/2019.

115542702

---

**FORM II**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo: DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 89/2019**

**Ombi la ELIZABETH ANDREW MWACHA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu MARIA SALOME SABAYA.**

**Kwa: YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**TANZANIA, BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 12/12/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 3/11/2019.

215544402

---

### KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**STEPHANO B. JEREMIA a**natangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya yenye namba za usajili **MC 905 CBG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa **ya polisi:**

**DOD/DOD/RB/526659/2019.**

215544302

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CITY FURNITURE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 649 AFH TOYOTA DYNA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi:

Taarifa ya polisi:

**DAR/OST/RB/4672/2019.**

115543702

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NYUMBA YA SANAA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 278 ABJ TOYOTA HILUX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi:

Taarifa ya polisi:

**DAR/OST/RB/4572/2019.**

115543802

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ADAM HALFAN MLONGANILE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 885 DJG MAZDA CX7.** CHASIS NO: **ER3P102275.** ENGINE **NO: L3EAA2275. RANGI: MAROON.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/509861/2019.**

215544102


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# AUBAMEYANG AMTABIRIA LJUNGBERG KITU ARSENAL

**LONDON,** England

FREDDIE Ljungberg anaweza kuipa Arsenal "kitu maalum" kwa kipindi chake akiwa kocha wa muda, kwa mujibu wa nahodha, Pierre-Emerick Aubameyang.

Winga huyo wa zamani wa 'Washika Bunduki' hao amepewa jukumu la kuinoa timu hiyo kwa muda, baada ya kufukuzwa kwa Unai Emery na kwenye mchezo wake wa kwanza alitoka sare ya kufungana 2-2 na Norwich City Jumapili.

Aubameyang alifunga mara mbili kuiwezesha Arsenal kupata sare hiyo kwenye Uwanja wa Carrow Road, lakini Washika Bunduki hao walifikisha mechi ya nane bila ushindi kwenye mashindano yote.

Hata hivyo, Aubameyang anajiamini kwamba Ljungberg - ambaye alishinda mara tano mataji akiwa anacheza pale Arsenal - anaweza kuinyanyua klabu wakati ikitafuta kocha mpya.

"Anaweza kutupa kitu fulani maalum," mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon alisema. "Kama sijakosea alikuwa sehemu ya kikosi kisichofungika.

"Mafanikio yake ya uchezaji yanaonyesha. Tutajaribu kumfuata na kufanya kitu bora zaidi kwa ajili yake. Kila mmoja anamheshimu Freddie. Ameichezea Arsenal, anajua kama mchezaji unajisikiaje.

# Van Dijk atia neno kukosa Ballon d'Or

**PARIS,** Ufaransa

VIRGIL van Dijk amebainisha kwamba, "anaheshimu uwezo" wa wachezaji baada ya kupoteza katika tuzo ya Ballon d'Or kwa Lionel Messi.

Mshambuliaji huyo wa Barcelona na Argentina, Messi alishinda tuzo ya sita na kuweka rekodi akiwa amefunga mabao 41 katika mechi 44 kwa klabu yake ya Barcelona, huku akishinda taji la 10 la Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, msimu uliopita.

Mafanikio ya kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya yalimjumuisha kwenye tuzo hizo, wakati Van Dijk alipoisaidia Liverpool kuifunga Barcelona kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita.

Kiwango cha Van Dijk kwenye michuano hiyo na ile ya Ligi ya Mataifa ya Uefa akiwa na Uholanzi, kimemwezesha kumaliza katika nafasi ya pili kwenye tuzo ya Ballon d'Or.

"Ilikuwa ya kufurahisha," alisema Van Dijk.

"Kwa bahati mbaya kuna wachezaji wengi kama yeye, lakini yeye alistahili zaidi nafikiri.

"Inavutia. Kushinda mara sita Ballon d'Or, unahitaji kuheshimu kiwango chake. Nilikaribia kuitwaa, lakini mtu mwingine kaibeba, na ilikuwa sawa.

"Najivunia kwa kile nilichofanikiwa kwa mwaka jana nikiwa na Liverpool, Uholanzi na nina matumaini naweza tena kufikia mafanikio hayo mwaka huu.






# Liverpool yapewa Everton Kombe la FA

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL amepangwa kucheza na Everton kwenye mchezo wa raundi ya tatu wa Kombe la FA, wakati bingwa mtetezi Manchester City ataanza kutetea taji lake dhidi ya Port Vale.

Toffees watacheza na kikosi cha kocha Jurgen Klopp leo Jumatano kwenye mchezo wa Ligi Kuu na watakwenda tena kwenye dimba la Anfield wiki hii ya kwanza ya Januari 2020 kwenye mchezo huo wa FA.

Kikosi cha Pep Guardiola, City ambacho kiliifumua Watford mabao 6-0 kwenye fainali ya FA msimu uliopita, sasa kimepewa timu hiyo inayonolewa na kocha John Askey ikiwa Ligi Daraja la Pili na itaanza katika Uwanja wa Etihad.

Manchester United itakabiliana na wapinzani wao kwenye Ligi Kuu ya England, Wolves, ambao msimu uliopita waliwatoa kwenye mashindano hayo hatua ya robo fainali, huku Arsenal watawakaribisha vinara wa Ligi Daraja la Kwanza Leeds United kwenye Uwanja wa Emirates.

Kocha mpya wa Tottenham, Jose Mourinho ataiongoza timu yake dhidi ya Middlesbrough, ikiwa inanolewa na mlinzi wa zamani wa Spurs, Jonathan Woodgate, na Chelsea itacheza na Nottingham Forest.

Mechi hizo zitapigwa kati ya Januari 3 na 6, mwakani.

Ratiba yote ya FA raundi ya tatu:

Leicester City v Wigan Athletic
QPR v Swansea City
Fulham v Aston Villa
Chelsea v Nottingham Forest
Wolves v Manchester Utd
Charlton A. v West Brom
Rochdale au Boston Utd v Newcastle United
Cardiff City v Forest Green Rovers au Carlisle United
Oxford United v Exeter City au Hartlepool United
Sheffield Utd v AFC Fylde
Southampton v Hudders' Town
Liverpool v Everton
Bristol City v Shrewsbury Town
Bournemouth v Luton Town
Brighton and Hove Albion v Sheffield Wednesday
Bristol Rovers au Plymouth Argyle v Coventry City or Ipswich Town
Eastleigh or Crewe Alexandra v Barnsley
Man City v Port Vale
M'brough v Tottenham
Reading v Blackpool
Watford v Tranmere Rovers
P.North End v Norwich City
Millwall v Newport County
Crystal Palace v Derby County
Solihull Moors au Rotherham United v Hull City
Brentford v Stoke City
Fleetwood Town v Portsmouth
Arsenal v Leeds United
Gillingham v West Ham
Burton Albion v Northampton Town
Burnley v Peterborough United
B'ham City v Blackburn Rovers

# Oxlade-Chamberlain asifia ari Liverpool

**LIVERPOOL,** England

ALEX Oxlade-Chamberlain anaamini kwamba ari ya Liverpool ndio imekuwa nguzo kuu ya kutawala kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

Vijana hao wa kocha, Jurgen Klopp wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa pointi nane kileleni baada ya mechi 14, wakiwa wameshinda 13 na kutoka sare mara moja.

Oxlade-Chamberlain mwenye umri wa miaka 26, amesema imani ya Liverpool imefanya kila kitu kuwa rahisi.

"Akili ya wachezaji wote iko sawa, kila mmoja anapokwenda kwenye mchezo anafikiri namna ya kushinda. Nafikiri hivyo ndivyo tunavyofikiri," alisema akinukuliwa na Gazeti la The Telegraph.

"Tunakwenda kwenye mechi tukiwa na matarajio makubwa ya kushinda na kwa uhakika tunakuwa kwenye wakati bora kabisa.

"Ukiwa na ari ya namna hiyo kwa wachezaji, unapoingia kwenye mchezo unakuwa na uhakika wa kushinda kwa asilimia 100 na hivyo ndivyo tunavyofanya mara zote."

Liverpool haijafungwa katika mechi 15 kwenye mashindano yote na leo Jumatano watacheza dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja Everton kabla ya kuwavaa Bournemouth Jumamosi.




# SANCHO MCHEZAJI BORA DORTMUND



**DORTMUND,** Ujerumani

JADON Sancho ametajwa kuwa mchezaji bora wa Novemba wa Borussia Dortmund, huku kukiwa na uvumi kwamba anaweza kuondoka katika klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alikuwa na mwanzo mbaya mwezi huo, wakati alipotolewa kipindi cha kwanza huku timu yake ikifungwa mabao 4-0 kutoka kwa Bayern Munich Novemba 9.

Alirudi kwenye mchezo uliofuata kwa kufunga bao dhidi ya Paderborn na Hertha Berlin, pamoja na kwenye kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sancho - amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa, ikiwamo Manchester United na Liverpool na amefunga mabao saba kwenye mechi 18 alizoichezea Dortmund kwenye mashindano yote msimu huu.

Nyota huyo wa zamani wa Manchester City anatajwa kwamba, ana nafasi kubwa zaidi ya kujiunga na Man United pale Old Trafford.




# *Messi: Rekodi yangu ya Ballon d'Or itavunjwa*

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi anaamini kwamba rekodi yake ya kutwaa mara sita tuzo ya Ballon d'Or itavunjwa.

Messi mwenye umri wa miaka 32, alitwaa tuzo hiyo kwa mara ya sita juzi Jumatatu jijini Paris akiwashinda mlinzi wa Liverpool, Virgil van Dijk na nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo.

Wakati Ronaldo akiwa pia ameshinda tuzo hiyo mara tano, Messi anahisi kwamba mtu mwingine anaweza kupata zaidi ya sita.

"Nafikiri hivyo. Sijui ni nani, lakini kuna uwezekano," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Rekodi zinawekwa ili zivunjwe, lakini sijui ni nani na lini. Lakini kwa wakati huu naishikilia rekodi hii na nina furaha kubwa."

Messi alishinda Ballon d'Or yake ya kwanza mwaka 2009 kabla ya kushinda tena mwaka 2010, 2011, 2012, 2015 na mwaka huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alisema: "Iikuwa ni jambo lisililofikirika kushinda moja na baadaye sita.

"Ni furaha kupata sita, ni jambo zuri kutambulika kwa watu wengine najivunia hilo."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO ATUZWA SERIE A, MESSI AKIBEBA BALLON D'OR

●●● Hii ni tuzo yangu ya sita, ni mwenye bahati sana, nitaendelea kuwa na ndoto...

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Cristiano Ronaldo ametangazwa rasmi kuwa mchezaji bora wa msimu uliopita katika Ligi ya Serie A, ikiwa ni saa chache baada ya mshindani wake, Lionel Messi kumpiku na kuweka rekodi ya kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka ya Ballon d'Or kwa mara ya sita.

**Ronaldo alipotezea kuhudhuria sherehe za kutangazwa mshindi wa Ballon-d'Or zilizofanyika usiku wa kuamkia jana jijini Paris, Ufaransa na badala yake akahudhuria hafla ya kutangazwa Mchezaji Bora wa Msimu wa Serie A ['Gran Gala del Calcio'] zilizofanyika Milan, Italia ambapo alitunukiwa tuzo hiyo kwa mafanikio aliyoipa Juve msimu uliopita.**

Alifunga mabao 21 kwenye ligi katika msimu wa 2018-19 na kuwasaidia 'Bianconeri' kutwaa taji la 'Scudetto' kwa mara ya nane mfululizo na tayari ana mabao sita katika mechi 11 alizoanza msimu huu, licha ya majeraha yaliyomsababishia kukosa muda wa kutosha dimbani mwezi uliopita.

"Ni wakati wa fahari kutwaa tuzo hii," Ronaldo alisema wakati akipokea tuzo, ambayo ilikwenda kwa Mauro Icardi, kipindi akiwa Inter, miezi 12 iliyopita.

"Ninataka kuwashukuru wachezaji wenzangu wa Juventus. Ulikuwa mwaka wangu wa kwanza nikiwa Serie A, ligi ngumu, na ni mwenye furaha sana. Shukrani kwa kunipigia kura.

"Sasa nitajaribu kurudia kile nilichokifanya kwa mwaka ujao."

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Michezo wa Juventus, Fabio Paratici alisisitiza kuwa nyota huyo wa kimataifa wa Ureno- ambaye amemaliza nafasi ya tatu katika kinyang'anyiro cha Ballon d'Or, akiwa nyuma ya kinara Messi na beki wa Liverpool, Mholanzi Virgil van Dijk, ataendelea kubaki Turin zaidi ya mwishoni mwa msimu.

Katika kinyang'anyiro cha Ballon d'Or, ambapo Messi ameitwaa kwa mara ya sita, moja zaidi ya Ronaldo aliyeibeba mara tano, Van Dijk ameshika nafasi ya pili akiwa mmoja kati ya wachezaji wanne wa Liverpool katika saba bora, akiwamo Sadio Mane aliyeshika nafasi ya nne.

Kipa wa Liverpool, Alisson ametwaa tuzo ya kipa bora mbele ya kipa wa Barcelona, Mjerumani Marc-Andre ter Stegen na raia mwenza wa Brazil Ederson anayeichezea Manchester City.

Beki Matthijs de Ligt aliyejiunga na Juve majira ya joto, amempiku mshambuliaji wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho na kutwaa tuzo ya Kopa Trophy, inayotolewa kwa mchezaji kinda bora mwenye umri chini ya miaka 21 na kuchaguliwa na mshindi aliyepita wa Ballon d'Or.

Beki wa England, Lucy Bronze amemaliza nafasi ya pili kwa upande wa Mchezaji Bora wa Kike wa Mwaka, akiwa nyuma ya Megan Rapinoe, ambaye alikuwa Mchezaji Bora ['Golden Ball'] wakati Marekani ikitwaa Kombe la Dunia 2019 kwa mara ya pili mfululizo.

Akizungumzia baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo, ambayo msimu uliopita ilikwenda kwa mshambuliaji wa Real Madrid na Croatia, Luka Modric, Messi alisema: "Leo [juzi] ni Ballon d'Or yangu ya sita. Ni wakati tofauti kabisa, niliishi na familia na watoto wangu.

"Kama mke wangu alivyosema, usiache kamwe kuwa na ndoto lakini mara zote endelea kujizatiti na endelea kufurahia. ni mwenye bahati sana, nimebarikiwa.

"Ninatumai kuendelea kwa muda mrefu. Ninakubali kwamba ni mwenye bahati sana, hata kama siku moja, kustaafu kutagonga. Itakuwa ni vigumu. "Lakini bado nina miaka mizuri mbele yangu. Muda unakimbia sana, hivyo nataka kufurahia soka na familia yangu."

## ZISIKUPITE

### AJITABIRIA KUTIMULIWA

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amewaambia wachezaji wake anaweza kutimuliwa kutegemeana na matokeo ya timu hiyo dhidi ya Tottenham na Manchester City kuelekea mechi hizo mbili zijazo. ***(Sun)***

### KOULIBALY ATEGWA MADRID

REAL Madrid inajiandaa kutoa ofa kwa beki wa Napoli, Msenegal Kalidou Koulibaly, 28, ambaye kwa muda mrefu amekuwa akiwindwa na Manchester United - kuelekea majira ya joto yajayo. ***(Calciomercato)***

### LIVERPOOL YAMRUDIA CAKIR

LIVERPOOL kwa mara nyingine imetuma mashushushu wake kwenda kumtazama kipa wa Trabzonspor, Mturuki Ugurcan Cakir, 23. ***(Mirror)***

### IBRA' KUICHOMOLEA UNITED

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na Sweden, Zlatan Ibrahimovic, 38, anajiandaa kukataa kurudi Ligi Kuu England na kukubali dili la kuitumikia AC Milan. ***(Telegraph)***

### MILAN WAITIWA GIROUD

AC Milan wamepewa ofa ya kumnunua mshambuliaji wa Chelsea, Mfaransa Olivier Giroud, 33. ***(Calciomercato)***

### ERIKSEN ATOA MSIMAMO

KIUNGO wa Tottenham, Mdenmark Christian Eriksen, 27, ameweka wazi kuwa hatasaini mkataba mpya na atakata ushawishi wowote wakumtaka kuendelea kubaki klabuni hapo. ***(Telegraph)***

### ARTETA ANUKIA ARSENAL

BODI ya Arsenal, inamtaka nahodha wao zamani, Mikel Arteta, ambaye kwa sasa ni kocha msaidizi wa Pep Guardiola katika kikosi cha Manchester City, kurithi mikoba ya Unai Emery hapo Emirates. ***(Mirror)***

### ANUSURIKA WEST HAM

MANUEL Pellegrini amejinunulia mwenyewe muda wa kuendelea kuwa kocha wa West Ham baada ya kuiongoza timu hiyo kushinda dhidi ya Chelsea. ***(Mail)***

### POCHETTINO AJIWEKA SOKONI

KOCHA wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino amefungua mlango wa kurudi mzigoni Ligi Kuu England, akifunguka mwenyewe kwamba yupo tayari kurejea uongozini. ***(Fox Sports, via Mirror)***

### HODGSON HAPEPESI KWA ZAHA

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson amesema anahesabu kuendelea kuwa na mshambuliaji wa kimataifa wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, 27, katika klabu hiyo kwa kipindi chake cha mkataba ambao unamalizika mwaka 2023. ***(Sky Sports)***

### ARSENAL, EVERTON VITANI

ARSENAL na Everton, ambayo kocha wao Marco Silva amekalia kuti kavu baada ya kuwa na msimu mbaya, zote zinavutiwa na kocha wa zamani wa Valencia, Marcelino. ***(Mail)***

# Tamasha la Twenzetu Kilimanjaro Fest laja

**Na Mwandishi Wetu**

WENYEJI wa Mkoa wa Kilimanjaro watakaoenda likizo mwaka huu kwa msimu wa sikukukuu, wameandaliwa burudani mbalimbali kwenye tamasha kubwa linalotarajiwa kufanyika Desemba 22 kwenye Viwanja vya Chuo cha Ushirika Moshi.

Tamasha hilo linalojulikana kama 'Twenzetu Kilimanjaro Fest' 2019 limendaliwa na Kampuni ya Real PR Solutions ya jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia tamasha hilo ambalo linatarajiwa kuzinduliwa rasmi hivi karibuni, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Clement Mshana alisema ni sehemu ya mkakati wa kufanikisha Mpango wa Kuendeleza Utalii wa Ndani (Domestic Tourism Promotion Initiative (DTPI) unaotarajiwa kufanyika mikoa mbalimbali nchi nzima kwa kuanza na Mkoa wa Kilimanjaro.

"Tamasha hili la Twenzetu Kilimanjaro Fest linatarajiwa kupambwa na matukio kadhaa ya burudani zikiwamo, Mbio za kujifurahisha za Capital Mountain Run zitakazohusisha kilometa 5, kilometa 10 pamoja na mbio za watoto za kilometa 3 na Mbio za Baiskeli za kilometa 60, maonyesho ya utalii na biashara, burudani na viburudisho mbalimbali ikiwamo michezo ya watoto, vyakula vya asili na muziki," alitaja.

Alisema katika Mkoa wa Kilimanjaro, tamasha hilo hasa litahusisha agenda kuu tatu ambazo ni pamoja na kutangaza utalii wa ndani, upandaji wa miti pamoja na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda katika mkoa huo.

Aidha, katika mkakati wake wa kufanikisha agenda hizo, kampuni hiyo ya Real Pr Solutions imeandaa matukio kadhaa ya kijamii ili kuunganisha wadau mbalimbali wa mkoa huo kama utembeleaji wa vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo mkoani Kilimanjaro ikiwamo, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na maporomoko mbalimbali ya maji yaliyopo mkoani humo.

"Tukio hili la utembeleaji wa vivutio na upandaji miti linatarajiwa kufanyika Desemba 21, mwaka huu yaani siku moja kabla ya tamasha," alisema huku akitaja tukio jingine kuwa ni upandaji wa miti zoezi ambalo litatekelezwa kwa uratibu wa pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) likihusisha wadau mbalimbali ikiwamo mashirika na taasisi za umma ikiwamo shule na vyuo mbalimbali mkoani Kilimanjaro.

Mbali na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), aliwataja baadhi ya wadau muhimu katika ufanikisha tamasha hilo kuwa ni pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

" Wengine ni pamoja na Kampuni ya Ujenzi ya CRJE (East Africa) Limited, HAL, Kilimanjaro Wonders Hotel, Nyumbani Hotels na Afrimax Strategic Partnerships."

# TANZANIA YAIFUMUA UGANDA SITA COPA COCA-COLA AFRIKA

**Mwandishi Wetu,** KENYA

TIMU ya soka ya Copa Coca-Cola Tanzania ya vijana chini ya umri wa miaka 16, imeendelea kufanya vizuri katika mashindano ya Copa Coca-Cola Afrika yanayoendelea mjini Thika nchini Kenya baada ya kuishushia kichapo cha mbwa mwizi Uganda kwa kuichapa mabao 6-2 jana, kwenye mechi ya hatua ya robo fainali.

**Katika mchezo wa awali wa mashindano hayo, Tanzania ilichuana na Afrika Kusini na kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 kisha mechi ya pili kukubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Zambia.**

Michuano hiyo ambayo ni mikubwa barani Afrika inazihusisha timu 10 ikiwa ni pamoja na Kenya ambao ni wenyeji, Zambia, Afrika Kusini, Zimbabwe, Uganda, Ethiopia, Namibia, Angola, Botswana na Msumbiji.

Katika mechi hiyo ya hatua ya robo fainali iliyopigwa juzi, safu ya ushambuliaji ya Tanzania ilikuwa moto wa kuotea mbali ikiongozwa na Paul Nyerere ambaye aliibuka nyota wa mchezo baada ya kufunga hat-trick, huku mabao mengine yakizamishwa nyavuni na Frank Zephania na Kassim Ibrahim.

Mashambulizi ya timu ya Tanzania yalikuwa ni ya kushtukiza huku wakitumia muda mwingi kujilinda kwa mipango dhidi ya Uganda ambao wachezaji wake walionekana kuwa hatari kutokana na ushindi wa mabao 11-1 walioupata dhidi ya Namibia siku ya ufunguzi wa michuano hiyo.

Abel Mtweve, kocha wa timu hiyo ya vijana wa chini ya miaka 16 kutoka Tanzania, baada ya mechi hiyo alisema amepokea sifa kedekede kutoka kwa Watazamaji kwa kuwa na mbinu nzuri za kusaka ushindi.

Kiongozi wa msafara ambaye ni makamu wa Rais UMISSETA, Mwalimu Vitalis Shija, kwa upande wake alisema: "Leo vijana hawa wamenishangaza kwa kuwa sikutarajia kabisa kuifunga timu ya Uganda kwa mabao sita, kwa kweli wameonyesha juhudi na kufuata maelekezo ya mwalimu.

"Kama serikali tupo pamoja na vijana kuwapa moyo kuwa wanaweza na natarajia mchezo wa kesho (leo) dhidi ya Kenya tutaibuka na ushindi na hatimaye kutinga fainali."

Katika mechi nyingine za robo fainali, Kenya itakayokutana na Tanzania nusu fainali, iliichapa Botswana bao 1-0, huku Zimbabwe ikishinda 4-1 dhidi ya Namibia na sasa itakutana na Zambia iliyoichapa Angola 8-1.



Mchezaji wa Timu ya Tanzania ya Copa Coca-Cola, Paul Nyerere (kulia), akimkaba mpinzani wake wa timu ya Uganda, Vincet Mulema katika mechi robo fainali ya Copa Coca-Cola Afrika iliyopigwa jana mjini Thika, Kenya na Tanzania kushinda 6-2. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Waamuzi FA Cup wapigwa Kahama*

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

WAAMUZI wa mechi ya mzunguko wa pili ya michuano ya Kombe la Shirikisho (FA CUP) kati ya Ujenzi FC ya mkoani Shinyanga na Kitayosa FC ya Tabora, wameonja joto ya jiwe baada ya kupokea kipigo kutoka kwa mashabiki kwa tuhuma za rushwa.

Katika mechi hiyo iliyopigwa mwishoni mwa wiki kwenye Uwanja wa Halmashauri ya Mji wa Kahama na kumalizika kwa Kitayosa FC kushinda kwa mabao 2-1, ilishuhudiwa mwamuzi wa kati Sweetberth Martin kutoka Mwanza na washika vibendera Mary Mwakitalima pamoja na Abiud Chakutema wakipokea kipigo kutoka kwa mashabiki ambao walikuwa wakidai fedha zao walizoeleza kuwahonga ili matokeo yaegemee upande wao.

Kipigo kwa waamuzi hao kilianza tu baada ya kumalizika kwa mechi, ambapo mmoja wa mabosi wa Ujenzi FC (jina tunalo), aliwafuata waamuzi hao na kuwataka warejeshe fedha zake alizowahonga kufuatia kushindwa kuisaidia timu yake kuibuka na ushindi.

Hatua hiyo ilisababisha kutokea majibizano kwa dakika kadhaa yaliyoliyowavuta mashabiki wa soka na kuchukua jukumu la kuwashushia kipigo huku wakiwataka kurejesha pesa hizo, ambapo waliamua kukimbilia ofisi za Chama cha Soka Wilaya ya Kahama (KDFA) zilizomo uwanjani hapo kutokana na mechi hiyo kuchezeshwa bila ulinzi wa polisi.

Hata hivyo, hiyo haikuwa dawa ya kukwepa kipigo kwani mashabiki hao waliwafuata huko, huku bosi huyo akishinikiza kurejeshewa fedha zake ambazo alikuwa akieleza kuwa ni kiasi cha Sh. 250,000, huku akimuomba mmoja wa wajumbe wa KDFA, kuwasihi waamuzi hao kuzirejesha.

"Waambie walete fedha zangu hawawezi kunitendea ndivyo sivyo na fedha yangu wamelamba...mimi silalamikii matokeo, walete hela yangu maana hawajaitumikia, "alisema.

# Michezo

Jumatano Desemba 4, 2019

Nipashe




Van Dijk atia neno kukosa Ballon d'Or UKURASA 28

SITA? UMETISHA...



Didier Drogba (kushoto) na mwenyeji wa sherehe ya utoaji tuzo ya Ballon d'Or, Sandy Heribert, wakimpongeza mshindi wa Ballon d'Or 2019, Lionel Messi, wakati akionyesha tuzo sita za kinyang'anyiro hicho alizotwaa kuanzia 2009, 2010, 2011, 2012, 2015 na mwaka huu, juzi jijini Paris, Ufaransa. **HABARI UK. 30**

# *Samatta arahisisha njia kuelekea EPL*

## ●●● Wakala wa Mo Salah amchukua, ni baada ya kuachana na yule wa awali kwa kushindwa...

**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) na klabu ya KRC Genk, Mbwana Samatta, sasa njia ni nyeupe kwake kuelekea kucheza soka Ligi Kuu England baada ya kuamua kumtema wakala wake, Margareth Byrne, kutokana na kushindwa kufanikisha dili hilo la kukipiga EPL.

Aidha, ili kufanikisha mpango huo wa kutua EPL, Samatta tayari amepata wakala mpya, ambapo sasa yupo chini ya Spocs Consulting, ambao pia wanamsimamia Mchezaji Bora wa Mwaka wa Afrika, Mohamed Salah wa Liverpool na beki wa pembeni wa zamani wa Chelsea, Baba Rahman, hao wakiwa ni miongoni tu kati ya wengi.

Mabadiliko hayo yamefanywa rasmi kupitia tangazo kwenye mitandao ya kijamii katika akaunti ya Spoc ambayo ilisomekaa 'Kila la heri kutoka Genk na karibu Mbwana Samatta kwa SPOCS'.

**Huyo anakuwa wakala wa tatu kwa Samatta, 26, ambaye hivi karibuni alichezea klabu ya Simba na kisha TP Mazembe ya DR-Congo kabla ya kutua Genk.**

Awali alikuwa chini ya Sportback Football, inayomilikiwa Nicolas Onisse ambao walifanikisha mpango wake wa kujiunga na KRC Genk.

Na kisha Samatta akaachana na wakala huyo na kujiunga na First For Players mwishoni mwa mwaka uliopita lengo likiwa ni kutaka kutekeleza ndoto yake ya kwenda kucheza Ligi Kuu England.

Byrne, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Sunderland, ambaye Samatta amemtema kwa sasa, ndiye wakala wake wa mwisho kabla ya kuamua kuwa chini ya Spocs Consulting, akitarajia kukamilisha ndoto zake za kucheza EPL kuelekea dirisha la usajili la Januari.

Samatta alikuwa na matumaini ya kukamilisha uhamisho wake wa kutoka Genk kwenda moja ya klabu za England Agosti mwaka huu, kufuatia kuwa na msimu mzuri kwenye Ligi Daraja la Kwanza Ubelgiji, lakini mpango huo ulishindikana.

Msimu uliopita aliiwezesha KRC Genk kutwaa ubingwa huku akitwaa tuzo ya Ebony Shoe, inayotolewa kwa mfungaji bora wa Afrika anayecheza Ubelgiji.

Katika mafanikio yake, pia aliiwezesha Tanzania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri ikiwa ni mara ya kwanza kwa Taifa Stars kushiriki baada ya miaka 39.

Amefunga mabao 20 na kutoa pasi za mwisho sita katika mashindano yote kwa klabu na taifa hadi sasa, huku akitajwa kuwa miongoni mwa wachezaji wanaowania tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Afrika 2019.

# Zahera aitwa Mwandila kufunguka

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Uongozi wa Yanga, ukimuita mezani aliyekuwa Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mwinyi Zahera ili waweze kumalizana, aliyekuwa msaidizi wake, Noel Mwandila amesema kesho naye atafunguka mpango mzima kabla ya kusepa zake Zambia.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Frederick Mwakalebela alisema, pesa wanazodaiwa na Zahera ni za vikwazo vya aina yoyote kwa kuwa kwanza ni haki yake kulipwa.

"Zahera tutamlipa pesa zake kwa sababu ni pesa za kawaida ambazo zinalipika kirahisi naamini kila kitu kitakwenda sawa, yeye aje tu klabuni maana tunasikia yupo jijini lakini hatujaonana.

"Siwezi kuweka hadharani kiasi cha pesa anachodai Zahera kwani hayo ni mambo ambayo yapo baina ya uongozi pamoja na mhusika mwenyewe," alisema Makamu huyo.

Katika hatua nyingine, msaidizi wa Zahera, Mwandila, amesema hana ugomvi na klabu hiyo na kwamba mkataba wake umemalizika jana na anatajia kurudi zake Zambia kwenda kujipanga na mambo mengine.

"Kwa sasa siwezi kusema chochote juu yangu na Yanga kwa sababu mkataba wangu unaisha leo [jana], Alhamisi [kesho] nitakuwa na mengi ya kusema, nitayaweka hadharani," alisema Mwandila.

Aidha, alisema amevutiwa na upendo pamoja na umoja walionao Watanzania katika kipindi chote alichokaa hapa nchini.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >